Jumatano Aprili 10, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579838

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Mtaalamu aeleza faida za mtu kung'atwa na nyuki

UKURASA 2


MAKALA: Ukaribu Uganda, Rwanda kihistoria sasa kuamua hatima ya Rais Kagame
Ukurasa 14

MAFUNZO YA UONGOZI, MAISHA KUTOKA KWA NJELU KASAKA - 1
Ukurasa 18

KIMATAIFA: Ulaya waichoka Uingereza 'kuangukia pua', sasa Aprili 12 hali isipobadilika
Ukurasa 20

siasa
JUMATANO APRILI 10, 2019
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

AIRO: Sitagombea ubunge 2020, ninang'atuka Rorya
Ukurasa 15

Migogoro na changamoto kwa miradi ya EAC

Na Mwandishi Wetu

MOJA ya madhumuni makubwa ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ni kuchagiza kasi ya ukuaji wa uchumi, biashara na ustawi wa maisha ya raia katika nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Jumuiya hiyo kwa mara ya kwanza iliundwa mwaka 1967 ikawa na nchi tatu zilizokuwa wanachama, yaani Tanzania, Kenya na Uganda.

Hata hivyo, ilipofika mwaka 1977, EAC ilivunjika hadi mwaka 1999 kuliposainiwa mkataba wa uanzishwaji wake kupitia wanachama hao hao, ingawa baadaye Rwanda, Burundi na Sudani Kusini ziliongezeka hivyo kuifanya idadi yao kuwa nchi sita.

Licha ya nia nzuri ya kuzileta pamoja nchi hizo za ukanda wa Mashariki mwa Afrika, bado tofauti za kati ya nchi moja na nyingine miongoni mwa zilizo wanachama wa EAC, zinazidi kukua kiasi cha kuhatarisha tena uhai wake.

Ingawa nchi zote na kwa nyakati tofauti zimewahi kuweka wazi dhamira ya kutokuwa tayari kuiona

ENDELEA UK 16

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Balozi Liberat Mfumukeko. PICHA: MTANDAO

UKURASA 13

# Kitendawili ripoti ya CAG kuteguliwa leo

UKURASA 2






Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akikagua Kikosi cha Mbwa na Farasi kilichoweka kambi nje ya maeneo ya viwanja vya Bunge, jana, kuimarisha ulinzi kutokana na tishio la vijana wa vyama vya upinzani kutaka kuandamana kulishinikiza Bunge kufanyakazi na CAG, Prof. Mussa Assad. **PICHA NDOGO:** Gari la maji ya kuwasha likiimarisha ulinzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Rais TLS aibua tena sakata la Tundu Lissu

UKURASA 3

## Ziara ya JPM yamng'oa DED

UKURASA 2

MASUMIN PRINTWAYS & STATIONERS LTD
TOLL FREE: 0800-11-00-24



Build your confidence
Attract more eyes

Promotional Items

BEST OF TANZANIA

Masumin Tower, Jamhuri / Mrima Street, P.O. Box 20073, Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 (0) 626 333 000 / (0) 622 325 488 / (0) 713 325 488
Tel: +255 (22) 2117090, Email: info@masumin.co.tz

www.masumin.co.tz
Masumin printways

215166002

HABARI KITAIFA

## 'Usiogope kung'atwa na nyuki, wanaondoa sumu mwilini'

Na Mwandishi Wetu

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umeeleza kuwa binadamu aking'atwa na nyuki hupata faida nyingi ikiwamo kusaidia kuondoa sumu mwilini.

Ofisa Ufugaji Nyuki kutoka TFS, Rueben Nyambita, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Minaki, wilayani Kisarawe pamoja na Shule ya Sekondari Pugu ya jijini Dar es Salaam.

TFS imeamua kuzungumza na wanafunzi hao kwa lengo la kuwapa elimu wanafunzi inayohusu utunzaji wa misitu, faida za uwapo wake na ufugaji nyuki katika misitu mbalimbali nchini.

"Hata kama mtu ataumwa na nyuki watatu au kumi bado watasaidia kuondoa sumu na iwapo mhusika atavimba sana kuliko kawaida maana yake mwili wake utakuwa na sumu nyingi, hivyo inapokutana na sumu ya nyuki inasababisha mzio," alisema.

Alisema mtu anayeng'atwa anapata faida nyingi katika mwili wake kwa kuondoa sumu iliyopo mwilini na kwamba nyuki huwa na sumu, lakini haina madhara sana kwa binadamu zaidi ya tiba.

"Iwapo binadamu ataumwa na nyuki wengi sana kwa wakati mmoja basi ni rahisi kupata madhara kwa kuwa sumu ya nyuki itakuwa nyingi mwilini, lakini nyuki wachache haina madhara, wanafunzi na wananchi msigope kuumwa na nyuki ni sehemu ya tiba," alisema.

"Asali ya nyuki inatengenezwa na sukari ambayo inaitwa glukosi inayopatikana kwenye mimea mbalimbali, nyuki anapotua kwenye mmea anafyonza maji yake na kuichukua sukari iliyopo mle ambayo ni kati ya asilimia 25 hadi 40. Nyuki wanavimeng'enya vya kutengeneza asali kwa asilimia 75 hadi asilimia 80," alisema.

Kuhusu asali kuganda, Nyambita alisema husababishwa na glukosi ambayo ipo ndani yake na inapokuwa hivyo haimaanishi imeharibika.

Nyambita alisema asali imekuwa na rangi tofauti ambazo zinatokana na mimea ambayo nyuki ameifikia.

"Nyuki anapotengeneza asali, hufanya hivyo kwa ajili ya chakula chake kwa kutumbua kuna nyakati za ukame na njaa, hujiandaa kwa kuwa na chakula cha akiba," alisema.

Nyambita alisema yapo maziwa ya nyuki ambayo ni maalumu kwa ajili ya kulishwa malkia wa nyuki kutokana na jukumu ambalo analifanya kwa nyuki wengine.

"Maziwa ya nyuki yana protini nyingi na kwa mwenye kuyatumia anakuwa na akili nyingi sana na kama ni mwanafunzi atakuwa anafanya vizuri kwenye masomo kwa kushika nafasi za juu," alisema.

# Kitendawili ripoti ya CAG kuteguliwa leo

Na Sanula Athanas, DODOMA

KITENDAWILI cha kuwasilishwa ama kutowasilishwa kwa ripoti ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2017/18, kinatarajiwa kuteguliwa leo zitakapotimia siku saba za mwanzo za mkutano wa kwanza wa Bunge tangu kuwasilishwa kwa ripoti hiyo kwa Rais.

Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais kila taarifa itakayotoa.

Kifungu cha nne (4) cha ibara hiyo, kinaeleza kuwa baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais ataagiza watu wanaohusika wakaiwasilishe taarifa hiyo kwenye mkutano wa kwanza wa Bunge utakaofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika mkutano huo kabla hazijapita siku saba tangu siku ulipoanza mkutano huo.

Juzi, Nipashe ilimuuliza Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwenye Viwanja vya Bunge jijini Dodoma kama ripoti ya CAG imeshawasilishwa bungeni, akaeleza kuwa hana taarifa za uwasilishwaji wake.

Nipashe ilihitaji kujua kama ripoti hiyo imeshawasilishwa bungeni, kwa kuwa serikali inapaswa kufanya hivyo ndani ya siku saba ambazo zinakoma leo.

Endapo serikali haitawasilisha bungeni leo ripoti hiyo, katiba inampa mamlaka CAG kuiwasilisha mwenyewe kwa uongozi wa Bunge.

Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inasema: "Endapo Rais hatochukua hatua ya kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge, basi CAG atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge au Naibu Spika ikiwa Kiti cha Spika kiko wazi au ikiwa kwa sababu zozote Spika hawezi kutekeleza shughuli zake, basi ataiwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge."

Kumekuwa na sintofahamu juu ya uwasilishaji wa ripoti hiyo bungeni kutokana na Bunge kuazimia kutofanya kazi na Prof. Mussa Assad, ambaye ni CAG na ndiye aliyekabidhi ripoti kwa Rais John Magufuli.

Jumanne ya wiki iliyopita, Bunge liliazimia kutofanya kazi na Prof. Assad, baada ya Kamati yake ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumtia hatiani kwa kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya chombo hicho cha kutunga sheria kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwaka akiwa New York, Marekani kwamba anafikiri "huo ni udhaifu wa Bunge".

Tangu kupitishwa kwa azimio hilo, kumekuwa na sintofahamu ya namna ambavyo ripoti ya ukaguzi wa CAG kwa mwaka 2017/18 itawasilishwa bungeni, ikizingatiwa ripoti inayopaswa kuwasilishwa imetiwa saini na Prof. Assad ambaye Bunge limekataa kushirikiana naye.

Hata hivyo, tayari Spika Job Ndugai ameshaweka wazi Bunge liko tayari kufanya kazi na maofisa wengine wa Ofisi ya CAG, lakini siyo mtu anayeitwa Prof. Mussa Assad, ambaye ni CAG na Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mujibu wa katiba.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Dk. Sira Ubwa Mamboya (kushoto), akitembelea miundombinu na mitambo ya mawasiliano inayosimamiwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa kutoka shirika hilo na Wizara ya Mawasiliano Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

# Ziara ya JPM yamng'oa DED

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, Dk. Oscar Mbyuzi.

Kufuatia uamuzi huo, Rais Magufuli amemteua Jimson Mhagama kujaza nafasi hiyo.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, bila kueleza sababu za uamuzi huo.

Rais Magufuli jana aliendelea na ziara yake mikoa ya kusini na kuzindua kiwanda cha kuchakata majani ya chai cha Kabambe kilichopo Mkoa wa Njombe.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Rais Magufuli aliwataka mabalozi wanaowakilisha Tanzania kwenye mataifa mbalimbali wakipata wawekezaji wakazungushwa kwenye taasisi, idara za serikali kwa siku 30, apelekewe majina ya wahusika.

"Mniletee hayo majina ya hao wanaowazungusha wawekezaji na kuwakatisha tamaa na mimi nitawazungusha kama matairi," alisema.

Alibainisha kuwa kuna matatizo maeneo matatu ambayo aliyataja kuwa ni katika mfumo wa kukusanya kodi, matatizo kwa baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na baadhi ya wawekezaji.

"Ndio maana namtaka waziri, watu wasitozwe kodi za kuonewa ambazo zinawakatisha tamaa wawekezaji. Saa nyingine inawakatisha tamaa wawekezaji, baadhi ya watendaji wanamuona mwekezaji kama adui, mbadilike, mtu anakuja kuwekeza kiwanda unamzungusha mwaka mzima, watu wangu wamekuwa na vichwa vigumu sana," alisema.

Alisema wapo wawekezaji ambao walikuwa na nia ya kuwekeza Tanzania, lakini mazingira magumu waliyowekewa na mlolongo mrefu ya urasimu waliamua kwenda Kenya.

"Masharti ya ovyo yamekuwa mengi tunajichewelesha wenyewe wawekezaji wanaipenda Tanzania, waziri na watendaji wengine mbadilike, Kituo cha Uwekezaji (TIC) nimekirudisha Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini nikiona mambo hayaendi vizuri nitakirudisha kwangu, nataka mtu akija kuwekeza leo, aanze kesho kuwekeza siyo mnamzungusha zungusha," alisema.

Pia aliwataka wanaotaka kujenga viwanda wajenge, halafu masuala ya vibali kutoka taasisi mbalimbali za serikali kama Wakala wa Usalama Kazini (Osha), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (Nemc) na michakato mingine itafuata.

Akizungumzia kuhusu kiwanda hicho ambacho kimejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 49.6, Rais Magufuli alisema kinahitaji asilimia 70 ya malighafi, hivyo aliwataka wakulima waongeze uzalishaji.

Pia alikishukuru kiwanda hicho kwa kutoa Sh. milioni 250 kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii.

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli alizitaka mamlaka husika kutengeneza mikakati ya kulinda viwanda nchini.

Alisema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wakati wa utawala wake alipenda viwanda, lakini baadaye havikulindwa na viliuliwa kwa sababu ama ya uongozi mbaya au kuvihujumu.

"Mamlaka husika ikiwamo wizara mhakikishe mnavilinda viwanda, shughulikieni changamoto za viwanda, sekta binafsi msiogope kuingia kwenye ujenzi wa viwanda, wabunge msiogope kuitwa mabepari kama mnataka kuwekeza kwenye viwanda wekezeni kwanza wananchi watawapenda na wataendelea kuwachagua," alisema.

Kuhusu fedha za ujenzi wa barabara kwe-

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Rais mpya TLS aibua sakata la Lissu

**Na Enock Charles**

RAIS wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, ameitaka serikali kufanya uchunguzi wa shambulio la kupigwa risasi kwa Mbunge wa Singida Mashariki (Chadema), Tundu Lissu, ili kujenga imani ya wananchi kwa serikali yao.

"TLS tunadai uchunguzi kamili tena siyo wa juu juu tu na kama hatuwezi sisi tuombe watu wa nje waje watusaidie kuchunguza, siyo aibu, ndiyo maana mataifa mengi wakipata matatizo wanaomba wa nje hii inasaidia kujenga imani ya wananchi juu ya serikali yao," alisema Dk. Nshala.

Dk. Nshala, alinukuliwa akizungumza na chombo cha habari 'online' kuwa kumekuwa kukitokea kesi mbalimbali za watu kutekwa, lakini vyombo vya dola vimekuwa kimya bila kufanya uchunguzi wowote.

"Kuna wengine hapa wamechunguza hata juzi Rais ametoa mfano wa kesi ya MO (Mfanyabiashara Mohamed Dewji), nini kimetokea kwa MO, kuna mambo yanayosikitisha kama Azory, hatufahamu yuko wapi, Ben Saanane, hatufahamu yuko wapi, ee haya mambo siyo mazuri," Dk. Nshala alisema.

Alilitaka Jeshi la Polisi nchini kuacha visingizio vya kukosekana kwa dereva au Tundu Lissu mwenyewe ili kufanya uchunguzi na ikibidi wawafuate huko waliko ili kuwahoji kuhusiana na tukio hilo ambalo ni kubwa na lililoleta hofu nchini.

Alisema vyombo vya usalama havitakiwi kutumia sheria ya nchi kwa matakwa ya mtu fulani wala kumbagua yeyote badala yake vifanyekazi kwa haki na kwa weledi.

Lissu yuko nchini Ubelgiji kwa matibabu baada ya kupigwa risasi na watu wasiojulikana Septemba 7, mwaka juzi karibu na makazi yake wakati akirejea nyumbani akitokea bungeni mjini Dodoma.

Hivi karibuni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alimtaka Lissu arejea nchini kwa madai kuwa mbunge huyo sasa amepona na kwamba hakuna anayeratibu mpango wa kumdhuru.

"Hakuna ambaye anaratibu mpango wa kumdhuru Lissu kwa hiyo usalama wake utalindwa kama walivyo Watanzania wengine," alisema Lugola.

Katika hatua nyingine, Dk. Nshala alisema chama hicho kitazungumzia mgogoro baina ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Bunge ili kuona namna ya kuishauri serikali na Bunge namna ya kushughulikia suala hilo.

"Suala la CAG tutalizungumza sisi wenyewe na kuangalia namna gani ya kuishauri serikali, kulishauri Bunge na hata kukutana na CAG kama inawezekana kuzungumza nadhani ni suala ambalo linatakiwa litatuliwe kwa busara," alisema Dk. Nshala.



Rais John Pombe Magufuli akiwa pamoja na Balozi wa Denmark nchini, Heinar Jensen, pamoja na wadau wa maendeleo wakipiga makofi baada ya kuzindua rasmi Kituo cha Afya Madaba mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**

## ASIMULIA ALIVYONUSURIKA MIKONONI MWA JAMBAZI

**Na Christina Haule, MOROGORO**

DEREVA wa bodaboda, Heryelisha Jonas (25), mkazi wa Mazimbu Manispaa ya Morogoro, amenusurika kifo baada ya abiria aliyempakia kumpiga na kitu kizito kichwani akijaribu kumpora pikipiki.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbord Mutafungwa, tukio hilo lilitokea Aprili 4 saa 3:30 usiku, katika maeneo ya Mazimbu mkoani hapa na kwamba kijana huyo aliokolewa na walinzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), waliokuwa lindoni.

Akisimulia tukio hilo, Kamanda Mutafungwa alisema kijana huyo akiwa eneo lake la kazi alikuja mteja Mkombozi Mdingwe (25), mkazi wa Sabasaba Manispaa ya Morogoro na kuomba apelekwe eneo lijulikanalo kama Take Two.

Alisema wakiwa njiani, mteja wake aliyekuwa na mzigo aliokuwa ameuweka kwenye mfuko wa Rambo, alibadilisha mawazo na kumtaka ampeleke eneo linaloitwa Ipoipo na walipokuwa njiani ndipo alimpiga na kitu hicho kizito kisogoni na kusababisha kuyumba ndipo alipoanza kupiga kelele kuomba msaada.

Kamanda Mutafungwa alisema askari wa Suma JKT walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa akiwa na jiwe kubwa aliloweka kwenye mfuko huo, ambalo alitumia kumpiga dereva huyo wa bodaboda.

Alisema mtuhumiwa huyo anashikiliwa na polisi na anaendelea kuhojiwa na atafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika.

# Zaidi ya watu 300 wajitokeza kupata miguu bandia

**Na Mary Geofrey**

ZAIDI ya watu 300 wamejitokeza kujiandikisha kupata vipimo na miguu bandia inayotarajiwa kutolewa bure katika Taasisi ya Tiba na Mifupa (MOI), ikiwa ni wiki moja tangu kutolewa tangazo hilo.

Hivi karibuni MOI, ilitangaza kushirikiana na Taasisi ya BMVSS ya nchini India kutoa huduma ya vipimo na miguu bandia 600 kwa wenye uhitaji watakaojitokeza mwezi huu.

Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, aliliambia Nipashe kuwa, idadi ya watu wenye kuhitaji waliojitokeza hadi juzi imefikia 300.

"Idadi ya wananchi wanaojitokeza kuandikisha kwa ajili ya kupata miguu bandia hadi leo (jana) asubuhi walikuwa zaidi ya 300 na bado wanaendelea kumiminika, hii inaonyesha ujumbe umewafikia wananchi wengi," alisema Mvungi.

Alieleza kuwa katika kipindi chote cha mwezi huu, watakuwa wanapokea orodha ya watu wenye kuhitaji na kazi ya ugawaji miguu itafanyika mwezi ujao.

Mvungi alisema idadi ya watu wanaopiga simu kuulizia huduma hiyo ni kubwa, hivyo amewataka wenye kuhitaji kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata huduma.

Tangazo la ugawaji wa miguu bandia lilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface na kuwasihi watu wenye kuhitaji kufika kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa, mpango huo ni sehemu ya mkakati wa MOI na serikali wa kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora kwa wakati kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi.

"Ni azima yetu MOI na serikali kuhakikisha huduma zote zinawafikia wananchi hususani wa kipato cha chini, hivyo miguu hii bandia itatolewa bure kwa watu wenye uhitaji, tunafahamu wapo Watanzania wengi ambao walishindwa kupata miguu hii bandia kutokana na kukosa fedha, hivyo tumeona ni vyema tukawaondolea changamoto hii," alisema Dk. Boniface.

Alisema wapo Watanzania wengi ambao wameshindwa kuendelea na maisha yao ya kila siku ya uzalishaji kwa kukosa miguu bandia. "Wapo wenzetu ambao walipoteza viungo na wakakata tamaa wakidhani huo ndio mwisho wa maisha yao, sisi MOI tunawatia moyo kwamba wakipata miguu bandia wanaweza kurudi katika shughuli zao za uzalishaji kama kawaida, hivyo wajitokeze ili waweze kupata miguu," alisema.


## EMPLOYMENT OPPORTUNITIES

China Civil Engineering Construction Corporation(CCECC) is currently offering employment opportunities to suitably qualified individuals on the **Rehabilitation Of Bububu – Mahonda – Mkokotoni Road (31 Km) And Upgrading to Bituminous Standard Three Rural Roads Fuoni – Kombeni (8.582 Km), Pale – Kiongele (4.611 Km) and Matemwe – Muyuni (7.58 Km) Road, Zanzibar.**

Applications are invited from ambitions, energetic and performance driven individuals to fill in vacant position (S) in the table below. Working area is Zanzibar.

| S/N | Position/Specialization | Total Works Similar Experience (Years) | In similar works Experience (Years) | Qualification |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Structure/Drainage Engineer (1) | 10 | 5 | Must be a professional Engineer Registered by ERB |

### How to Apply

**Application for the position must include:**

- Cover letter illustrating your suitable for the position
- Certified copies of academic certificates, Training certificates will be an added advantage.
- Detailed Curriculum vitae showing contact address, emails, mobile phone number (s) and three (3) referees. One being your last employer.

Application will be considered valid if sent (Received before 19th April 2019. Please note that only short – listed candidates meeting the equipment's will be contacted.

Send your application to (ccecc.zanzibar@gmail.com) in MS word or PDF file. Indicate the name of the position on the subject line of your email. For more information contact with this number: **0754855960, Lisa.**

115166202

# Kuelekea uchaguzi: LHRC yatoa angalizo

Na Salome Kitomari

MKURUGENZI wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu nchini (LHRC), Anna Henga (pichani), amefanya mahojiano maalum na gazeti hili na miongoni mwa suala alilozungumzia ni matukio ya vurugu wakati wa uchaguzi mbalimbali zinapofanyika nchini na kutaka vyombo vya dola kutimiza wajibu wao bila kuegemea upande wowote.

Amesema mara kwa mara kunapofanyika uchaguzi nchini, matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu hujitokeza ikiwamo watu kujeruhiwa, kuuawa na kupotea.

Ametoa mfano wa tukio la uchaguzi wa marudio katika Jimbo la Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mwaka jana, ambalo lilisababisha kifo cha aliyekuwa mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam (NIT), Akwilina Akwilini, kwa kupigwa risasi wakati akiwa kwenye daladala.

Kadhalika, kiongozi wa Chadema katika Kata ya Hananasif, kukutwa amefariki katika mazingira ya kutatanisha, huku wananchi wengine wakijeruhiwa na wengine kushindwa kushiriki kupiga kura.

LHRC ni moja wa waangalizi wa uchaguzi unaofanyika nchini na hutoa elimu ya uraia na mpigakura kila mwaka.

Katika mahojiano haya mkurugenzi anafafanua:

**Swali: Tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu mwakani na uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, nini kifanyike ili kusiwe na matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu?**

**Mkurugenzi:** Lazima tutoe elimu ya uraia kwa kiasi kikubwa, mwananchi ajue kuwa uchaguzi siyo vita anapoona mgombea wake kashindwa, akubali matokeo asiende kuchana bendera au ofisi za wenzake.

Lakini wenye mamlaka au dola waone uchaguzi siyo vita, unapotumia polisi au vyombo vya dola kuwapiga wananchi au wanachama wa vyama mbalimbali pia ni kosa.

Tutajitajidi sana tutoe elimu ya uraia ambayo tumeanza sasa kwa njia mbalimbali, na ikifika elimu ya mpigakura na tukapata kibali tutawafikia wananchi wengi zaidi ili wawe na uelewa.

**Swali: Tunapoelekea kwenye uchaguzi, unaviambia nini vyombo vya dola ambavyo mara nyingi vinalaumiwa kutumia nguvu kubwa?**

**Mkurugenzi:** Vyombo vya dola navishauri visiegemee upande wowote wa siasa kwa maana ya upinzani na utawala, wafanye kazi yao kwa mujibu wa haki.



Kazi yao kubwa ni kulinda usalama wa raia na mali zao, unapompiga raia na kumuumiza unakuwa umevunja jukumu lako la kwanza unalotakiwa kufanya.

Wakiacha kufuata upepo wa aina yoyote watatenda haki kwa Watanzania wote, lakini wakifuata itakuwa shida kwa sababu watawaumiza wanaotakiwa kuwalinda.

**Swali: Kumekuwa na matukio ya watu kupigwa risasi na watu wasiojulikana, kupotea, kujeruhiwa. Je, unalizungumziaje?**

**Mkurugenzi:** Kama watu wa haki za binadamu tumekuwa tukilisema sana hili suala kuwa ukuaji wa matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu Tanzania unazidi kukua na unaiweka Tanzania kwenye nafasi mbaya duniani.

Katika jamii ya Umoja wa Mataifa tuna nafasi mbaya, hebu fikiria mtu anapotea tu umeamka asubuhi ndugu yako humpati, hujui yuko wapi, hujui yuko hai, hujui kafa, hujui ulie msiba au ufanye nini au katekwa atarudi, bora iwe ulimzika sehemu fulani unaona kaburi lake, lakini wakati wa uchaguzi watu wanapigwa na wanaumizwa, hili haliko vizuri kabisa.

Tunaona utawala wa sheria umekuwa mgumu sana kwa kuwa watu wananyimwa dhamana bila sababu na ni haki ya kisheria, mwanafunzi Akwilina alifariki akiwa siyo mwanasiasa na hakuwa kwenye masuala ya kisiasa, lakini yote yalikuwa ni matokeo ya nguvu kutumika kupita kiasi.

Haya yote yamekuwa hivi kutokana na mazingira yaliyowekwa yanayovunja haki za binadamu na sisi kama watu wa haki za binadamu tunaona ni jambo baya na hatutaacha kusema pale tunapoona mambo yanazidi kushuka.

**Swali: Unafikiri kwa kusema kwenu kumekuwa na mabadiliko yoyote?**

**Mkurugenzi:** Tumeona kumekuwa na mabadiliko ambayo wakati mwingine wavunjaji wa haki wanakuwa wakali wanasema hawa wanaharakati wanaongea sana, wanaungana na wapinzani na hata kutupa majina, lakini ukiangalia kwenye vitendo unaona kuna vitu vimebadilika.

Wakati wa kifo cha Akwilina tuliongea sana na baada ya muda tuliona mabadiliko sehemu mbalimbali ikiwamo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) na vipigo vya polisi dhidi ya raia kwenye chaguzi zilizofuata havikutokea.

**Swali: Tanzania imesaini mikataba na kuridhia matamko mbalimbali ya haki za binadamu. Je, inatekeleza?**

**Mkurugenzi:** Kwa kiasi fulani inafuata na kuheshimu, kwa mfano mkataba wa haki za mtoto ambao umeingia katika sheria za nchi na kuna sera mbalimbali zimetungwa.

Ukiangalia bado kuna changamoto kama ndoa za utotoni ambazo bado hazijakatazwa na sheria, waliopata ujauzito kurudi kuendelea na shule imekuwa changamoto.

Tanzania imeendelea kuwa miongoni mwa nchi 16 za Afrika zilizokataa kutia saini na kuridhia mkataba wa Umoja wa Afrika unaohusu demokrasia, mikataba ya kidemokrasia na utawala bora (ACDEG), kujitoa kwenye demokrasia maana yake hutaki demokrasia.

Kuna mikataba ya kidemokrasia hatuifuati vizuri, mikataba ya haki za binadamu, mikataba ya upatikanaji wa taarifa na habari kiasi cha taasisi za habari na kutetea haki za binadamu kufungua kesi Mahakama ya Afrika Mashariki, ambayo imeamua kuwa Sheria ya Huduma kwa Vyombo vya Habari kufanyiwa marekebisho.

Machi 28, mwaka huu, Mahakama ya Afrika Mashariki, ilisema baadhi ya vipengele vya sheria hiyo vinakiuka uhuru wa kujieleza na vinapingana na mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao Tanzania imeridhia.

Tanzania inakwenda kinyume na mkataba wa Afrika Mashariki kwenye vyombo vya habari, inaonyesha wazi tuna safari ndefu na iwapo mikataba hiyo ingefuatwa kazi ingekuwa ndogo.

**Swali: Unafikiri kwanini viongozi hawaifuati au kuheshimu mikataba licha ya kuifahamu vyema na kuiridhia?**

**Mkurugenzi:** Nafikiri ni utamaduni wa kuona haki za binadamu siyo kitu cha msingi, kwa sababu utasikia viongozi wanasema tunataka tuboreshe huduma fulani, lakini masuala ya haki za binadamu ni baadaye.

Wanafikiri haki ni kitu tofauti, kumbe binadamu anaenda na haki yake, zipo kabla hajazaliwa, amezaliwa na amekufa, huwezi kumtenga binadamu na haki ndiyo maana huruhusiwi kutoa mimba kwa kuwa kabla hajazaliwa ana haki zake, akifariki kama ameacha urithi unaheshimiwa kwa kuwa ni haki.

Wanaominya wanafikiri haki iko pembeni na ubinadamu uko pembeni, jambo ambalo siyo sahihi kabisa.

**Swali: Tanzania imetajwa kama nchi ambayo wananchi wake hawana furaha duniani, je, nini kimeifikisha Tanzania kwenye nafasi hiyo?**

**Mkurugenzi:** Wanasema ili upinge utafiti lazima ufanye utafiti tunajua waliosema Tanzania iko nyuma kwenye furaha wametumia vigezo gani?

Mimi naona furaha huwezi kuielezea, kwa furaha yako inaweza isiwe furaha yangu na huzuni yangu inaweza isiwe huzuni yangu.

Ninachojua Tanzania ni miongoni mwa nchi maskini kwa kuwa kuna watu wanaishi chini ya dola moja kwa siku, kwamba kuna wenye familia, lakini hawana Sh. 2,000 kwa siku, hivyo umaskini unaweza kuwa ni sababu.

Umaskini ni suala la haki za binadamu kwa kuwa kuna haki ya rasilimali, kuwa na kipato, haki ya kuendelea, ingawa masuala ya maendeleo yanaathiri watu kwa upana na siyo mtu mmoja mmoja.



# Uchaguzi mdogo madiwani Mei 19

Na Mwandishi Wetu

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza uchaguzi mdogo wa madiwani kwenye kata zilizopo kwenye halmashauri sita katika mikoa sita ya Tanzania Bara.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji wa Rufani Semistocles Kaijage, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa uchaguzi huo utafanyika Mei 19, mwaka huu.

Akisoma taarifa kwa umma iliyotolewa na Tume, Jaji Kaijage, alisema fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa Aprili 15 hadi 19, mwaka huu.

Jaji Kaijage alisema uteuzi wa wagombea utafanyika Aprili 19 na kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia Aprili 10 hadi 18, mwaka huu.

Alifafanua kwamba uchaguzi katika kata hizo, utafanyika sambamba na uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

Kiti cha ubunge cha Arumeru Mashariki kiko wazi baada ya aliyekuwa mbunge wake, Joshua Nassari, kukosa sifa za kuendelea kushikilia nafasi hiyo kutokana na kushindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya bunge kama kanuni zinavyosema.

"Tume inapenda kuvikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha uchaguzi huu mdogo," alisema Jaji Kaijage.

Awali Jaji Kaijage alisema uamuzi wa kutangaza uchaguzi kwenye kata hizo umefanyika baada ya tume kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 aliiarifu tume juu ya uwapo wazi wa nafasi hizo.

Alisema nafasi hizo wazi zimetokana na vifo vya madiwani watano (5) na mmoja kujiuzulu.

Kata hizo ni za Uwanja wa Ndege (Mpanda mkoani Katavi), Kitobo (Missenyi mkoani Kagera), Kyela (Kyela mkoani Mbeya, Mikocheni Manispaa ya Kinondoni (Dar es Salaam), Mvuleni (Lindi) na Manda Chamwino mkoani Dodoma.

**"Tume inapenda kuvikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha uchaguzi huu mdogo," alisema Jaji Kaijage.**


## Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

**MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2018**

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

### WARAKA WA MIZANIA
Kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka Uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 849 | 1,126 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,585 | 7,153 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 49,487 | 46,814 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 16,109 | 304 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,737 | 41,524 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 69,993 | 74,231 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,905 | 2,444 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Kodi iliyoahirishwa | 299 | 351 |
| 16 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,267 | 386 |
| 17 | **JUMLA YA MALI** | **156,230** | **174,333** |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 18 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 50,067 | 65,697 |
| 19 | Amana za Wateja | 68,764 | 70,280 |
| 20 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 21 | Amana Maalumu | 22 | 170 |
| 22 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 23 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 44 | 67 |
| 24 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,224 | 2,456 |
| 25 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 26 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 27 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 28 | Dhima Nyingine | 905 | 1,363 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **122,028** | **140,034** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **34,203** | **34,299** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,341 | 3,215 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 6,123 | 4,263 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,484 | 4,233 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 755 | 1,088 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **34,203** | **34,299** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 5,978 | 6,057 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,967 | 6,971 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,361 | 1,251 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 21.89% | 19.67% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.96% | 9.24% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 60.04% | 55.44% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 44.80% | 42.58% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.51% | 93.25% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -12.61% | 5.13% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -10.38% | 6.42% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
Kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31 Desemba 2018 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2017 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 13,547 | 15,221 |
| 2 Gharama za Riba | (5,488) | (5,596) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **8,059** | **9,625** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (945) | (885) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,077** | **1,357** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 234 | 418 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 839 | 938 |
| 6.3 Gawio | 3 | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,541)** | **(4,037)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (1,540) | (1,498) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (172) | (65) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,830) | (2,473) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,649** | **6,060** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (1,165) | (1,827) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,484** | **4,233** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **2,484** | **4,233** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 29 | 31 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 116 | 197 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.21% | 4.01% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7.25% | 15.39% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 31.05% | 24.35% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.57% | 7.01% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
Kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31 Desemba 2018 | Mwaka uliopita 31 Desemba 2017 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 3,649 | 6,060 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali nyinginezo | 36 | 82 |
| | - Hasara Katika Mali | 224 | 59 |
| | - Mikopo iliyofutwa | (2,151) | |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 4,237 | (3,287) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (3) | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (17,145) | 8,300 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (4,743) | 593 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (467) | (1,620) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 845 | (1,275) |
| | -Mabadiliko Halisi mikopo ya muda mrefu itolewayo na mabenki mengine | 2,676 | (68) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (1,625) | (1,959) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(14,467)*** | 6,885 |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (989) | (95) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (29) | (28) |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 5 | 4 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(1,014)*** | ***(120)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | | |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (645) | (538) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(645)*** | ***(538)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | (16,126) | 6,228 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka / Mwaka | 58,311 | 52,083 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka / Mwaka** | **42,185** | **58,311** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI
Kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | 21,500 | - | 8,496 | 3,215 | 1,088 | - | **34,299** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,484 | - | - | - | **2,484** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (430) | - | - | - | **(430)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,943) | 2,277 | (333) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (mikopo iliyofutwa) | - | - | - | (2,151) | - | - | **(2,151)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2018** | **21,500** | - | **8,607** | **3,341** | **755** | - | **34,203** |
| **Mwaka uliopita 2017** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2017** | **21,500** | - | **6,515** | **1,672** | **1,024** | - | **30,711** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 4,233 | - | - | - | **4,233** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (645) | - | - | - | **(645)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,543) | 1,543 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (64) | - | 64 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2017** | **21,500** | - | **8,496** | **3,215** | **1,088** | - | **34,299** |

**BANK OF INDIA (TANZANIA) LTD**
**DAR ES SALAAM**

**Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Mr. Ashwani Kumar Negi**<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | **Imesainiwa** | **29.03.2019** |
| **Mr. Poncian B. Katesigwa**<br>**Mkuu wa Fedha** | **Imesainiwa** | **29.03.2019** |
| **Mr. Allen Richard**<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | **Imesainiwa** | **29.03.2019** |

**Hapo juu ni baadhi ya taarifa kutoka katika taarifa ya fedha ya benki kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31. Desemba 2018, na zimeandaliwa kwa kulingana na sera za kimataifa (IFRS).**

**Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa Baker Tilly DGP & CO na zimepata hati safi.**

**Taarifa hii ya fedha imepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi na imesainiwa na wakurugenzi wafuatao kwa niaba ya wenzao**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **1. Mr. Fredrick Mbala- Mkurugenzi** | **Imesainiwa** | **29.03.2019** |
| **2. Mr. S.K Mukherjee - Mkurugenzi** | **Imesainiwa** | **29.03.2019** |

115167802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vifo hivi viwe janga la kitaifa

**KATIKA** mambo ambayo yanawanyong'onyesha wanawake ni vifo vinavyotokea kwa sababu zinazohusiana au kuhusishwa na uzazi.

Leo kati ya wanawake 100,000 wanaojifungua takribani 558, wanapoteza maisha, inatokea mama anafariki wakati wa kujifungua au baadaye, lakini yote hayo yakitokea ndani ya siku 40 baada ya uzazi.

Idadi kubwa ya vifo vinaelezwa kuwa vinatokana na matatizo ambayo yangeweza kudhibitiwa. Changamoto hizo ni kukosa dawa, kukosekana vituo vya afya, wahudumu, umbali wa kufikia huduma, lakini pia kuendekeza mila potofu ikiwamo kutumia dawa za asili kuchochea uchungu na kuongeza njia ya uzazi.

Wanawake wengi hufariki kutokana na kuvuja damu nyingi, maambukizi mbalimbali, malaria, uchungu pingamizi, kupasuka mfuko wa mtoto pia utoaji mimba unaofanywa kienyeji mitaani.

Kwa ujumla vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi havikubaliki. Si jambo la kupuuzwa ni kitu kinachoumiza na kukatisha tamaa ni kama unapobeba mimba ni kama kujitia kitanzi.

Cha kushangaza siku za nyuma vifo vilipungua vikishuka hadi wanawake 460 katika kila vizazi hai 100,000, lakini leo vimefikia watu zaidi ya 550. Hili ni janga la kitaifa.

Kama ambavyo baadhi ya magonjwa kama VVU na Ukimwi vilitajwa kuwa janga la kitaifa ni wakati sasa wa kuwatangazia wananchi kuwa vifo vya wazazi ni janga la kitaifa.

Tunaamini hatua hiyo italeta msukumo mpya na mikakati kabambe ya kuikabili. Kwa maana hiyo, serikali itaweka mikakati na bajeti ya kutosha kama ilivyoweka kuzuia maambukizi mapya ya VVU, kutoa dawa za kufubaza makali na kuwalinda watoto wachanga wasiambukizwe.

Tunaona kuwa ni muda wa kuweka mikakati ya kuwaokoa wanawake wasiangamie kwenye uzazi. Tunataka kuona vikianzishwa vyombo vya ulinzi, ufuatilia na usimamizi wa afya na usalama wa wajawazito vijijini na mijini.

Ni muda wa kutenga bajeti ili ufuatiliaji umtambue mjamzito, anahudhuria kliniki, anaishi maisha gani na iwapo anahitaji msaada tena ufahamike ni wa namna gani.

Taarifa hizo zikifahamika kwenye ofisi za vijiji, zahanati, vituo vya afya vya kata, kwenye hospitali za wilaya na za rufani itakuwa rahisi kuandaa bajeti, wataalamu, dawa, vitendea kazi na miundombinu ya kuwahudumia wajawazito ili kupunguza vifo.

Tunaona kuwa pamoja na kutoa elimu na kuanzisha kampeni nyingi na programu za kila aina, haitakuwa na tija kama hatutachukua hatua kufuatilia hali za wajawazito mitaani na vijijini na kuwasaidia.

Tunaamini kuwa iwapo kutakuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara unaofanywa na kamati za afya za wajawazito za kijiji na mitaa mijini, itakuwa rahisi kumgundua mama anayesumbuliwa na malaria mara kwa mara.


Aidha, itakuwa rahisi pia kumhudumia, iwapo ana matatizo ya damu kwa kuwa taarifa zake zitafikishwa kwenye zahanati na wataalamu kutoka vituo vya afya vya kata na hospitali za wilaya zitamfuatilia pia.

Kamati za afya za wajawazito mitaani na vijijini zitakuwa na jukumu la kuwatambua na kuanzisha mchakato wa kuwahudumia mara moja wanawake wenye dalili hatari za ujauzito kama kutokwa damu, kuumwa anemia, shinikizo la juu la damu, kuvimba sana na kusumbuliwa na malaria.

Shime, hatua zichukuliwe kwa matendo na si kuongea kwa kuwa maelfu ya wanawake hufa kila siku na huenda namba ya vifo ikifikia 1,000 kwa vizazi hai 100,000.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Shule ya Msingi Nata imeonyesha njia, iigwe

**UTORO** wa baadhi ya wanafunzi kwa shule za msingi na sekondari ni moja ya changamoto nchini ambayo kwa namna moja au nyingine inafanya wanafunzi hao washuke kitaaluma wakati mwingine.

Kuna baadhi ya mikoa ambayo imewahi kutajwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ikiwamo ya Tabora, Geita, Mtwara na Shinyanga, kwa shule zake kuongoza katika suala hili la utoro.

Mikakati mbalimbali ya kukabiliana na kadhia hii imekuwa ikichukuliwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha dawati la wanafunzi watoro shuleni lenye jukumu la kuwafuatilia ili kuhakikisha wanahudhuria masomo.

Miongoni mwa shule zilizoanzisha madawati hayo ni Shule ya Msingi Nata iliyopo wilayani Nzega Mkoa wa Tabora.

Dawati lake limesaidia kupunguza utoro na mahudhurio kuongezeka kutoka asilimia 60 hadi 90.

Kwa mujibu wa mjumbe wa kamati ya shule hiyo Masoud Twaib, dawati hilo hukutanisha wazazi, watoto wao na walimu hatua ambayo imeleta ushirikiano uliowezesha kurudisha wanafunzi watoro shuleni kwa asilimia kubwa.

Muungwana anaona kwamba hatua hiyo ni muhimu ili kukabiliana na tatizo hilo, linaloonekana kuwa sugu kwenye baadhi ya shule hapa nchini, hivyo si vibaya shule nyingine zikaiga mfano huo.

Iwapo utaratibu huo utaendelezwa utasaidia kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi na hatimaye kutimiza ndoto walizojiwekea kwa ajili ya maisha yao ya baadaye.

Ikumbukwe kuwa dhamira ya serikali ni kuwashirikisha wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo kuwekeza katika elimu na kuzalisha raslimali watu yenye ujuzi na stadi zitakazowezesha kuchochea mapinduzi ya viwanda ili nchi iwe ya uchumi wa kati ifikapo 2025.

Kwa maana hiyo ili kufikia hatua hiyo ni muhimu kukomesha vitendo vya utoro ambavyo vimekuwa vikifanywa na baadhi ya wanafunzi kwa sababu zozote zile.

Serikali inatambua ili kuwa na maendeleo ya uchumi, ni lazima kujenga jamii inayoheshimu na kufuata misingi ya uwajibikaji, ubunifu pia kujenga taifa lenye amani na utulivu, msingi wake mkuu ukiwa ni uwekezaji zaidi katika elimu.

Tayari imeonyesha nia ya kuwekeza kwenye elimu kwa kuruhusu wanafunzi wa shule za msingi hadi kidato cha nne kusoma bila ada, hivyo ni fursa kwao kuichangamkia badala ya kuendekeza utoro.

Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inaweka wazi kwamba moja ya mahitaji ya msingi ya mtoto ni elimu, lakini baadhi yao wamekuwa hawathamini haki hiyo kwa kuendekeza utoro, hali ambayo mwisho wao kitaaluma si mzuri.

Mbali na utoro unaohusisha wanafunzi wa jinsia zote, lakini upo pia unaohusisha wa kike ukisababishwa na mimba za utotoni ambazo mwisho wake huwa ni kukatisha masomo.

Tanzania imewahi kutajwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika utafiti wake uliochapishwa Januari mwaka 2016, kwamba ni nchi ya tatu barani Afrika kwa matukio ya ndoa na mimba za utotoni kwa asilimia 28.

Sasa inawezekana katika mazingira haya wapo wanafunzi ambao wamekatisha masomo na wengine kuwa watoro na kushindwa kunufaika na moja ya haki zao za msingi ambayo ni elimu.

Kwa upande wake Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), linasema kwa wastani watoto wa kike wawili kati ya watano huolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 ikiwa ni mwendelezo wa kukosa elimu.

Sababu kuu zinazotajwa kuchangia kukua kwa tatizo hili ni desturi na mila potofu, sheria na sera kinzani, mifumo dhaifu ya uongozi katika ngazi ya kata, vijiji, mitaa hadi kwenye vitongoji.

Utoro shuleni ni tishio kwa mwanafunzi, kwa sababu linamfanya asitimize ndoto zake.

Sasa kila mmoja asijiweke pembeni bila kushiriki katika mikakati ya kuudhibiti kwa kuunga mkono kwa dhati hatua ya kuanzisha madawati ya utoro shuleni kama ilivyofanya Shule hiyo ya Msingi Nata wilayani Nzega.

HABARI KITAIFA

# TADB, TIRDO kuwezesha wakulima, wasindikaji

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Kilimo Tanzania (TADB) na Shirika la Utafiti wa Viwanda na Maendeleo (TIRDO), zimekubaliana kushirikiana kuviendeleza vyama vya wakulima na wasindikaji wa mazao ya kilimo, ili kuchochea kilimo biashara, usindikaji mazao na kupunguza umaskini.

Makubaliano hayo yalifikiwa kupitia mkataba ambao ulisainiwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine na Mkurugenzi Mkuu wa TIRDO, Prof. Mkumbukwa Mtambo (pichani), jijini Dar es Salaam.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kisheria cha TADB, Neema John, alieleza kuwa mkataba huo unatoa msingi imara na mwanya mpana wa taasisi hizo kushirikiana katika kutambua matatizo na mahitaji halisi ya vyama vya wakulima na wasindikaji mazao na kuyapatia ufumbuzi.

Aidha, kupitia mkataba huo, wafanyakazi wa Benki ya Kilimo watanufaika kwa mafunzo yanayohusu mambo tofauti katika kuendesha miradi ya viwanda vya kusindika mazao ya kilimo.

John alieleza kwamba taasisi mbili hizo zina majukumu yanayolandana katika kuwahudumia wakulima, kuinua kilimo na kuendeleza viwanda vya kusindika mazao ya wakulima, hivyo mkataba huo umezipa taasisi zao msingi kujadiliana, kuratibu na kutekeleza shughuli zinazohusu ustawishaji wa miradi ya viwanda vya kusindika mazao.

"Makubaliano haya yanatupa msingi mzuri wa kuwa na ushirikiano wa maana na endelevu baina na mshirika yetu mawili. Huu ni mkataba mzuri na tunauthamini sana," alifafanua.

Alisema mkataba huo unazipa nafasi taasisi zao kuanzisha mtandao na kanzidata utakaokuwa na taarifa na takwimu za kutosha juu ya mazao na viwanda vya usindikaji mazao ili zisaidie kufanya maamuzi sahihi katika ngazi za utekelezaji miradi na kutunga sera.

Kadhalika, alisema kwa mkataba huo, taasisi hizo zinajifunga kwa ahadi ya kuhakikisha vyama vya wakulima, wasindikaji mazao na wadau wengine wa kilimo wananufaika vilivyo kutokana na huduma zinazotolewa na taasisi hizo.

TADB ina jukumu la kutoa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu ili kuendeleza kilimo na kuinua uchumi wa taifa, wakati TIRDO ina jukumu la kufanya utafiti ili iwe rahisi kuchambua vitendea kazi au malighafi za ndani na kubuni teknolojia zinazofaa katika kuanzisha shughuli za viwanda.

# Kortini tuhuma kuchapisha picha za ngono mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

WATU watano akiwamo mfanyakazi wa benki, William Kimaro (35), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashtaka matano ya kuchapisha picha za ngono kwa njia ya mtandao kupitia kurasa zao za WhatsApp.Washtakiwa wengine ni Oscar Mariselian (30), Don Godfrey (36), Feisal Mohammed (37) na Abdurhaman Muhidin (34).Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mmbando.

Wakili wa Serikali, Jenifer Masue, alidai kuwa Aprili 4, 2016, Oscar alichapisha picha za ngono kupitia ukurasa wake wa mtandao wa jamii wa WhatsApp.

Katika shtaka la pili mpaka la tano, ilidaiwa kuwa Aprili 5, 2016 washtakiwa Godfrey, Kimaro, Mohammed na Muhidin walichapisha picha za ngono kupitia kurasa zao za mtandao wa jamii wa WhatsApp.

Masue alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, lakini akadai kuwa upande wa Jamhuri hauna pingamizi la dhamana.

Hakimu alisema kila mshtakiwa anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua inayotoka taasisi inayotambulika atakayetia saini bondi ya Sh. milioni tano.

"Sitaki barua na vitambulisho vya kughushi wala barua ya serikali ya mtaa," alisema Hakimu Mmbando wakati akisisitiza masharti ya dhamana.


TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII - TASAF

KITENGO CHA HUDUMA KWA MTEJA.

**Mfuko wa maendeleo ya jamii - TASAF** unapenda kuwajulisha walengwa wake, wadau na wananchi wote kwamba imeanzisha kitengo cha huduma kwa mteja.

**Huduma hii inapatikana kupitia namba +255 22 2190200 na 0739 000038 siku za Jumatatu hadi ijumaa kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 2:00 usiku.**

ESTABLISHMENT OF A CALL CENTER

**Tanzania Social Action Fund (TASAF)** wishes to inform its beneficiaries, stakeholders and the general public on establishment of a call center.

**The call center is reachable through telephone number +255 22 2190200 and 0739 000038 on week-days (Monday to Friday) from 8:00 to 20.00**

Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF
Jengo la PSPF, Ghorofa ya nne
Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete
S.L.P 2719
DODOMA

Simu: + 255 026 2963866
Nukushi: +255 026 2963871
Barua pepe: info@tasaf.go.tz
Tovuti: www.tasaf.go.tz

215167402




# Ziara ya JPM

INATOKA UK 2

nye mashamba ya chai, alisema atazifuatiliwa kujua kama zinaendelea kutolewa kwa sababu zilikuwa zinatolewa na Umoja wa Ulaya (EU).

Akizungumzia kodi kwenye vinywaji kama bia na konyagi, Rais alisema lina utata ndiyo maana Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda hakuzungumza serikali ilikuwa inakusanya kiasi gani cha kodi mwanzoni.

"Angezungumza hilo kwamba kabla ya kugonga stempu tulikuwa tunakusanya ngapi, tungepata jibu vizuri, tulikuwa hatukusanyi fedha, katika eneo ambalo tumepigwa sana ni hilo la vinywaji."

"Walikuwa wanavileta vinywaji, palikuwa na stempu ambazo hapa Tanzania zilikuwa zinatengenezwa, kuna wakati zilikamatwa zenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 10, wakapewa wenye viwanda, wakishirikiana na TRA," alisema.

Alisema wapo wafanyakazi wa TRA ambao walikuwa wanazichapisha stempu kisha wanaziuza kwenye viwanda vya vinywaji vikali na kusababisha serikali ikose fedha.

"Ndiyo maana serikali ikakaa na kutafuta utaratibu mzuri ili hawa wenye viwanda tusipoteze fedha ,zaidi zikatengenezwa zabuni, zikatafutwa kampuni, ukileta kampuni ikafuatilia mtambo wa kutengeneza spiriti inayotengenezwa kiwandani," alisema.

Alisema kifaa hicho ndicho kinachowezesha serikali kukusanya kodi kwa sababu kinawasaidia kujua kampuni husika imetengeneza vinywaji kiasi gani.

Alisema hata kwenye mfumo wa kukusanya mapato kwa kutumia mashine za kielektroniki EFD upo mchezo mkubwa unaochezwa ndiyo maana mtaalamu wa E-Government alikaa kutengeneza programu nyingine.

Awali, Rais Magufuli alizindua Kituo cha Afya cha Madaba kilichopo Ruvuma na kuagiza halmashauri nchini kuhakikisha fedha za sekta ya afya zinapotolewa zitumike eneo hilo.

Pia aliwashukuru wadau wa maendeleo kutoka Canada, Uswis, Denmark, Korea na kwinginepo kwa kuendelea kuisaidia Tanzania.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas (kushoto), akisisitiza jambo kwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, baada ya kukitembelea Kituo cha Abood Media, kilichopo mkoani Morogoro hivi karibuni. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**






# Shahidi kesi ya Malinzi adai nyaraka benki zilighushiwa

**Na Hellen Mwango**

OFISA Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Sosthenes Kiwengo (44), amedai mahakamani kwamba muhtasari wa mkutano wa Kamati ya Utendaji wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) wa Juni 5, 2016 uliowasilishwa benki ya Stanbic ulioonyesha agenda ya kubadilisha watia saini, ulighushiwa.

Kadhalika amedai kwamba muhtasari halali wa mkutano huo haukuwa na agenda ya kubadilisha watia saini wa TFF.

Kiwengo alitoa ushahidi huo jana mbele ya Hakimu Mkazi Kasonde Maira, anayesikiliza kesi ya kutakatisha Dola za Marekani 173,335 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu dhidi ya Rais wa zamani wa TFF, Jamal Malinzi na wenzake wanne.

Kiwengo ambaye ni Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, alidai kuwa majukumu yake ni kuchunguza tuhuma mbalimbali zinazohusu rushwa.

Alidai kuwa alipewa kazi na Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru kuchunguza tuhuma za kughushi nyaraka zilizotumika kubadilisha watia saini benki ya Stanbic.

"Nilianza kwenda benki, nikaomba nyaraka zilizotumika kubadilisha watia saini akaunti sita za TFF. Nilipozichambua nyaraka hizo nilibaini kulikuwa na muhtasari wa Kamati ya Utendaji wa Juni 5, 2016 na miongoni mwa agenda walizojadili ikiwamo kubadilisha mtia saini kutoka Edger Masoud na kuwa Nsiande Mwanga," alidai.

"Sikuishia hapo nilikwenda TFF nikaomba nyaraka za mkutano wa Juni 5, 2016, nilipozipitia niliona muhtasari wa mkutano huo na kwamba miongoni mwa agenda zilizojadiliwa na Kamati ya Utendaji hakukuwa na agenda ya kubadilisha watia saini," aliongeza.

Akifafanua zaidi alidai kuwa katika muhtasari wa benki, idadi ya wajumbe waliohudhuria walikuwa 20 na sekretarieti wanane wakati ule alioupata TFF walikuwa 18 na sekretarieti sita, hivyo kuonyesha tofauti japo tarehe ya mkutano ilikuwa moja.

Shahidi huyo wa 13 wa Jamhuri aliendelea kudai kuwa baada ya kupitia nyaraka hizo, aliwahoji wajumbe wa Kamati ya Utendaji na Sekretarieti pamoja na watumishi wa benki.

Alidai kuwa alibaini nyaraka za kubadilisha watia saini ziliwasilishwa benki ya Katibu Mkuu wa zamani wa TFF, Selestine Mwesigwa.

Akiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Leonard Swai, alidai kuwa uchunguzi wake ulibaini nyaraka zilizowasilishwa benki zilighushiwa na kwamba zilitiwa saini na vigogo wawili, Mwesigwa na Malinzi.

Alidai kuwa kwa ufahamu wake walioandaa nyaraka hizo moja kwa moja wanahusika na kughushi. Hakimu alisema ushahidi wa Jamhuri utaendelea Aprili 17, mwaka huu.

Mbali na Malinzi Mwesigwa na Mhasibu wa TFF, Mwanga, wengine ni Meneja wa Ofisi ya TFF, Miriam Zayumba na Karani wa TFF, Flora Rauya, ambao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walikula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wanaendelea kukaa rumande kwa sababu wanakabiliwa na mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.

HABARI KITAIFA

# Sera ya Taifa ugatuaji madaraka kuwa na meno

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

SERIKALI imesema Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka ya mwaka 2019 ambayo ipo katika hatua ya rasimu itakapokamilika itakuwa na nguvu ya kisheria na kisera tofauti na ile ya mwaka 1998 ambayo haikuwa na nguvu ya kisheria.

Hayo yalielezwa mjini Masasi, mkoani Mtwara na Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Kisheria kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Edwin Mgendera, baada ya kufunguliwa kwa kikao kazi cha kupokea maoni ya wadau juu ya Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka ya mwaka 2019 kwa wananchi wa mikoa ya kusini ya Mtwara, Lindi na Ruvuma.

Mgendera alisema mafanikio na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji ya mwaka 1998 imeiwezesha serikali kuja na sera ya jumla ya ugatuaji kitaifa ambayo itakuwa na nguvu za kisheria na namna bora ya kutekeleza na kutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi kutoka juu serikalini hadi ngazi za chini za kitongoji na mtaa kule kwenye halmashauri.

Alisema mwelekeo wa serikali kwa sasa ni wa kuwahudumia wananchi kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka ambayo itawekewa nguvu za kisheria na kisera ili kurahisisha suala la utoaji huduma kwa wananchi moja kwa moja kutoka serikali kuu hadi ngazi za kitongoji na mtaa.

Alifafanua kuwa Msingi wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka, 1977, Ibara ya 145 na 146 ambazo zimetoa uhalali wa kuanzishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kubainisha madhumuni ya kuanzishwa kwa mamlaka hizo yakiwamo kuzipa Mamlaka za Serikali za Mitaa madaraka ya kujiamulia mambo yao ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo yao kwa uhuru.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Kisekta kutoka Tamisemi, Juma Idd, alisema timu yake ipo katika mikoa hiyo ya kusini baada ya zoezi hilo kukamilika katika mikoa ya nyanda za juu kusini ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na Rukwa.

Alieleza baada ya kukamilika katika mikoa hiyo timu ya kupokea maoni itaelekea katika nyanda za mashariki ambapo mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma itashirikishwa na baadaye kuhamia mikoa ya Kaskazini, Magharibi na Kanda ya Ziwa.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, alieleza umuhimu wa kikao hicho na kuwa toka mwaka 1998 serikali kupitia Rasimu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP) imekuwa ikitekeleza dhana ya ugatuaji wa madaraka ili kufikisha na kuharakisha utoaji wa huduma za kijami, kiutawala na kiuchumi kwa wananchi kwa haraka na kwa usawa. Mbunge wa Nachingwea, Hassan Elias Masala, alisema kikao hicho ni muhimu kwao kama wawakilishi wa wananchi kwa kuwa utekelezaji wa ahadi nyingi za serikali kupitia chama kilichopo madarakani unategemea sana utekelezaji wa sera hii ya ugatuaji wa madaraka.

Miriam Mwaibula, mshiriki kutoka asasi isiyo ya kiserikali ya Twaweza, alisema maoni yao ni muhimu kwa sababu yatawezesha serikali kupata sera madhubuti na ambayo itakubalika na jamii yote na hivyo kurahisisha utekelezaji wake.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Sirari wilayani Tarime Mkoa wa Mara wakisikiliza masuala ya ubora wa bidhaa walipokutana na maofisa wa Shirika la Viwango la Taifa (TBS). **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya TBS yamalizika wilayani

**Na Neema Mtemvu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limemaliza kampeni yake ya kutoa elimu kwa umma katika wilaya za Nachingwea, Kilwa, Songea, Bukoba, Kahama, Tarime, Nyamagana, Korogwe, Kilombero na Kisarawe Juu ya umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa na shirika hilo.

Kampeni hiyo ya elimu kwa umma imefanyika katika maeneo mbalimbali zikiwamo shule za msingi na sekondari, masoko, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Ofisa Masoko Mwandamizi, Gladness Kaseka, aliwakumbusha wananchi wote kuwa vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee bali ni ya Taifa kwa ujumla.

"Kampeni hii imeweza kuwafikia wananchi 22,322 kati yao wajasiriamali 437, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 6,653 na wananchi 15,232," alisema Kaseka.

Aliwasisitiza wananchi kuendelea kutoa taarifa kupitia mawasiliano waliyopewa pale wanapogundua uwapo wa bidhaa hafifu katika soko.

Vilevile shirika lilipata fursa ya kutoa semina kwa wajasiriamali wanaojihusisha na bidhaa mbalimbali zikiwamo za nafaka, sabuni, mikate, maziwa, pilipili, siagi ya karanga, karanga, korosho, mvinyo, mafuta ya kula, asali, batiki, vikoi na unga lishe juu ya utaratibu wa kupata leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS bure.

Kampeni hiyo imemalizikia katika Wilaya za Korogwe, Kilombero na Kisarawe.

**"Kampeni hii imeweza kuwafikia wananchi 22,322 kati yao wajasiriamali 437, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 6,653 na wananchi 15,232," alisema Kaseka.**

# Mazingira yajengwa mnada wa chai Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya DL Group ambayo kwa miaka mitatu iliyopita imejikita katika kuwekeza katika zao la chai nchini, imejenga ghala kubwa litakalo wapunguzia wazalishaji gharama ya asilimia 50 ya usafirishaji na kujenga mazingira ya usimamizi mzuri ya kuwapo mnada wa kikanda wa chai nchini Tanzania.

Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni hiyo, Dk. David Langat, alisema jijini Nairobi, Kenya, kuwa chai ni zao mkakati katika shughuli za kampuni yao na kwamba kampuni hiyo imedhamiria kushirikiana kwa karibu na serikali na wakulima kukuza ulimaji na biashara ya chai nchini Tanzania.

"Moja ya mambo ambayo yamekuwa yakirudisha nyuma ulimaji na biashara ya chai Tanzania ni ukosefu wa "warehouse" (ghala mahususi) kwa ajili ya kusimamia ufanyikaji wa minada ya chai," alisema na kuongeza:

"Sasa tunajenga ghala hilo ili iwezekane kusimamia ufanyikaji wa minada hiyo maana kwa miaka 49 haukupata kufanyika mnada wa chai Tanzania. Kuwa na ghala ni hatua nzuri na muhimu."

Alisema nia ya kampuni yao ni kuhakikisha mnada wa chai kutoka Tanzania, Rwanda, Burundi na Malawi unafanyika Dar es Salaam na chai hiyo inasafirishwa nje kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Dk. Langat, ghala hilo la Dar es Salaam limeshathibitishwa kama mwanachama wa Chama cha Biashara ya Chai Africa Mashariki (EATTA) ambacho kinaendesha mnada wa Mombasa ambao ni mkubwa duniani.

Alisema kukosekana kwa ghala lililothibitishwa na EATTA kulikuwa kunarudisha nyuma juhudi za uzalishaji, usindikaji na uuzaji wa chai kwa kiwango stahiki.

"Lengo letu ni pana; maana tunataka wakulima wapate bei nzuri, tuongeze zao la chai thamani na kuondoa kila aina ya adha inayokwamisha chai kuuzwa ng'ambo. Mafanikio katika juhudi hii yatachochea uuzaji wa chai nchi za nje," alifafanua Dk. Langat.

Alikumbusha kwamba Tanzania ni nchi ya pili katika Afrika Mashariki na Kati katika kuuza chai nje na kwamba kwa fursa zilizopo nchini na ina nafasi ya kupanua vikubwa uzalishaji na usindikaji wa chai.

Hivi karibuni Dk. Langat alieleza mipango ya kampuni yake kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha ulimaji na biashara ya chai barani Afrika.

# Mashamba yaliyotaifishwa Azimio la Arusha kukaguliwa

Na Augusta Njoji, DODOMA

HALMASHAURI nchini zimeagizwa kuendelea kukagua mashamba yote yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha ili yaandaliwe mipango ya matumizi ya ardhi na kupimwa.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Moshi Vijijini (Chadema), Anthony Komu.

Katika swali lake, Komu alihoji ni lini serikali itatekeleza ahadi yake ya mara kwa mara ya kuyapima upya mashamba yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha ambayo hivi sasa yamebadilishwa matumizi na kujengwa shule, zahanati, hospitali, makazi.

Akijibu swali hilo, Mabula alikiri kuwa kuna mashamba kadhaa nchini yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha.

"Baadhi ya mashamba hayo yaligawiwa kwa mashirika na taasisi za umma kwa ajili ya kuendeleza hususan kwa kilimo cha kahawa na mkonge," alisema.

Hata hivyo alisema baadhi ya mashamba hayo yamebadilishiwa matumizi na yamekuwa yakitumiwa na wananchi kwa matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwamo makazi, shule, zahanati, hospitali.

"Wizara yangu kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini imeendelea kukagua, kuyaandalia mipango ya matumizi ya ardhi na kupima upya baadhi ya mashamba hayo," alisema.

Aidha, alisema baadhi ya mashamba ambayo wizara kwa kushirikiana na halmashauri imeyaandalia mpango wa matumizi ya ardhi ni pamoja na Kihuhwi Estate, Sagulas Estate, Lewa Estate, Bombwera Estate, Geiglitz Azimio, Kipapula pamoja na Kibaranga yote ya Mkoa Tanga.

"Mashamba mengine ni New Msowero Farm, Mvumi Farms/Estate Kilosa na Luipa Estate, yaliyopo mkoani Morogoro, kimsingi jukumu la kuandaa mipango ya matumizi ya mashamba hayo ni la halmashauri husika yalipo mashamba hayo," alisema.

Alitoa rai kwa halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya kupanga na kupima mashamba husika ili yaweze kutumika kwa tija kulingana na mahitaji halisi ya sasa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, akizungumza bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

## Serikali kukutana na wawekezaji wa nchi 10

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angellah Kairuki, amesema serikali inatarajia kukutana na wawekezaji kutoka nchi 10 zinazoongoza kwa uwekezaji hapa nchini ili kusikiliza changamoto zao.

Kairuki aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Busega (CCM), Dk. Raphael Chegeni, ambaye alisema wawekezaji wamekuwa wakichukua muda mrefu kupata vibali jambo ambalo linachafuta taswira ya nchi katika suala zima la uwekezaji.

Alihoji serikali ina mkakati gani katika kuondoa hali hiyo.

Akijibu swali hilo, Kairuki alisema serikali itaanza kukutana na wawekezaji kutoka China katika kikao kitakachofanyika Aprili 17, mwaka huu.

"Tutafanya hivyo kwa wawekezaji wa Uturuki, Marekani, Uingereza na nchi zingine, lengo ni kukutana na wawekezaji wote kutoka kwenye nchi 10 ambazo zinaongeza kwa uwekezaji kwa kuanzia," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alisema kaulimbiu ya serikali ya awamu ya tano ni pamoja na kuongeza na kuvutia wawekezaji ndani na nje ya nchi.

"Je, nini mkakati wa serikali wa kuhakikisha kuwa vikwazo vinavyosababisha kuathiri dhana hiyo vinaondolewa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Kairuki alisema mkakati wa serikali ni kuhakikisha vikwazo vinavyoathiri uwekezaji na biashara nchini vinaondolewa kwa kuweka miundombinu muhimu na mazingira ya kisera, kisheria, kikanuni na kiutendaji ambayo ni wezeshi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi.

Aliitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu wezeshi kama vile ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, umeme na maji hatua ambayo alisema, inapunguza gharama za uendeshaji wa biashara na uwekezaji na kuleta wepesi katika uwekezaji na biashara.

Alisema serikali imeendelea kuhakikisha uwapo wa mazingira bora ya uwekezaji kwa kutekeleza programu za kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Kadhalika, alisema pamoja na mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa mazingira ya biashara nchini, serikali inaendelea kuimarisha ushirikiano na majadiliano na sekta binafsi kupitia Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) pamoja na mikutano ya wadau mbalimbali kwa ngazi za kitaifa, mikoa na wilaya, ambapo changamoto zitakazobainishwa zipatiwa ufumbuzi.



# 'Hakuna ushahidi haki za wananchi kuvunjwa'

BUNGE limeelezwa kuwa hakuna kielelezo wala ushahidi kwamba haki za kimsingi za wananchi wa kata za Ighombwe, Iglansoni zilizopo wilayani Ikungi mkoani Singida zilivunjwa wakati wa kuwaondoa wavamizi kwenye Hifadhi ya Msitu wa Minyughe.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Mwita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Jesca Kishoa.

Katika swali lake, aliuliza kwa muda mrefu sasa Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Miraji Mtaturu, amekuwa akijichukulia sheria mkononi na kuwanyanyasa wananchi wa Kata za Ighombwe, Iglansoni na maeneo ya wilaya hiyo.

Alihoji serikali inaweza kutoa majibu ni mamlaka ipi aliyonayo mkuu huyo ya kuwanyanyasa na kuamrisha mali za wananchi kuchomwa moto au kuporwa na serikali bila utaratibu wowote wa kisheria kwa kisingizio kuwa wanaishi maeneo yasiyoidhishwa kwa makazi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kata hizo zinapakana na Hifadhi ya Msitu wa Minyughe yenye ukubwa wa hekta 264, 600 na kwa nyakati tofauti shughuli za kibinadamu kwenye vijiji vinavyozunguka msitu huo zilianza kuhatarisha mazingira ya hifadhi hasa baada ya wananchi kadhaa kuvamia eneo la hifadhi na kujenga.

"Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kupitia vikao vya kisheria vya Baraza la Madiwani iliazimia kuulinda msitu huo na kuwaondoa wavamizi, hivyo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye mwenye mamlaka aliyopewa na sheria ya tawala za mikoa chini ya kifungu cha 15," alisema.

Alisema zoezi la kuwaondoa wavamizi lilifanyika kwa awamu mbili mwezi Mei na Oktoba mwaka 2017 na watu 119 waliondolewa kwenye hifadhi hiyo pamoja na ng'ombe 2,243, mbuzi 455 na kondoo 169.

"Zoezi hili lilishirikisha askari wa Jeshi la Polisi waliofanya kazi yao kwa weledi wa hali ya juu kwa sababu hakuna raia aliyejeruhiwa wala kupoteza mali zao," alisisitiza Waitara.

Alisema ni dhahiri uwapo wa askari hao ambao ni wasimamizi wa sheria uliwezesha operesheni hiyo kufanyika salama na hakuna kielelezo wala ushahidi kwamba haki zao za kimsingi zilivunjwa.

Akiuliza swali la nyongeza, Mbunge wa Rombo (Chadema), Joseph Selasini, alihoji serikali inawachukulia hatua gani watendaji ambao wamekuwa wakiwaacha wananchi wanajenga na baadaye wanaenda kuwabomolea.

"Serikali inachukua hatua zipi kwa wakuu wa wilaya ambao bado wamekuwa wakiendeleza vitendo vya kuwakamata watu na kuwaweka ndani?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Tamisemi Selemani Jafo, alisema tayari serikali ilishatoa maelekezo kwa watu kutovamia maeneo.

Akizungumzia kuhusu wakuu wa wilaya na viongozi wengine wenye tabia ya kukamata na kuwaweka watu wengine ndani wakiwamo viongozi walio chini yao, Jafo alisema vitendo hivyo vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Alisema bado serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa viongozi hao kuhakikisha wanaacha tabia hiyo.

# Raia wa DRC aliyetimuliwa nchini kulipwa fidia mil. 10/-

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), imeitaka serikali kumlipa fidia ya Sh. milioni 10 raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia Congo, Lucien Ikili Rashidi na Sh. milioni moja kwa kila mwanafamilia yake, baada ya kupata athari ya kuvunjiwa haki, heshima na utu wake.

Rashid ambaye kwa sasa anaishi Burundi, aliingia nchini mwaka 1993 kwa kutumia visa ya muda mfupi na kisha mwaka 1999 mke na watoto wake waliingia nchini kama wakimbizi, lakini hawakukaa kwenye makambi ya wakimbizi badala yake wakafikia Dar es Salaam.

Alidai kuwa Juni 9, 2006, maofisa kutoka Idara ya Uhamiaji walimkamata kwa madai ya kuishi nchini kinyume cha sheria licha ya kuwa alikuwa akisikiliza shauri lake la madai mahakamani.

Baada ya kuwasilisha malalamiko yake mahakama za nchini bila mafanikio, alifungua shauri AfCHPR, akitaka alipwe fidia akidai kuvunjwa kwa haki zake za kuishi, kutembea, utu na haki ya kusikilizwa mahakamani.

Katika hukumu iliyotolewa na mahakama hiyo hivi karibuni, Jaji Angelo Matusse, alisoma mbele ya jopo la majaji wenzake, Suzanne Mengue, Tujilane Chizumila, Chafika Bensaula, Blaise Tchikaya na Stella Anukaman, akitaka serikali kulipa fidia hiyo kwa Rashidi.

Upande wa serikali uliwakilishwa na Mkurugenzi wa Divisheni ya Masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, Sarah Mwaipopo, Mkurugenzi wa Masuala ya Sheria kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Afrika Mashariki na Ushirikiano wa Kimataifa, Baraka Luvanda.

Wengine ni wanasheria wakuu waandamizi wa serikali, Nkasori Sarakikya na Mark Mulwambo, Aidan Kisumo na Blandina Kasagama.

Kwa upande wake, Rashidi, alikuwa anatetewa na Chama cha Mawakili cha Pan African, (PALU).



Balozi wa Japan hapa nchini, Shinichi Goto na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, wakikata utepe kuzindua Kituo cha Afya Manyire kilichopo katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, juzi, ambapo nchi hiyo imechangia kiasi cha Sh. milioni 191 katika ujenzi huo. Wa (pili kushoto) ni Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, Gipson Ole Meseyeki na (kulia) ni Mbunge Viti Maalumu kwa Walemavu, Amina Mollel na (wa pili kulia) ni Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Wilson Mahera. **PICHA: ALLAN ISACK**

## Wamachinga watoa zawadi ya ng'ombe kwa JPM

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAFANYABIASHARA ndogo ndogo wa Jiji la Arusha maarufu kama (machinga) wametoa zawadi ya ng'ombe kwa Rais John Magufuli, kama ishara ya shukrani baada ya kutangaza wasibughudhiwe katika shughuli zao wakiwa na vitambulisho vya machinga.

Akizungumza jana na wafanyabiashara hao eneo la Samunge Jiji la Arusha, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, baada ya kupokea zawadi hiyo kwa niaba ya Rais Magufuli, alisema machinga hao kwa umoja wao wametoa ng'ombe mmoja, kama zawadi kwa Rais Magufuli na kuahidi kuifikisha.

"Kitendo hiki ni ishara kubwa ya upendo na kukubali kile alichowafanyia Rais wetu, hivyo mimi nitafikisha kwa muhusika kama mlivyonituma," alisema.

Alisema katika ugawaji wa vitambulisho hivyo baadhi ya wakurugenzi na wakuu wa wilaya wanazembea kuvigawa, hali inayosababisha mkoa huo kuwa nyuma katika ugawaji wa vitambulisho hivyo na kumkwamisha kupeleka taarifa kwa Rais juu ya ugawaji huo. "Mimi natakiwa kila siku kutoa taarifa kwa Rais kwa njia ya WhatsApp nimegawa vitambulisho vingapi, lakini nashindwa sababu baadhi ya wakuu wa wilaya na wakurugenzi wananikwamisha, hili sitakubaliana nalo nitapeleka majina yao," alisema.

Aidha, alisema katika hilo atalazimika kumwandikia barua Rais Magufuli, ifikapo Aprili 30, mwaka huu, kwa ajili ya wakuu wa wilaya na wakurugenzi ambao wamefanya vibaya katika zoezi la ugawaji wa vitambulisho hivyo vya machinga mkoani hamo, ili achukue hatua dhidi yao.

Gambo alisema zoezi la ugawaji vitambulisho kwa Mkoa wa Arusha, haliridhishi na baadhi ya wilaya wanaleta visingizio mbalimbali, lakini kila mmoja lazima aelewe vitambulisho hivyo vinatakiwa viishe. Naye mwenyekiti wa wamachinga Jiji la Arusha, Amina Njoka, alisema machinga hao wamegawanyika katika kanda sita, ambazo ni Kwamrombo, Kilombero, Mianzini, Samunge Mjini Kati na Mount Meru na hadi sasa wapo zaidi ya 12,000.

Pia wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa maeneo ya kufanyia kazi zao na mikopo ili waweze kuboresha biashara zao na kuomba Jiji la Arusha, kuwasaidia kupata mikopo yao. "Sisi tukienda kukopa benki tunanyimwa sababu tuna biashara za kuhamahama, hivyo Jiji tunaomba mtupatie mikopo yenu," alisema. "Tumempa Rais Magufuli zawadi hii kama asante kwa kututambua na kusema tusibughudhiwe, tunashukuru mwambie tunampenda na vitambulisho tutakata, maana hatutaki usumbufu hivi sasa tunafanya kazi zetu kwa amani na tunamwombea Rais wetu maisha mema na marefu ametujali wanyonge," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro, aliwataka machinga hao kuhakikisha wanakuwa na vitambulisho hivyo na kuacha kufanya biashara kwenye maeneo ya barabarani, kwani wanaweza kusababisha ajali badala yake wakae kwenye maeneo yenye usalama zaidi na kuzingatia usafi ili kuepuka magonjwa ya milipuko.

# Mradi wa maji waleta neema kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu, BABATI**

WAKAZI wa Kijiji cha Sangara, Kata ya Riroda, wilayani Babati, waliokuwa na changamoto ya ukosefu wa maji, wanatarajia kuondokana na tatizo hilo baada ya mradi wa maji kuwekwa jiwe la msingi.

Mradi huo mkubwa wa maji wa thamani ya Sh. milioni 210, umefadhiliwa na mashirika ya Water Aid, Habitat for Humanity na wananchi wa kijiji hicho.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kuweka jiwe la msingi la mradi huo, aliwataka wananchi wa eneo hilo kuulinda pindi utakapokamilika.

Alisema wananchi wa eneo hilo wanatakiwa kuilinda na kuitunza miundombinu ya mradi huo mkubwa wa maji ambao utakuwa na faida kwao na vizazi vijavyo.

Aliwashukuru wadau hao wa maendeleo kwa kushirikiana na wananchi kuweza kujenga mradi huo wa maendeleo utakaowapatia majisafi.

"Tunawashukuru sana wadau wetu na wananchi kwa ujumla kwa kuwa mradi huu upo kwenye hatua ya mwisho kabla ya uzinduzi wake kufanyika hivi karibuni," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Hamis Malinga, alisema mradi huo utawanufaisha wananchi wa kijiji hicho na majirani zao kwani hivi sasa watakuwa wanapata huduma ya maji kwa karibu zaidi.

Alisema suala la umakini na utunzaji wa mradi huo pindi ukimalizika ndiyo unatakiwa hivyo wananchi wa eneo hilo wajipange kwa hilo, kwa kuwa kupata mradi ni jambo moja na kutunza mradi ni jambo lingine.

Mkazi wa Kijiji cha Sangara, Daudi Dahaye, alisema mradi huo utakapokamilika utakuwa faraja kwao kwani tatizo la ukosefu wa maji litakuwa limefika ukingoni.

"Hivi sasa wanawake ndiyo wanapata changamoto kubwa ya kufuata huduma ya maji hadi kule Riroda hivyo kusababisha shughuli nyingi kukamatwa ila kupitia mradi huu mkubwa utatusaidia mno," alisema.

Mkazi mwingine Joyce Sulle alisema suala la upatikanaji wa maji kwenye eneo hilo itakuwa historia pindi mradi huo utakapokamilika, kwa kuwa wameteseka kwa kukosa maji kwa muda mrefu.

"Watoto wetu walikuwa wanachelewa shuleni kwa kufuata maji hadi kule Riroda, ila mradi huu ukikamilika utatunufaisha kwa kweli tunawashukuru wote waliohusika na kuufanikisha mradi huu," alisema.

## KESI YA MAUAJI YA MWANAFUNZI

# MAHAKAMA YAKUBALI PANGA KAMA KIELELEZO

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Moshi imemaliza ubishi wa malumbano makali ya kisheria kati ya jopo la mawakili wa utetezi na upande wa mashtaka katika kesi ya mauaji ya kukusudia ya mwanafunzi wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari ya Scholastica, Humphrey Makundi (16), baada ya Jaji Firmin Matogolo kukubali kupokea 'panga' kama kielelezo cha ushahidi wa shahidi wa 11.

Akitoa uamuzi mdogo kuhusu pingamizi lililowekwa na mawakili wa utetezi waliopinga kupokelewa kwa kielelezo hicho cha tatu cha upande wa mashtaka kama kielelezo cha ushahidi, Jaji Matogolo ameeleza kuwa baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili na kuchunguza majibu aliyoyatoa shahidi Jackson Daudi baada ya kuulizwa swali, kwa tafsiri yake shahidi alitaka panga hilo lipokelewe.

"Inaonyesha panga lilitolewa na shahidi kwa uelewa wake wa nini anatakiwa kujibu, lakini kwa kuchunguza majibu aliyoyatoa baada ya kuulizwa swali na Wakili Mkuu wa Serikali (John Pande), kwa tafsiri yangu alitaka panga hilo lipokelewe. Sioni tatizo kwa kile ambacho shahidi amesema kwa maana hiyo pingamizi hili linatupiliwa mbali na panga linapokelewa na kuwa kilelezo cha upande wa mashtaka," alieleza Jaji Matogolo.

Mabishano hayo yaliibuka jana mahakamani hapo na kudumu kwa dakika 30, baada ya shahidi wa 11 wa upande wa mashtaka, Jackson Daudi ambaye ni Mlinzi wa Shule ya Sekondari ya Scholastica iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo, Wilaya ya Moshi kutoa ushahidi wake.

Humphrey anadaiwa kutoweka shuleni hapo Novemba 6, mwaka 2017 na baadaye mwili wake ulibainika kuzikwa na Manispaa ya Moshi kwa madai ya kutotambuliwa. Inadaiwa kuwa Novemba 17, mwaka 2017 mwili wake ulifukuliwa, baada ya baba mzazi wa mtoto huyo kupata amri ya mahakama ya kuufukua mwili huo ukiwa umekaa kaburini kwa siku sita.

Wanaokabiliwa na kesi hiyo, namba 48 ya mwaka 2018 ni mshtakiwa wa kwanza Hamisi Chacha, ambaye ni mlinzi wa shule hiyo, mmiliki wa shule hiyo Edward Shayo 'king size' na mwalimu wa nidhamu Laban Nabiswa.

Kabla ya Jaji Matogolo kutupilia mbali pingamizi hilo, Wakili wa Utetezi, Elikunda Kipoko, alisimama na kupinga ombi la Wakili Mkuu wa Serikali, John Pande, aliyeiomba mahakama hiyo ipokee panga hilo kama kielelezo cha ushahidi wa shahidi wa 11 wa upande wa mashtaka, akidai kuwa maelekezo yanayotolewa na Wakili Pande siyo sahihi na wao wanaoomba jibu lililotolewa na shahidi huyo liingie katika kumbukumbu za mahakama.

Kilichoibua mjadala huo wa malumbano ya kisheria ni ombi la shahidi huyo (Jackson) kusema: "Naomba hili panga litolewe hukumu." Baada ya kauli hiyo Wakili Elikunda Kipoko, alisimama tena na kuwasilisha pingamizi akisema ni dhahiri kwamba shahidi ameshaeleza anataka nini kifanyike, lakini anachofanya Wakili Mkuu wa Serikali ni kumfundisha shahidi.

"Wakili kumuuliza shahidi two times (mara mbili) anataka mahakama ifanye nini katika kielelezo. Sisi wa utetezi tunapinga hilo ombi lake la kutaka panga lipokelewe na sio kauli ya shahidi," alidai Wakili Kipoko.

Dakika chache baadaye, Wakili Gwakisa Sambo, alisimama na kuieleza mahakama hiyo kwamba wanapinga ombi hilo la Wakili wa Serikali kwa sababu kwanza yeye siyo shahidi wa kutoa kielelezo hicho na submission yao 'hoja' ni kwamba procedure (taratibu) za mahakama za Tanzania, ni shahidi peke yake ambaye anaweza akatoa ombi hilo.

Katika hoja yake, Wakili Sambo alieleza: "Hivyo basi, kwa kuwa Wakili Mkuu wa Serikali siyo shahidi, kwenye macho ya sheria hana nafasi ya kuleta ombi hilo. Tunaomba ombi lake likataliwe."

Akijibu hoja za mawakili wa utetezi, Wakili Mkuu wa Serikali alidai mahakamani hapo kuwa anaungana na hoja ya Wakili Sambo kwamba anayetoa kielelezo ni shahidi, lakini anayeomba kielelezo kipokelewe ni Public Prosecutor 'Mwendesha Mashtaka wa Serikali' kwa hiyo ni vitu viwili tofauti.

"Ni rai ya upande wa mashtaka kwamba maneno aliyotumia shahidi wa upande wa mashtaka, tunaomba yapokelewe kutokana na uelewa wa shahidi," aliwasilisha hoja hiyo Wakili Mkuu wa Serikali.

Juzi, shahidi wa 10 katika kesi hiyo ya mauaji ya kukusudia ya mwanafunzi wa kidato cha pili, F.3988, Detective CPL (mpelelezi), Luis aliieleza mahakama hiyo kuwa yeye ndiye aliyepeleka nyama za makalio, paja, mifupa ya kifua na nyama ya kibofu cha mkojo chenye nywele kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, Oktoba 22 mwaka 2017.

Shahidi huyo ambaye ni mpelelezi anafanya kazi katika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkoa wa Kilimanjaro, alidai mahakamani hapo pia alipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ute wa mate na damu ya Jackson Makundi na Joyce Makundi.

Sampuli nyingine alizozipeleka kwa Mkemia huyo ni nyama ya kisigino kinachodaiwa kuwa cha Humphurey Makundi na viatu seti mbili, sampuli ambazo ziliandikwa lebo (kumbukumbu) kila moja na kuhifadhiwa katika kisanduku maalumu cha kuzuia visiharibike.

Kachero huyo, alikuwa akitoa ushahidi wake katika mahakama hiyo akiongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula.



Shahidi huyo alidai mahakamani hapo kuwa, viatu hivyo vilikuwa vimehifadhiwa katika bahasha ya kaki na kwamba kabla ya safari ya kupeleka vipimo hivyo aliandaliwa barua ya kwenda kumtambulisha Makao Makuu ya Polisi jijini Dar es Salaam.

Pia alidai kuandikiwa barua ya kwenda kumtambulisha kwa Mkemia Mkuu wa Serikali akiwa ameambatanisha na fomu namba 180.

Alidai alipofika kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, alipokelewa na baada ya kujitambulisha aliitwa Hadija ambaye pia alielezwa kuwa ndiye aliyekuwa amepokea sampuli kama hizo kwa Ofisa wa Polisi kutoka Kilimanjaro na kwamba vipimo hivyo baada ya kuvipokea alisaini kwenye 'Dispatch Book' aliyotoka nayo Makao Makuu ya Polisi.

"Baada ya zoezi hilo, mimi nikawa nimeshamaliza mchezo huo nikaondoka zangu nikaendelea na mambo yangu kwa kuwa mzigo niliokuwa nao nilishaumaliza," alidai shahidi huyo.

Aidha, shahidi huyo aliendelea kudai mahakamani hapo kuwa ujuzi huo alipata kwa kusoma kozi mbalimbali katika vyuo vya polisi na Chuo cha Maofisa wa Polisi Kurasini-jijini, Dar es Saalam.

Shahidi huyo alidai kuwa yeye ndiye aliyehusika kusafirisha sampuli mbalimbali za DNA (vinasaba) hadi ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam Oktoba 20, mwaka 2017.

Akiongozwa na Wakili wa Mwandamizi wa Serikali Chavullah, shahidi huyo alidai alipeleka vipimo vya Joyce Makundi, Jackson Makundi, ikiwamo damu na jino la mwili wa marehemu ambaye hakujulikana jina na sampuli hizo alipita nazo Ofisi ya DCI (Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai) na kukiombea kibali cha kupeleka vipimo hivyo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali baada ya kupata barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kilimanjaro.

Alidai kuwa aliondoka Novemba 21, mwaka 2017 mjini Moshi na kwenda jijini Dar es Salaam kwa gari ndogo ya Polisi na alifika Dar es Salaam siku inayofuata majira ya saa 3:00 usiku.

Alidai kuwa sampuli hizo zilikuwa zimehifadhiwa na kufungwa na 'lakiri' maalumu na kuhifadhiwa katika kisanduku.

Baada ya wakili wa upande wa mashtaka kumaliza jukumu la kumwongoza shahidi huyo kutoa ushahidi wake, Wakili wa Utetezi, David Shilatu, alianza kumfanyia mahojiano shahidi huyo.

**Wakili Shilatu:** Ni kweli haukwenda Jijini Dar es Saalam tarehe ulioitaja hapa mahakamani?

**Shahidi:** Utakuwa umesema uongo kabisa.

**Wakili:** Hukukabidhi vielelezo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali?

**Shahidi:** Nimesema nilikabidhi barua na vipimo.

**Wakili:** Ulipewa majibu baada ya vipimo?

**Shahidi:** Sikupewa hadi leo.

Wakili: Ulichopelewa kwa Mkemia hujapewa majibu?

**Shahidi:** Ni kweli.

Wakili: Hii barua ya RCO (Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kilimanjaro) na DCI (Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai) umeileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Sijaileta.

**Wakili:** Ndio maana nakwambia hukwenda Dar?

**Shahidi:** Mimi nilienda Dar wewe ndio hukwenda.

**Wakili:** Ulipiga picha za mwili wa marehemu zikifukuliwa?

**Shahidi:** Hapana.

**Wakili:** Uliona picha za kufukuliwa mwili wa marehemu?

**Shahidi:** Sikuona, tupo wengi mimi sina studio ya kusafisha picha.

**Wakili:** Tukisema picha za kufukua maiti zipo ofisini kwenu ni sawa?

**Shahidi:** Zipo.

**Wakili Paul:** Unajua sampuli ulizopeleka kwa Mkemia Mkuu ni za nani?

**Shahidi:** Sijui.

**Wakili:** Barua ya RCO uliipeka kwa Mkemia wa Serikali?

**Shahidi:** Sikuipeleka kwa kuwa barua ile ilikuwa ya kunitambulisha Ofisi ya DCI (Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai), Makao Makuu ya Polisi.

Aidha, shahidi wa tisa katika kesi hiyo ambaye ni mlinzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Godlisten Kitomari, alidai mahakamani hapo kuwa hakutambua maiti aliyoipokea Novemba 11, mwaka 2017, kwa kuwa mwili huo ulishaanza kuharibika na hakuutambua kama ni mwili wa mtoto ama mtu mzima kwa kuwa giza lilishaanza kuingia.

Shahidi huyo aliieleza mahakama hiyo kuwa siku hiyo Novemba 11, 2017 majira ya saa 3:00 za usiku akiwa kazini akipewa maelekezo na mkuu wa zamu siku hiyo ya kupokea maiti isiyojulikana kutoka Himo wakiwamo askari polisi wawili.

Alisema kiongozi wake wa zamu alimwomba msaada wa kuwasaidia wale askari polisi kuingiza maiti ndani ya chumba cha kuhifadhia maiti na kabla ya kwenda kuhifadhi mwili huo, nilimuuliza bosi wangu mwili huo umetoka wapi, nikajibiwa Himo na je, umeshaandikisha katika daftari la kumbukumbu nikajibiwa ndio.

Alidai wakati huo maiti ilikuwa ndani ya gari la polisi nje ya geti na baadaye niliwafungulia geti na polisi waliingiza mwili ndani na nikawaambia wauweke kwenye sinia ama karai ili uje kuhifadhiwa siku ya pili na mtu anayehudumia mochwari.

Alidai mwili hao ulikuwa umefunikwa na khanga na aliufungua na kuuangalia ili kujiridhisha ni binadamu kweli ama la na baadaye aliutambua ni wa binadamu ukiwa umevalia bukta, soksi na tisheti.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo inayovuta hisia za wakazi wengi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini, unaongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, John Pande, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavullah, Wakili wa Serikali, Omary Kibwana na Wakili wa Serikali, Lucy Kyusa.

Wakati jopo la mawakili wa utetezi linaongozwa na mawakili wasomi Elikunda Kipoko, Wakili David Shilatu, Wakili Gwakisa Sambo na Wakili Patrick Paul.

Ukurasa 18



MAFUNZO YA UONGOZI, MAISHA KUTOKA KWA NJELU KASAKA- 1

## MAKALA:

Ukaribu Uganda, Rwanda kihistoria sasa kuamua hatima ya Rais Kagame



Ukurasa 14

## KIMATAIFA:




Ulaya waichoka Uingereza 'kuangukia pua', sasa Aprili 12 hali isipobadilika

Ukurasa 20


# siasa

JUMATANO APRILI 10, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU





## AIRO:

Sitagombea ubunge 2020, ninang'atuka Rorya

Ukurasa 15

# Migogoro na changamoto kwa miradi ya EAC

**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya madhumuni makubwa ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ni kuchagiza kasi ya ukuaji wa uchumi, biashara na ustawi wa maisha ya raia katika nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Jumuiya hiyo kwa mara ya kwanza iliundwa mwaka 1967 ikawa na nchi tatu zilizokuwa wanachama, yaani Tanzania, Kenya na Uganda.

Hata hivyo, ilipofika mwaka 1977, EAC ilivunjika hadi mwaka 1999 kuliposainiwa mkataba wa uanzishwaji wake kupitia wanachama hao hao, ingawa baadaye Rwanda, Burundi na Sudani Kusini ziliongezeka hivyo kuifanya idadi yao kuwa nchi sita.

Licha ya nia nzuri ya kuzileta pamoja nchi hizo za ukanda wa Mashariki mwa Afrika, bado tofauti za kati ya nchi moja na nyingine miongoni mwa zilizo wanachama wa EAC, zinazidi kukua kiasi cha kuhatarisha tena uhai wake.

Ingawa nchi zote na kwa nyakati tofauti zimewahi kuweka wazi dhamira ya kutokuwa tayari kuiona

ENDELEA UK 16



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Balozi Liberat Mfumukeko. **PICHA: MTANDAO**

UCHAMBUZI

# Ukaribu Uganda, Rwanda kihistoria sasa kuamua hatima ya Rais Kagame

**Na Ani Jozeni**



Jenerali Kayumba Nyamwasa. **PICHA: MTANDAO**

BAADHI ya wanasafu katika vyombo vya habari hapa nchini wamesikika hivi karibuni wakisema au kutoa ishara kuwa iwapo Uganda na Rwanda zitaingia katika mtafaruku wa wazi, nchi zilizobaki zichukue jembe kulima, wakipatana wawauzie mahindi, mchele, n.k.

Ni ule usemi kuwa ndugu wanapopigana au kuzozana, usiingilie ugomvi huo kwani ukifikia tamati yake, hawatakujua wewe, wakati unaweza kujipalia mkaa iwapo utaingilia kwa njia ya kusuguana na mmoja wao.

Nchi hizi zinajaribu kuelewa ugomvi wa Uganda na Rwanda lakini zinapata shida, kwa kuwa kimsingi kiongozi wa Rwanda Paul Kagame anahofia hifadhi ya wapinzani Uganda kwa kuwa wanaweza kupata nafasi ya kuanzisha vita kama alivyoanzisha yeye nyakati zilizopita, kuleta mabadiliko.

Tatizo la msingi linalojitokeza hasa kwa nchi za jirani ni kuwa kuna uhusiano kati ya nchi hizi mbili ambao siyo uswahiba wa kawaida bali ni undugu wa kisiasa, na hata kwa uhusiano binafsi kutokana na chimbuko la tawala zote mbili kuwa ni moja.

Ni chama kinachotawala Uganda, National Resistance Movement (NRM) ambako Rais Kagame alikuwa kada, mpiganaji na mkuu wa intelijensia kwa muda mrefu katika chama hicho.

Baada ya ushindi mwaka 1986 ndipo makada wake wanaotokea Rwanda walipoanza kujipanga kuondoa utawala wa ki-Hutu wa Rais Juvenal Habyarimana, hadi walipokaribia kuingia serikalini kupitia makubaliano ya Arusha.

Kuzuia hali hiyo, maofisa wa jeshi chini ya Habyarimana wasiotaka kusikia kuna muafaka na wa-Tutsi - hasa baada ya Melchior Ndadaye kushinda kura Burundi, akatawala miezi mitatu na kuuawa na vikosi vya jeshi lililosheheni wa-Tutsi Oktoba 1993.

Mauaji hayo yaliondoa shaka yoyote kuhusu dhamira ya Watutsi pindi wakiingia serikalini na jeshini; wangekuwa na uwezo wa kupindua serikali wakisaidiana na watawala wa ki-Tutsi nchini Burundi.

Ndipo likazuka wazo la kuwaua wa-Tutsi wote kuzuia wasitwae madaraka ya nchi, jambo hilo likapangwa Ikulu ya Habyarimana bila yeye kujua, ndege yake ikaanguswa akitokea Tanzania, mauaji yakaanza.

Usiku wa Aprili 6, 2019 ni miaka 25 ya kuanza kwa mauaji ya kimbari yaliyotikisa Afrika na dunia kwa jumla, na utawala wa ki-Hutu uliokuwa unafanya kazi moja tu ya kusaka wa-Tutsi kokote walipo na kuwaua haukuchukua muda kuparaganyika kwani ulikuwa unaendeshwa kwa amri za kijeshi za mdomoni na si utawala wa kawaida.

Hivyo kukawa na nafasi kubwa zaidi ya vikundi vya wapiganaji wa Rwanda Patriotic Front (RPF) kulizunguka jeshi hilo la wauaji na kulitoboa hapa na pale, kisha kupiga maeneo yaliyo dhaifu yasiyoweza kupata msaada, kubeba silaha hizo na kukusanya raia waliokuwa tayari kuongeza nguvu kuondoa utawala wa wauaji jijini Kigali.

Hatua ya pili ya uswahiba na undugu wa Uganda na Rwanda ikawa ni operesheni ya pamoja ya kuondoa utawala wa Rais Mobutu Seseseko wa iliyokuwa Zaire, ambako hasa Rwanda iliongoza, ikahitilafiana baadaye na Laurent Kabila waliyemsaidia kuingia madarakani, halafu vita ikazuka nchi za Kusini mwa Afrika zikiingilia kati.

> Kimsingi jemadari huyo wa zamani wa Rwanda anaishi Afrika Kusini, ila shughuli zake za kuunda chama cha upinzani zinaendeshwa kutoka Uganda.

Miaka 20 baadaye hali imetulia DRC kwa kiasi fulani lakini uthabiti wa serikali ya Kagame uko mashakani kiasi, kwani ameshindwa kuliondoa kundi kubwa la mabaki ya vikosi vya mauaji ambalo baadaye lilijipachika jina la Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR), kana kwamba wanapigania demokrasia.

Hao hawana uwezo wa kutetemesha serikali ya Rwanda kimaadili, bali wapinzani waliotokea RPF miaka ya karibuni.

Rwanda National Congress (RNC) ndiyo chama cha wapinzani waliotokea ndani ya chama cha RPF na uwezo wao dhidi ya Rais Kagame unaweza kufananishwa na kundi la Dk. Kiiza Besigye nchini Uganda, aliyekuwa daktari binafsi wa Rais Yoweri Museveni halafu vyama vingi vilipokolea, akaona aongoze upinzani, kwani ule wa zamani enzi za Idi Amin na Milton Obote wa pili ulishafifia.

Wakati Rais Museveni ametumia kila nguvu aliyonayo kunyamazisha upinzani uliotokea NRM, anawapa nafasi ya kupumua wapinzani wa Rais Kagame.

Moja ya matatizo ni jinsi walivyofarakana kuhusu DRC, licha ya kuwa Uganda ina mpaka mrefu na DRC na haikuwa na haja ya kutegemea Rwanda ila inafanya nini mipango yake kuhusu raslimali isikwamishwe na Rwanda.

Kilichomsaidia Museveni dhidi ya wapinzani wake ni kuwa wanatokea zaidi Jimbo la Kusini la nchi hiyo, Buganda ambalo pia linapakana na ziwa, na makundi hayo hayana uwezo wa kupata misaada kutoka serikali za Kenya au Tanzania ambao kila moja ina mpaka mrefu na Uganda.

Rwanda ni tofauti, kwani wengi kati ya maswahiba wa jadi wa Kagame wanajulikana Uganda, hivyo wakiingia nchini humo kueleza matatizo yao ni kama wako nyumbani, kielelezo kile kile cha kundi la M23 la upinzani DRC, ambako wakienda Kigali kueleza matatizo yao na kile wanachokitaka, wako nyumbani kwani Rwanda ilikuwa chimbuko la utawala wa Rais Kabila mwaka1997 na halafu mwanae Joseph Kabila Kabange akatwaa madaraka baba yake alipouawa na hao hao vijana wa kutoka Rwanda waliowasaidia kina Kabila kuchukua madaraka. Ni hivyo pia Rwanda na Uganda.

Kwa maana hiyo viongozi wakuu wa serikali ya Rwanda, hasa Kagame na Waziri wa Mambo ya Nje, Dk. Richard Sezibera (aliyekuwa katibu mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki), wanapigana na vivuli wanapoikosoa Uganda kuhusu kumhifadhi mara kwa mara au kumpa ushirikiano Jenerali Kayumba Nyamwasa.

Kimsingi jemadari huyo wa zamani wa Rwanda anaishi Afrika Kusini, ila shughuli zake za kuunda chama cha upinzani zinaendeshwa kutoka Uganda.

Kutokana na historia ya mauaji ya kimbari ambayo wengi nchini Rwanda bado wanahofia kundi la DRC (FDLR) lina mpango wa kuyaendeleza, Rais Kagame amekuwa hana mpango wowote wa kukubali uwepo upinzani wenye nguvu nchini humo.

Ndiyo hapo anapata tabu kuelewana na mwalimu wake wa zamani, Kaguta, akimkumbusha walivyosema wahenga 'wakati ukuta,' kuwa upinzani sasa ni lazima.



Mbunge wa Rorya, Lameck Airo. **PICHA: MTANDAO**

# AIRO: Sitagombea ubunge 2020, ninang'atuka Rorya

- Ninaheshimu sana utaratibu wa kuachiana vijiti
- Nilikuta shule za sekondari 16 na sasa zimefikia 30

**Na Sabato Kasika**

LAMECK Airo ni Mbunge wa Jimbo la Rorya mkoani Mara, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambaye amekuwa maarufu kwa kuweka wazi elimu yake kuwa ni ya darasa la saba, tofauti na baadhi ya wabunge wanaoficha.

Katika kampeni za 2010 zilizompa ushindi, alijinadi na kuweka wazi kwamba amehitimu darasa la saba na anajivunia elimu hiyo na kusikika kwenye vyombo vya habari akisema 'lasaba hoyee' na akashangiliwa na wafuasi wake.

Mbunge mwingine anayejivunia elimu hiyo ni wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku 'Msukuma,' ambaye kama ilivyo kwa Airo, naye amekuwa haoni aibu kutaja kiwango cha elimu mbele ya umma.

Wiki hii Airo alizungumza na gazeti hili kuhusu mikakati yake kwenye siasa na kuweka wazi kwamba mwaka 2020, atapumzika kupisha wanachama wengine wa CCM kuwania nafasi hiyo ya ubunge.

Anasema miaka 10 inatosha na ndio aliyokuwa amejipangia na anaongeza kuwa iwapo Mungu ataendelea kumpa uzima, basi atatimiza ahadi yake hiyo ya kujiweka pembeni kwenye nafasi ya ubunge.

"Unaweza kushangaa, lakini huo ndio uamuzi wangu kwamba mwaka 2020, sitagombea tena ubunge... nitamwachia kijiti mwanachama mwingine wa CCM na nitamsaidia kwenye kampeni kuhakikisha anashinda," anasema Airo.

**SABABU ZA KUTOGOMBEA**

Mbunge huyo anataja sababu kuu mbili zinazomfanya asigombee tena ubunge, mojawapo ikiwa ni kupata muda wa kutosha wa kusimamia biashara zake, ambazo ziko maeneo mbalimbali nchini ikiwamo jijini Mwanza.

"Sababu nyingine ni kwamba ninataka kung'atuka wakati bado nikiwa na nguvu za kutosha huku wananchi wakiwa bado wananipenda...si kusubiri wanichukie na kunifukuza ndipo niachie ubunge," anasema.

Anabainisha kwamba hataki kuwa kama baadhi ya wabunge ambao wamekuwa waking'ang'ania nafasi hata kama uwezo wao wa kuongoza umefikia mwisho na hatimaye kujikuta wakikataliwa na wapigakura.

Mwakilishi huyu wa wananchi wa Rorya anasema katika mazingira hayo wapo ambao hujikuta wakipata magonjwa ya moyo bila kutarajia, kwa sababu ya kukataliwa, wakiwa hawana jinsi ya kufanya na hivyo kuwa na mawazo mengi mioyoni mwao.

"Mimi sitaki kufikia hali kama hiyo, ninaheshimu sana utaratibu wa kuachiana vijiti, ndio maana ninachukua hatua hiyo...nimekuwa diwani kwa miaka 10 na sasa ubunge nao miaka 10, muda huo unatosha," anasema.

Airo anasema tayari ameshaanza kuwaaga wapigakura wake na kuwaeleza sababu ya kutogombea tena ubunge katika uchaguzi mkuu ujao, lakini anafafanua kuwa baadhi yao wamemkatalia.

"Labda niseme kwamba mimi siyo kama wengine ambao huwa wanafanya uamuzi kwa ajili ya kuwajaribu wapigakura halafu baadaye wanachukua fomu kuwania ubunge...nimeshaamua kupumzika, sirudi nyuma," anasema.

Anafafanua kuwa mwaka kesho atakuwa anatimiza umri wa miaka 54, hiyo inatosha kukaa pembeni na kuachia vijana wenye nguvu kuanzia pale atakapokuwa amefikia katika juhudi zake za kuleta maendeleo ya Rorya.

> Prof. Tibaijuka alitangaza uamuzi huo alipokuwa akizungumzia miaka miwili ya Rais John Pombe Magufuli tangu aingie madarakani wakati rais huyo akiwa kwenye ziara mkoani Kagera.

**MCHANGO WAKE JIMBONI**

Anasema moja ya kazi ya mbunge ni kuleta msukumo kwa kuhamasisha wananchi kujiletea maendeleo na kwamba tangu achaguliwe amefanya kazi hiyo kwa kushirikiana nao kwenye baadhi ya maeneo.

"Kwa mfano wakati ninachaguliwa, nilikuta jimbo lina shule 16 za sekondari, lakini hadi sasa zimefikia 30, na zinaendelea kujengwa nyingine zaidi...haya ni mafanikio makubwa," anasema.

Anabainisha kwamba wakati mwingine amekuwa akitumia pesa zake kwa ajili ya maendeleo ya Rorya, hali ambayo imewafanya wananchi kumuunga mkono kwa juhudi hizo anazoonyesha.

"Unapozungumzia maendeleo huwezi kuyatenganisha na elimu, na kama nilivyosema, nilikuta kuna shule za sekondari 16 na sasa zimefikia 30, haya ni maendeleo ya kujivunia," anasema.

**WIZI WA MIFUGO**

Aidha, anasema alipochaguliwa alikuta tatizo la wizi wa mifugo wa mara kwa mara na akashirikiana na serikali kuweka mikakati ikiwamo kuanzisha kanda maalum polisi ambayo imesaidia kukomesha wizi huo.

"Binafsi niliwahi kukutana na viongozi, wananchi wa kabila la Wajaluo na Wakurya katika Kata za Koryo Rorya na Bumera Tarime na kuwataka wasiibiane mifugo, waweke tofauti zao pembeni na kuendeleza ushirikiano, upendo na kuilinda amani iliyopo kwa maendeleo yao," anasema.

Mbunge huyo anasema kwa kuwa wizi huo ulishakoma na amani kurejea, sasa wananchi wanafanya shughuli za kujiletea maendeleo bila hofu na anaamini kuwa atastaafu huku jimbo hilo likiwa limepiga hatua nzuri ya maendeleo.

Abainisha kuwa hayo ni miongoni mwa mambo makubwa ya msingi ambayo anajivunia, kwamba anaiacha Rorya ikiendelea kupiga hatua kielimu na pia kuwa na utulivu na amani.

**WENGINE WANAONG'ATUKA**

Airo atakuwa mbunge wa pili wa CCM kuweka bayana kutowania ubunge mwaka ujao baada ya Profesa Anna Tibaijuka ambaye ni Mbunge wa Muleba Kusini mkoani Kagera, kutangaza uamuzi huo mwaka juzi.

Prof. Tibaijuka alitangaza uamuzi huo alipokuwa akizungumzia miaka miwili ya Rais John Pombe Magufuli tangu aingie madarakani wakati rais huyo akiwa kwenye ziara mkoani Kagera.

Mbunge huyo anamkubali Rais Magufuli kuwa ni mtetezi wa wajane wanaonyanyaswa na mifumo dume na kuporwa haki zao na watoto wao na kwamba wanawake hawana budi kumshukuru na kumpongeza.

Kama ilivyo kwa Airo, mbunge huyo naye amekuwa mbunge wa jimbo hilo tangu mwaka 2010 na sasa anasema anataka kuwaachia kijiti vijana wenye damu changa ili waendeleze pale atakapoishia.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# Migogoro na changamoto kwa miradi ya EAC

EAC 'inakufa' lakini kama hilo halitatokea, dalili za kudhoofika kwa uhusiano kuanzia ngazi ya moja na nyingine zimeanza kuonekana.

Mgogoro unaoendelea kati ya Uganda na Rwanda na ule wa Burundi na Rwanda ni miongoni mwa mambo yanayokwamisha mwenendo wa ukuaji wa jumuiya hiyo. Kwa maana haiwezekani nchi wanachama zikashirikiana ama kutekeleza itifaki mbalimbali za EAC, wakati zikiwa katika mgogoro.

Baada ya kushutumiana na 'vita ya maneno', Rais Yoweri Museveni wa Uganda ameonekana kujielekeza nchini Kenya ili pamoja na mambo mengine aweze kuimarisha uhusiano uliopo na kunufaika na fursa mbalimbali hasa zinazohusiana na matumizi ya bandari ya Mombasa.

Wakati hali ikiwa hivyo, Rais Paul Kagame naye akawasili Tanzania katika kile kilichoelezwa kwamba ni ziara yenye lengo la kuimarisha uhusiano wa nchi mbili hizo.

Ikumbukwe kwamba katika mpango wa ujenzi wa reli ya viwango vya juu (SGR) kutoka Bandari ya Mombasa kupitia Uganda hadi Kigali, Rwanda unaelezwa 'kusua sua' ingawa Rais Museveni katika ziara yake ya hivi karibuni nchini Kenya, amefanikiwa kuibua matumaini ya ujenzi wa kutokea Malaba palipo mpaka wa nchi hizo hadi Kampala.

Naye Rais Kagame sasa anaelezewa kujielekeza zaidi katika ujenzi wa SGR kuanzia eneo la Isaka mkoani Tabora.

### MUSEVENI AINGIA NAIROBI

Moja ya manufaa ya ziara ya Rais Museveni nchini Kenya ni kukabidhiwa ardhi na Rais Uhuru Kenyatta ili ajenge bahari kavu kwenye mji wa Naivasha.

Akiwa nchini Kenya, Museveni alifika mjini Mombasa kwa mazungumzo na Rais Kenyatta. Mazungumzo hayo yalitajwa kuwa na lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa hayo jirani.

Vyanzo mbalimbali viliripoti kuwa marais hao waliitembelea Bandari ya Mombasa na baadaye kuekelekea jijini Nairobi kwa kutumia usafiri wa treni ya SGR, hivyo kumfanya Museveni kuwa Rais wa kwanza wa kigeni kutumia usafiri huo uliofadhiliwa na China.

Wakiwa mjini Mombasa walipokelewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Usafirishaji ya Kenya, James Macharia, Gavana Hassan Joho na Mkuu wa Bandari ya Mombasa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Kenya, Daniel Manduku.

Museveni anasema kukamilika kwa SGR ya nchini Kenya kutaiondolea Uganda tatizo la ucheleweshwaji wa mizigo uliokuwa umekubuhu kutoka kwenye Bandari ya Mombasa na anaamini kwamba mradi huo utapanuliwa hadi kufika jijini Kampala, Uganda.

Kwa mujibu wa Museveni, hatua hiyo itawezesha mizigo kutoka Bandari ya Mombasa, penye urefu wa kilomita 273, kutumia saa 24 kufikishwa Kampala.

Safari ya kutumia SGR kwa marais hao ilitafsiriwa na wachunguzi wa ushirikiano wa kidiplomasia kama ishara kwa nchi mbili hizo kuufanya mradi huo ufike jijini Kampala kupitia eneo la mpaka wa Malaba, Magharibi mwa Kenya.

### MPANGO WA AWALI

Kwa mara ya kwanza, Kenya ilikusudia kujenga njia ya reli kuelekea upande wa Kusini hadi mjini Kisumu ili kuunganisha miundombinu ya kusafirisha mizigo kupitia Ziwa Viktoria kwenda bandari za Mwanza, Entebbe, Bell na Jinja nchini Uganda.

Kwa mabadiliko hayo, Kenya sasa inatanua ujenzi wa SGR kutoka Nairobi hadi bandari kavu ya Naivasha, mradi unaofadhiliwa na China.

Awamu ya kwanza ya ujenzi wa SGR

> Baadhi ya watu kwenye Bandari ya Mombasa walikuwa wanasababisha ucheleweshaji mizigo kwa makusudi. Walifikiri kwamba wanachokifanya ni hisani tu kwa Waganda, hawakujua kwamba walikuwa wanahujumu uchumi wa nchi zote Uganda na Kenya,"



Rais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto), akiwa na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Rais John Magufuli wa Tanzania (kushoto), akiwa na Rais Paul Kagame wa Rwanda.

kutokea Mombasa hadi Nairobi uligharimu Dola bilioni 3.2 za Marekani na malipo ya deni hilo yanatajwa kuwa miongoni mwa vipaumbele vya serikali ya Kenya.

Kwa mujibu wa Museveni, kabla ya kusainiwa kwa 'makubaliano ya Mombasa' wafanyabiashara wa Uganda walikuwa wakisumbuliwa na maofisa wa mamlaka za Kenya kwenye bandari hiyo na wakati mwingine kuchelewesha usafirishaji wa mizigo.

Ni kutokana na hali hiyo, Rais Kenyatta aliingilia kati ya kuwezesha mamlaka 21 zinazofanya kazi kwenye bandari hiyo kusaini makubaliano hayo yenye lengo la kuboresha mazingira na uhusiano wa kibiashara katika ushiroba wa Kaskazini.

"Baadhi ya watu kwenye Bandari ya Mombasa walikuwa wanasababisha ucheleweshaji mizigo kwa makusudi. Walifikiri kwamba wanachokifanya ni hisani tu kwa Waganda, hawakujua kwamba walikuwa wanahujumu uchumi wa nchi zote Uganda na Kenya," Rais Museveni anasema.

Kamishna Mkuu John Njiraini wa Mamlaka ya Mapato Kenya (KRA), anasema ujazo wa mizigo inayotolewa bandarini hapo kwenda Uganda umeongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ikiwa ni matokeo ya matumizi ya kituo kimoja cha forodha (SCT) na uanzishwaji wa SGR katika ushoroba wa Kaskazini.

Njiraini akasema katika mwaka huu wa fedha, idadi ya kontena za kwenda Uganda kupitia SCT hadi kufikia Februari mwaka huu ilifikia 64, 015 na kwamba zinakadiriwa kuongezeka hadi 96,015 ifikapo Juni mwaka huu.

Takwimu zinaonyesha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, idadi ya kontena za kwenda Uganda ilikuwa 62,022 wakati mwaka 2016/2017 zilikuwa 19,759.

### KAGAME AITEMBELEA TANZANIA

Wakati hali ikiwa hivyo, Rais Paul Kagame wa Rwanda alisafiri hadi jijini Dar es Salaam kukutana na Rais John Magufuli kwa kile kilichoripotiwa kuwa ni kuimarisha ushirikiano wao kati ya mataifa hayo.

Akiwa nchini Tanzania, Rais Kagame alifuatana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanza, Dk. Richard Sezibera, Waziri wa Miundombinu, Claver Gatete, Waziri wa Mambo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Olivier Nduhungirehe na Mkuu wa Intelijensia, Jenerali Joseph Nzabamwita. Ziara ya Rais Kagame inatambulishwa na vyanzo tofauti kwamba ni miongoni mwa zenye kuimarika kwa uhusiano wa nchi mbili hizo ulioanza kulegea wakati Tanzania ilipokuwa katika utawala wa awamu ya nne.

Gazeti moja linalochapishwa katika ukanda wa Afrika Mashariki limeandika kuwa ziara ya Rais Kagame ina umuhimu mkubwa kutokana na kudhoofika kwa uhusiano wake wa kidiplomasia na Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rwanda, nchi yenye eneo dogo la kijiografia isiyozungukwa ama kuwa na sehemu ya bahari inahudumiwa kupitia ushoroba wa kati, unaoanzia Dar es Salaam na ule wa Kaskazini unaotokea Mombasa kupitia Uganda.

Wachunguzi wa masuala ya kiuchumi wanasema ushoroba wa kati una umuhimu mkubwa kwa Rwanda wakati huu ambapo mgogoro kati yake na Uganda unazidi kukua, wakati Kenya ikionekana kuimarisha ushirikiano na Uganda.

Mathalani, mpango wa ujenzi wa SGR kutoka Mombasa kupitia Uganda hadi Rwanda 'umekwama' kutokana na ukosefu wa fedha, hofu kuhusu manufaa ya kiuchumi na gharama kubwa za ujenzi.

Ujenzi wa SGR hiyo yenye urefu wa kilomita 1,500 kutoka Mombasa, Kenya hadi Kigali nchini Rwanda ulitarajiwa kukamilika ifikapo 2018, lakini Kenya imefanikiwa kukamilisha hatua za awali kutokea mji huo uliopo pwani ya bahari ya Hindi hadi jijini Nairobi.

Rwanda ni mshirika wa mpango wa ujenzi wa mtandao wa reli hiyo, lakini hivi sasa inasemekana kujielekeza zaidi kwenye SGR ya Tanzania kwa ujenzi wa reli itakayoanzia Isaka mkoani Tabora hadi Kigali, Rwanda.

Inaelezwa kuwa gharama za 'njia mpya' hiyo ni pungufu ya Dola milioni 200 ikilinganishwa na kama ingejengwa kutoka Mombasa kupitia Uganda.

### NAFASI YA JPM

Hata hivyo, mchambuzi wa masuala ya uhusiano wa kimataifa ambaye pia ni Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Rwanda, Ismael Buchanan, anasema Rais Joseph Magufuli anafaa kuwa msuluhishi mzuri wa mgogoro wa Uganda na Rwanda kutokana na uhusiano mzuri alionao kwa marais wa nchi hizo.

Jambo la msingi linabaki kuwa, ni namna gani EAC inaitafsiri migogoro inayozidi kuchukua muda mrefu kwa nchi wanachama wake na njia muafaka za kufikia suluhu kabla haijatanuka, ikaenea na kuwa katika hali ngumu ya kupata suluhu yake?

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com**



Rais Donald Trump na Katibu Mkuu wa NATO, Jens Stoltenberg. **PICHA: MTANDAO**

# Marekani yarejesha ushirikiano wake na NATO

RAIS wa Marekani, Donald Trump, anaonyesha kurejesha ushirikiano na Umoja wa Majeshi ya Kujihami ya Ulaya (NATO), akimpongeza kiongozi wake na umoja huo wiki iliyopita, wakati wa mikutano yake kadhaa na katibu mkuu.

"Hatua kubwa imefikiwa ya kuboreshwa kushirikiana majukumu kati ya wanachama wa mataifa huru 29 waliosaini mkataba wa NATO, " Trump amesema, lakini akaongeza kuwa Ujerumani, ukweli haichangii kiwango kinachostahiki.

Trump amesisitiza wasiwasi wake kuwa wakati Marekani inatumia fedha nyingi kuilinda Ulaya, "wao wanatunyonya sisi katika biashara."

Trump, akiwa pamoja na Jens Stoltenberg mbele ya Ofisi ya Ikulu ya Oval, amempongeza kiongozi huyo kwa uhodari wake wa kuiongoza NATO.

"Sisi tunashirikiana vizuri kabisa," Trump amesema akimsifia waziri mkuu huyo wa zamani wa Norway.

Rais alijisifia juu ya mchango wake katika kubadilika kwa umoja huo wa NATO ambao siku za nyuma alisema kuwa ulikuwa umepitwa na wakati.

"Kama mnavyojua wakati nachukuwa madaraka, umoja huo ulikuwa hauko vizuri, hivi sasa wanapiga hatua," kwa wanachama wake kufikia lengo la kuchangia asilimia mbili ya pato lao la kitaifa (GDP) katika ulinzi.

"Lakini nafikiri lazima iwe zaidi ya kiwango hicho," ameongeza Trump.

Stoltenberg amemshukuru Rais kwa uongozi wake shupavu katika kushirikiana kwenye majukumu," akiongeza, "sisi tumechukua hatua za pamoja kukabiliana na ugaidi na tunawekeza zaidi katika hilo."

Trump aliulizwa na mwandishi kuhusu Russia, hasimu wa Vita Baridi ambayo ilipelekea kuundwa kwa umoja huo.

"Natumai kuwa haitaendelea kuwa ni tishio la usalama. Nafikiri tutaweza kushirikiana na Russia," amejibu Trump, ambaye kampeni ya uchaguzi wake 2016 ulikuwa umemulikwa na uchunguzi wa miaka miwili uliofanywa na mchunguzi maalum juu ya madai ya kuwa na mafungamano na Moscow.

Katika mikutano ya baadaye iliyofanyika katika Chumba cha Baraza la Mawaziri, Stoltenberg, akiwa upande wa pili mkabala na Trump, alisema Russia imekuwa ikikiuka mkataba wa Silaha za Masafa ya Kati za Nyuklia (INF), akieleza kuwa "Washirika wa NATO wamekuwa wakiunga mkono kikamilifu msimamo wa Marekani juu ya hilo."

Kuanzishwa Jumuiya ya Kujihami ya NATO

Mataifa kumi na mawili ya Ulaya yalianzisha Jumuiya ya kujihami ya NATO mwaka 1949. Leo hii, Rais wa Marekani Donald Trump ana wasiwasi iwapo NATO itaweza kuhimili miongo mingine saba ijayo.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa kwanza wa Jumuiya ya NATO, Lord Hastings Ismay, lengo la kuanzishwa kwa jumuiya hiyo lilikuwa kutoushirikisha muungano wa zamani wa Sovieti, kuiingiza Marekani kundini na kuiweka Ujerumani chini.

Hii ilikuwa ni baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia wakati ambapo Muungano wa nchi za Sovieti wakati huo ulipokuwa ukidhibiti nusu ya Ulaya ikiwa ni pamoja na Ujerumani Mashariki.

Ujerumani ya Mashariki haikupewa nafasi kwa muda mrefu na mwaka 1955 Serikali ya Shirikisho la Ujerumani ilijiunga na NATO. Kisha Mashariki, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ujerumani, (GDR) ikajiunga na ushirikiano wa kirafiki wa makubaliano ya Warsaw uliokuwa chini ya Udhibiti wa Umoja wa nchi za Sovieti.

Sasa ni miaka 70 imepita tangu kuundwa kwa jumuiya ya NATO na hali inafanana na ile iliyokuwapo wakati wa vita baridi, vita kwa mara nyingine. Maofisa wa Urusi walihisi kutishwa na Jumuiya ya NATO ambayo imejitanua na sasa Urusi inaimarisha majeshi yake.

Hili limesababisha jumuiya hii kutojitanua zaidi. Kwa mfano nchi za Georgia na Ukraine zimepoteza matumaini ya kujiunga na NATO kwani viongozi wa NATO wanataka kuepuka migogoro zaidi.

Pamoja na migogoro katika jumuiya hiyo, Katibu Mkuu wa sasa wa NATO, Jens Stoltenberg, amewahi kunukuliwa akieleza jinsi tofauti zinavyoendelea kuigubika jumuiya hiyo.

Amesema katika historia ya NATO kumekuwa na tofauti nyingi lakini zimeweza kutatuliwa na kwamba wanachama wote na washirika wa NATO wanafahamu kuwa Amerika ya Kaskazini na Ulaya ziko salama zaidi zikiwa pamoja.

Stoltenberg aliwahi kunukuliwa katika hotuba ya mwaka 2018 akisema haijaandikwa kwenye jiwe kuwa jumuiya hiyo itadumu milele na kwamba tofauti kati ya wanachama zipo.

Katika historia yake ya miaka 70, NATO imewahi kupitia kile kinachojulikana kama hali ambayo masharti ya muungano yaliwalazimu wanachama wote kutetea mwanachama aliyepigwa: Na hii ilitokea katika shambulio la kigaidi lililotokea Septemba 11 mwaka 2001 nchini Marekani. Hata hivyo, uamuzi huu ulileta mgogoro ambao umekuwa ukistawi kwenye jumuiya hiyo.

Katika mkutano wa mwaka 2014 wa jumuiya hiyo, viongozi walikubaliana kutenga sehemu ya mapato ya nchi zao na kuyaingiza katika bajeti ya ulinzi katika umoja huo. Kansela wa Ujerumani Angela Merkel ameahidi kutoa asilimia 1.5 ya bajeti ya ulinzi wa jumuiya hiyo mpango ambao unapingwa na chama cha SPD.

# Mafunzo ya uongozi, maisha kutoka kwa Njelu Kasaka- 1

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA historia ya siasa za Tanzania, kabla na baada ya uhuru, wamekuwapo wanasiasa wengi ambao kwa namna mbalimbali walishiriki katika maendeleo ya nchi kutokana na nafasi zao.

Wanasiasa hao ni wengi na orodha yao inaweza kujaza vitabu kadhaa. Katika orodha hiyo wamo Julius Nyerere, Rashidi Mfaume Kawawa, Aboud Jumbe, Seif Sharif Hamad, Ali Hassan Mwinyi, Joseph Warioba, Chrisant Mzindakaya, Joseph Mungai, John Malecela, Sheikh Abeid Amani Karume, Peter Siyovelwa, Salim Ahmed Salim, Bakari Mwapachu, Paul Bomani na Edward Moronge Sokoine.

Hao ni sehemu ya orodha ya wanasiasa ambao kwa nafasi zao wamefanya mambo mbalimbali katika historia ya Tanzania na wengi wao wametangulia mbele ya haki. Lakini mchango wao bado utaendelea kuwa kumbukumbu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Pamoja na wanasiasa hao, yumo Njelu Kasaka ambaye aliweka alama muhimu katika historia za Tanzania kutokana na kuibua bungeni hoja ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika. Shabaha yake hasa ilikuwa kuwapo kwa serikali tatu- ya Muungano, ya Zanzibar na Tanganyika.

Kasaka aliibua hoja hiyo ambayo ilivuta hisia za Watanzania wengi mwaka 1993. Kama wahenga wasemavyo mwanzo wa ngoma ni lele, Kasaka alianza kuzungumzia hoja hiyo wakati akichangia hotuba ya Waziri Mkuu wakati wa Bunge la Bajeti la 1993/94 na hatimaye kuendelea nayo.

Matokeo ya hoja hiyo yalizaa kundi la wabunge lililojulikana kama G55 ambalo lilisimama kidete na hatimaye kuwasilisha bungeni hoja ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika ambayo hata hivyo ilikumbana na vigingi na hatimaye azimio la kuundwa kwake kufutwa na bunge.

Mwanasiasa huyo mkongwe ambaye baada ya mwaka 2005 amekuwa akisikika au kuonekana kwa nadra, ameibuka na kuandika kitabu kiitwacho 'Njelu Kasaka Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika G55' ambacho kwa sasa kimesambaa nchini kote na kuvuta hisia za watu juu ya matukio muhimu ya kisiasa ndani ya Tanzania.

Ndani ya kitabu hicho, Kasaka ameelezea mchakato mzima juu ya vuguvugu la kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika na vigingi walivyokumbana navyo ikiwamo kutishiwa kufukuzwa uanachama.

Licha ya undani wa suala hilo, mwanasiasa huyo, ndani ya kitabu chake anaweka bayana mambo mbalimbali ambayo yanapaswa kuwa funzo kwa watu waliowahi kuwa viongozi katika siasa, taasisi za umma, binafsi na za kimataifa.

Mafunzo hayo yanatokana na mambo aliyoyafanya alipokuwa akitumika katika nafasi mbalimbali za kisiasa na zisizo za kisiasa. Kwa ujumla anatoa mafunzo ambayo ni chanya na pia yanapaswa kufuatwa na vijana ambao wanatarajia kuwa viongozi katika taasisi mbalimbali na nafasi za kisiasa.

Kasaka ambaye aliwahi kuwa meneja wa benki ya CRDB, Mbunge wa Chunya na baadaye Lupa, Naibu Waziri wa Kilimo, Mkuu wa Mkoa wa Iringa na Tabora kisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, kutokana na nafasi hizo, anatoa mafunzo muhimu kwa jamii. Miongoni mwa mafunzo hayo ni;-

> "Nyerere alitueleza kuwa kama tumeamua kuwa suluhisho la matatizo ya Muungano ni kuundwa kwa serikali ya Tanganyika, Muungano hautadumu, utakufa. Akatuomba tuachane na madai ya Tanganyika lakini tulikataa,"

**KUWA NA MSIMAMO**

Katika maisha yake ya uongozi na utumishi, mwanasiasa huyo ambaye ni msomi wa ngazi ya shahada ya uzamili katika uchumi kilimo, kupitia kitabu hicho ambacho kimesheheni historia ya maisha yake, anaonyesha ni mtu mwenye msimamo katika kila jambo analoamua na kulifanyia kazi bila kusita.

Msimamo wake, kwanza unaonekana katika suala la kusimamia hoja ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika ambalo alilisimamia mwanzo mpaka mwisho bila kuyumba. Anaeleza katika kitabu chake kuwa hata kundi lao lilipoitwa kwa ajili ya kunyamazishwa, walisimama kidete bila kujali vitisho ambavyo walikuwa wakikabiliwa navyo.

Fundisho la watu kuwa na msimamo katika eneo hilo ni pale Mwalimu Nyerere alipowaita G55 nyumbani kwake, Msasani jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mazungumzo kuhusu hoja iliyokuwa imeshika kasi - hoja ya Tanganyika.

Katika kikao hicho cha Agosti 5, 1993 Kasaka na wenzake, wakiwamo Mateo Qaresi (Babati), William Mpiluka (Mufundi), Patrick Qorro (Karatu), Abdallah Saidi Nakuwa (Lindi Mjini), Arcardo Ntagazwa (Kibondo), Mussa Nkhangaa (Singida Mjini), Jjared Gachocha (Ngara) na Jenerali Ulimwengu (Taifa) waliweka msimamo wa kutoyumbishwa.

"Nyerere alitueleza kuwa kama tumeamua kuwa suluhisho la matatizo ya Muungano ni kuundwa kwa serikali ya Tanganyika, Muungano hautadumu, utakufa. Akatuomba tuachane na madai ya Tanganyika lakini tulikataa," anasema Kasaka.

Hata katika kikao cha Agosti 14, 1993 juu ya suala la Tanganyika, kilichojumuisha baadhi ya viongozi wa CCM, serikali na wabunge, mwanasiasa huyo anasema waliendelea kusimamia hoja yao bila kuyumbishwa licha ya kwamba kulikuwa na shinikizo kubwa la kutaka hoja hiyo iondolewe.

**UFUATILIAJI WA MAMBO**

Katika eneo hilo, Kasaka anajaribu kuweka sawa kuwa mtu katika nafasi yoyote aliyopo anapaswa kuwa mfuatiliaji mkubwa wa mambo hadi kuhakikisha anafanikisha. Anabainisha hilo alipokuwa mbunge wa kawaida kwa kufuatilia umeme katika mji wa Chunya.

"Kazi yangu ya kwanza niliyoifanya nikiwa Mbunge wa Chunya ilikuwa kutembelea Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco) kuulizia mpango wa kupeleka umeme Wilaya ya Chunya hususan mji wa Chunya.

"...nilifuatana na William Mpiluka Mbunge wa Mufindi, nilifika makao makuu ya Tanesco na kukaribishwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Salvatory Mosha ... nilijitambulisha kuwa ni Mbunge wa Chunya na mwenzangu akajitamulisha kuwa ni Mbunge wa Mufindi na kwamba shida yetu iilikuwa kutaka kujua mipango ya shirika kupeleka umeme katika majimbo yetu," anasema.

Anaeleza kuwa baada ya kueleza hayo, mkurugenzi huyo wa Tanesco alianza kufuatilia sababu za Chunya kutokuwa na umeme ilhali ni mji mkongwe na wa zamani na kuagiza wataalamu wawili wanede huko kufuatilia suala hilo na kutoa taarifa ndani ya siku 14.

Kutokana na jitihada hizo, anasema umeme ulifikishwa katika mji wa Chunya Desemba 24, 1994 saa 3:00 usiku na hiyo ni kutokana na jitihada zake za kuhakikisha azima hiyo inatimia.

Pamoja na kufanikiwa huko, anaeleza bayana kwamba alianza kufuatilia jambo hilo baada ya kuapishwa kuwa mbunge Novemba 1990 na lakini mambo yalitimia miaka minne baadaye.

Hiyo ilitokana na milolongo mirefu ya ufuatiliaji kuanzia Tanesco, ilitokuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na hatimaye Wizara ya Mipango ili kuhakikisha suala hilo limewekwa kwenye mipango na kisha katika bajeti.

**Itaendelea Jumatano ijayo...**



Njelu Kasaka

# Kimbunga chamngoja Rais Trump huku akidai ‘amesafishwa kabisa’

**Na Michael Eneza**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wa chama cha Democratic ambao ndiyo wengi baada ya uchaguzi katikati ya muhula mwaka jana, wanajiandaa kuiangalia kwa kina ripoti ya mwendesha mashtaka maalum Robert Mueller, kuhusu tuhuma za Russia kuingilia uchaguzi mkuu wa Marekani mwaka 2016.

Muller alitoa muhtasari wa ripoti yake kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, William Barr, uliosema kimsingi kuwa hapakuwa na ushahidi wa kutosha kudhihirisha ushirikiano (kula njama za pamoja) kati ya Russia na timu ya kampeni ya Rais Donald Trump wakati wa uchaguzi mkuu.

Ilitosha kwa Trump kutangaza ushindi kwa kila kitu alichotuhumiwa.

Wachambuzi wa habari hata hivyo wamekuwa wakieleza kuwa hata katika muhtasari huo mwendesha mashtaka hakuthibitisha kuwa hapakuwa na njama za kuzuia ukweli kujulikana, kwani tangu aingie madarakani Rais Trump amekuwa akibadili, kufukuza kazi, maofisa Ikulu walio katika ngazi za juu hasa kuhusiana na masuala ya sheria.

Idara ya Upelelezi (wa Jinai) nchini humo, FBI imepata misukosuko ya aina hiyo ambako aliyekuwa mkurugenzi wake mkuu, James Comey, aliyeteuliwa na Rais Barack Obama mwaka 2013 aliondolewa mwezi Mei 2017, wakati shinikizo likizidi kwa Trump kuhusiana na uchunguzi wa kuingiliwa uchaguzi mkuu Marekani.

Wako wengine walipoteza nafasi zao kutokana na kuwa na shauku ya wazi kutaka kufuatilia zaidi suala hilo.

Mwendesha mashtaka au (mwanasheria mchunguzi maalum) Robert Mueller ni mtu mwenye heshima kubwa nchini Marekani, akiwa na nishani ya ushujaa katika medani ya vita nchini Vietnam, mtu mwenye uzoefu mkubwa serikalini (alizaliwa Agosti 7, 1944).

Ni mwanasheria, ofisa wa juu serikalini kwa miaka mingi na alikuwa mkurugenzi wa sita wa FBI, kuanzia mwaka 2001 hadi 2013.

Licha ya kuwa Mueller alikabidhiwa mikoba ya uchunguzi huo, ni Comey ndiye alikuwa nyota wa suala zima, kwani aligongana uso kwa uso na Trump akijaribu kufuatilia kisheria na kwa uadilifu nini kilitokea, akamuudhi Trump kuliko maelezo.

Licha ya kuwa amekuwa mfuasi wa Republican muda mwingi kimaisha, aliwahi kusema hana utii halisi kwa chama hicho.

Shughuli pevu iliyofikia hatua ya kutolewa ripoti ya Mueller hivi karibuni ilianza kitambo kidogo, wakati Comey akiwa mkurugenzi (mkuu) wa FBI (baada ya kuteuliwa na Obama mwaka



Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi. **PICHA:MTANDAO**

2013), hivyo Obama akiwa bado madarakani likazuka suala la matumizi ya barua pepe binafsi kwa shughuli za serikali kwa upande wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje muhula wa kwanza wa Obama, Hillary Clinton (zamani ‘first lady’).

Wakati suala hilo linaendelea ndio uchaguzi mkuu ukawa umewadia kuelekea mwisho wa 2016 na hapo Comey alichukua hatua za kiutawala kuhusu uchunguzi wa suala la Clinton zilizomgombanisha na pande zote mbili za kisiasa nchini humo.

Aliamua kuanza tena upelelezi wa matumizi ya barua pepe muda mfupi kabla ya kura kupigwa.

Hata hivyo uswahiba huo tarajiwa na kampeni ya Trump kwa kusaidia kuingiza kampeni ya Clinton mchangani kwa kufungua tena majalada ya hizo barua pepe haukudumu kwani baada ya utawala mpya kuingia kufuatia uchaguzi mkuu, aliendelea kuvalia njuga suala la kuchunguza kuhusika kwa Russia.

Ni mada iliyomuudhi Trump ambaye amekuwa akikosoa uchunguzi huo kuwa unavuruga matumizi ya muda na raslimali, na hauna faida yoyote.

Comey (akiwa mkuu wa FBI) aliandika barua kuwa haoni haja ya Clinton kufunguliwa mashtaka yoyote, jambo ambalo liliwaudhi wafuasi wa Trump, lakini likajulikana tu nje mwezi Desemba 2017 akiwa si mkurugenzi wa FBI, lakini ikachangia kuweka hisia za raia wa Marekani pande tofauti kuhusu uchunguzi huo.

Wafuasi wa Trump walimpinga kuwa alianza kuandika barua kuondoa mashtaka bila kukamilisha uchunguzi.

Yako maeneo ambako ripoti ya Mueller kuhusu kuingiliwa uchaguzi wa Marekani na mawakala wa Russia inafanana na hiyo barua ambayo watu wa Trump waliichukia, kwani yako maeneo mengi ambayo yanaleta dukuduku kuhusu mwelekeo wa Trump katika suala hilo.

Ila mpelelezi maalum aliona amwachie suala hilo Mwanasheria Mkuu Barr ambaye aliharakisha kusema kuwa kwa msingi wa ripoti hiyo hakuna msingi wa kufungua mashtaka yoyote, jambo ambalo haliendi sawa na hisia za wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi upande wa Democratic.

Spika Nancy Pelosi alisema katika mahojiano kuwa hawauhitaji na hawana kazi na ushauri wa mwanasheria mkuu, wanachotaka ni ripoti nzima kikamilifu ili waifanyie kazi bungeni, kuona kama kuna ushahidi wa kutosha kufungua mashtaka dhidi ya Trump kuweka vizingiti ukweli usijulikane, kudhamiria.

Vyombo vya habari vya Marekani vinasema kuwa baada ya kufukuzwa (ukurugenzi FBI) mwezi huo huo Comey alielewana na rafiki yake, Daniel Richman ambaye ni profesa wa ‘Chuo Kikuu cha Columbia (jijini New “York) kuvujisha kwa vyombo vya habari angalizo (memo) aliyoiandika baada ya mkutano kati yake na Rais Trump. Ilisema Trump alimwambia amalize uchunguzi wa FBI dhidi ya Michael Flynn, aliyekuwa mshauri wa masuala ya usalama wa taifa katika Ikulu ya Trump.

Kwa maana hiyo kufukuzwa kwa Comey, angalizo hilo na ushahidi ambao Comey alitoa kwa kamati ya Bunge la Marekani ni uthibitisho kwa watu wengi au wachunguzi walio wengi nchini humo kuwa Trump alifanya juhudi za wazi na bila kificho kuzuia ukweli wa suala la Russia.

Ndiyo maana wakinzani katika vyombo vya habari na bungeni hawaoni kuwa ripoti ya Mueller ndiyo mwisho wa suala hilo, kinyume na tangazo la ushindi la Trump - na hata kuvuka mpaka, akidai kuwa walioweka ajenda ya uchunguzi huo walifanya ‘vitendo vya kihaini,’ yaani hawana uzalendo kwa nchi yao!

Alisema kuwa kuna haja ya watu hao kuchunguzwa - jambo ambalo halielekei kuwa lina maana ya kugusa itikadi zao, misimamo yao kuhusu uchaguzi mkuu, ila kama kuna maslahi maalum yaliyowasukuma.

Inakuwa kana kwamba ni wao ndio wanahitaji kuchunguzwa kuhusiana na taifa kubwa la nje kuingilia uchaguzi wa Marekani na mfaidika wa hali hiyo kuonyesha waziwazi hataki suala hilo liguswe, ila tu haijathibitishwa kama alishirikiana nao.

Lakini Bunge sasa linataka kuangalia kama kuna ushahidi wa kutosha kuwa Trump alitaka kuzuia ukweli usijulikane hasa katika jitihada ya FBI pale mwanzoni, halafu kumfukuza kazi mkurugenzi wake na aliyoyasema akiongea nao.

MAKALA

# Ulaya waichoka Uingereza 'kuangukia pua', sasa Aprili 12 hali isipobadilika

Na Nimi Mweta

ULAYA pamoja na Uingereza wako katika mchecheto wa kihistoria, kama vile kungoja 'kiama'; ambacho saa yake imetangazwa na kila mtu anajua ni lini, lakini hakuna la kufanya kuondoa madhara ya hali hiyo.

Ndicho kinachotokea katika mtiririko wa matukio ya kukamilisha mpango wa Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya (EU), hatua ambayo Ulaya walikubali kuiahirisha kwa wiki mbili endapo hakuna mpango unaokubalika wa jinsi ya kujitoa, na mwezi mmoja endapo mpango huo utakuwa umepitishwa.

Ni mpango wa pili na wa mwisho uliokubaliwa kati ya serikali ya Theresa May na nchi 27 za Ulaya (Tume ya EU na mkutano wa wakuu wa nchi).

Tatizo ni kuwa mpango huo umekataliwa kwa kura nyingi, kwani wabunge wa upinzani (hasa chama cha Labor) wakiupinga na sehemu isiyo ndogo ya chama tawala, Conservative, kwa sababu zinazotofautiana.

Wakinzani ndani ya Conservative wanahisia kuwa bado kuna maeneo mengi yatakayoendelea chini ya mpango huo badala ya Uingereza kujitoa kikamilifu, wakati wengine wanachelea athari za kuondoa makubaliano ya kibiashara au kujitoa kabla ya makubaliano maalum kama umoja wa forodha kufikiwa.

Ndiyo pendekezo mbadala ambalo lilipata kura nyingi wakati wabunge waliposhindwa kupitisha mojawapo kati ya mapendekezo nane 'mbadala.'

Wakati May alipoanguka tena akifikisha kitu kama rasimu fupi ya kujitoa ambayo msingi wake ni mkataba uliokataliwa, ili angalau kuwe na mwelekeo wakati wa kujitoa, bado inaaminika kuna uwezekano wa 'kitu fulani' kukubaliwa katika wiki moja iliyobaki, hadi Aprili 10.

Endapo hadi tarehe hiyo Uingereza haitakuwa imepeleka waraka wowote kuhusu walichokubaliana kilicho thabiti kiasi cha kutosha, EU itakuwa tayari kutangaza kuwa siku mbili baadaye Uingereza itachupa nje ya Ulaya bila makubaliano.

Kwa maana hiyo biashara kati yake na EU itaanza kutawaliwa na kanuni za Shirika la Biashara la Umoja wa Mataifa (WTO).

Inahofiwa kuwa hali hiyo italeta mlolongo wa malori kuingia na kutoka nchi za EU, na wakazi wa Uingereza walioko katika nchi hizo kufumba na kufumbua waombe upya vibali vya kukaa katika nchi hizo na kufanya kazi, jambo ambalo si rahisi katika hali ya kawaida.

Pia kuna wasiwasi kuwa kuingiza bidhaa za Uingereza katika jedwali la kodi zinazotozwa kwa nchi za nje na siyo za EU kutafanya bidhaa hizo kukosa soko nchi nyingi za Ulaya wakati ndiyo tegemeo katika sekta kadhaa, hasa kilimo, maziwa nyama, n.k.

Na isitoshe kuna suala la mpaka kati ya Ireland ya Kaskazini na Jamhuri ya Ireland, kuwa usiwe mpaka mgumu (vizuizi, vibali, hati za kusafiria) kwani itaanza kuleta sokomoko katika uthabiti wa kisiasa, mikataba ya utawala iliyomaliza machafuko.

Jambo la kushangaza ni kuwa wakati wabunge wa Conservative wameshindwa kumpa May ushirikiano anaohitaji ili kukamilisha zoezi la kujitoa EU (Brexit, kikwao) bado hawana mbadala wa nani anaweza kuwa waziri mkuu badala yake, kwani hakuna ambaye mpango wake au mwelekeo wake kuhusu suala hilo unaweza kupata kura za kutosha bungeni.

Mmojawapo ni aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Boris Johnson, ambaye ni moja ya wale wanaounga mkono Uingereza kujitoa kwa haraka zaidi ya kinachoonekana kwa Waziri Mkuu, akishirikiana na mkereketwa-mtanashati mwingine, Rees-Mogg.

Viongozi wa Ulaya kimsingi wamekuwa wakimsikitia May, kwani Bunge la Uingereza linajua hakuna mkataba bora zaidi ya huo unaoweza kupatikana kutoka Umoja wa Ulaya, lakini kila kundi bungeni linataka Ulaya ilegeze hiki au kile, hadi liridhike!

Kwa maana hiyo imefika mahali Ulaya inangoja Uingereza ifanye uamuzi na inaelekea haiwezi kabisa kufanya maamuzi yoyote, hali inayoiweka katika hali ngumu kutoka bila makubaliano yoyote au kukiri kuwa imeshindwa kutoka.

Mazungumzo na wananchi katika mitaa tofauti jijini London na kwingineko yanaonyesha kuwa tofauti zilizokuwapo kati ya sekta mbalimbali na hisia tofauti za kimaslahi na kiitikadi kuhusu Umoja wa Ulaya kimsingi ziko pale pale na kwa maana hiyo suala la kupigia kura tena suala hilo bado haliko mezani bungeni, halitakiwi.

Ina maana kuwa uwezekano wa kuchupa bila mkataba unakubalika zaidi kwa wabunge wengi wa Conservative kuliko kufikia mkataba ambao kimsingi unakubalika EU, kwani matakwa yao na masharti ni kile wanachokataa.

Wakati wapigakura wa Uingereza waliporudisha wingi wa kura kwa Uingereza kujitoa, mwaka 2016, kulikuwa na athari za wazi kuonyesha kuwa azima hiyo haitatekelezwa kwa urahisi, kwani chama cha Labour kilifikia mkanganyiko ambako kiongozi wake bungeni, David Miliband aliachia ngazi.

Suala la msingi lilikuwa ni kushindwa kufanya kampeni ya dhati kupinga kujitoa Ulaya, ikatafsiriwa na wabunge wenzake kuwa kampeni yake legelege ilisaidia mkondo wa kujitoa Ulaya kupata wingi wa kura - hali ambayo baadhi yao walisema haikutarajiwa.

Kwa upande wa pili, chama cha Conservative kiliamini kuwa hali hiyo (dhamira ya kujitoa) sasa imethibitishwa, hivyo baada ya miezi michache, akihisi kuwa kuna migawanyiko hata katika chama tawala kuhusu mkakati wa kujitoa, May akaitisha uchaguzi mkuu uliowahi zaidi - akapoteza viti, akaweka Brexit juani.

Kwa maana hiyo mkanganyiko ulipo sasa ni kielelezo kuwa suala hilo limeendelea kuwagawa Waingereza kwa kina na hata kura nyingine ya maoni ingepigwa mgawanyiko huo ungetokea na kushamiri kama ilivyokuwa awali.

Ila kwa sababu kura ya maoni tayari ilishapigwa na jibu la 'kujitoa' likapatikana, chama tawala hakina nia yoyote ya kulipeleka suala hilo kwa wapigakura kuona kama bado kuna wingi wa kutaka kujitoa au hapana, kwani ni kama kuteka nchi wakati wa vita kugombea mpaka au umiliki wake, halafu baadaye mazungumzo yafanyike nchi iliyotekwa irudishwe.

Conservative walishashinda kuhusu suala la kujitoa Ulaya, hivyo kura zote hizo ni kuwasikiliza tu wapinzani na makundi tofauti ya washika dau nchini humo, bila kubadili suala la msingi.

Ukimsikiliza May, kuna jambo moja tu ambalo ana uhakika nalo ni 'Brexity,' yaani dhamira ya Uingereza kujitoa na siyo itajitoa endapo itakuwa imefikia makubaliano na Ulaya.

Itajitoa kwa makubaliano ikiwezekana na bila makubaliano ikishindikana, kwani tatizo kuhusu makubaliano halipo Ulaya ila Uingereza, kwani hitaji la makubaliano lazima liendane na pande zote mbili na hakuna upande unaoweza kuweka kipaumbele hisia za upande wa pili na siyo za kwake mwenyewe kama wabunge wa Uingereza wanavyoonekama kuikoromea Ulaya.

Nchini Uingereza vilevile, hakuna kiwango cha kukoromeana kinachoweza kuwabadili wanaotaka hili au lile katika maslahi yao lifikiwe kwanza kabla ya kuunga mkono mpango wa kujitoa.

Ila kwa vile kujitoa hakuna mpango, na May hajawahi kuzungumzia sharti la kushiriki uchaguzi wa Bunge la Ulaya ili kuweza 'kusikilizia' kwa muda mrefu zaidi, ni wazi kuna mazingira ya kujitoa Ulaya, hata ingekuwa ni kwa kuangukia pua.

Ni kama maumivu ya hapa na pale ambayo yatapona kwa muda, siyo kuingia mkataba ambao mazingira yake ni kero tu.




Baadhi ya waandamanaji wanaotaka Uingereza ijitoe mara moja katika Umoja wa Ulaya (EU). **PICHA: MTANDAO**

"Ila kwa vile kujitoa hakuna mpango, na May hajawahi kuzungumzia sharti la kushiriki uchaguzi wa Bunge la Ulaya ili kuweza 'kusikilizia' kwa muda mrefu zaidi, ni wazi kuna mazingira ya kujitoa Ulaya, hata ingekuwa ni kwa kuangukia pua.



# Halmashauri yatenga fedha ujenzi uzio wa stendi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imetoa kiasi cha Sh. milioni 10 kwa ajili ya kujenga uzio na kukarabati kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani kilichopo katika kata ya Sisimba.

Akizungumza na Nipashe, Diwani wa Kata ya Sisimba, Geofrey Kajigili, alisema fedha hizo zilitolewa kwa lengo la kujenga uzio kuzunguka stendi na kukarabati upya stendi hiyo, ambayo alidai haiendani na hadhi ya Jiji la Mbeya kutokana na uchakavu wa miundombinu.

Kajigili alisema stendi hiyo ya mkoa inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ufinyu wa eneo kwa ajili ya magari kupaki au kuingia na huduma nyingine ikiwamo jengo bora la kupumzikia abiria.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa kuzunguka stendi hiyo ya mabasi yaendayo mikoani na maeneo mengine ya Mkoa wa Mbeya kutasaidia kuongeza mapato ya halmashauri.

"Tunatarajia stendi yetu kuwa ya kisasa kwa sababu itakuwa kubwa na itafanya kazi saa 24, tunachokiomba ni abiria na madereva kukabiliana na changamoto ambazo zitajitokeza wakati wa shughuli za ujenzi zitakapokuwa zikiendelea," alisema Kajigili.

Aliwahakikisha wafanyabiashara wa eneo hilo, miundombinu yao itaboreshwa vizuri ulikinganisha na ilivyo sasa na kuwasisitiza kunufaika na stendi hiyo ambayo baada ya kukamilika itakuwa na uwezo mkubwa wa kutoa huduma za usafi na usafirishaji kwa saa 24.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema lengo la ujenzi huo ni kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuwa biashara mbalimbali zitafanyika, lakini magari mengi pia yataingia na kutoka hapo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akizungumza na wafanyakazi wa benki hiyo tawi la Tunduma hivi karibuni, wakati akihitimisha ziara yake ya kibiashara aliyoifanya katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba kujengewa daraja Mto Mbaka

**Na Mwandishi Wetu, KYELA**

WANANCHI wa Kijiji cha Ilondo, Kata ya Mwaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwajengea daraja la kudumu katika Mto Mbaka ambao umetajwa kuwa tishio kwa maisha ya watu kutokana na idadi kubwa ya mamba.

Waliyasema hayo jana walipokuwa wanazungumza na Nipashe ambapo walieleza kuwa wanatumia daraja ambalo sio la kudumu wala imara ambalo linahatarisha maisha ya wananchi wanaotumia daraja hilo.

Mmoja wa wananchi hao, Gwamaka Mwakyusa, alisema daraja wanalolitumia kwa sasa siyo salama kwa kuwa linaharibika mara kwa mara kitendo kinachohatarisha maisha yao.

Alisema wanalazimika kutumia daraja hilo kwa sababu ndio kiunganishi pekee cha mawasiliano ndani ya Kijiji cha Ilondo na kwamba pindi linapoharibika wananchi hushindwa kufuata huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo mengine.

"Mto wa Mbaka ni hatari kwa sababu wananchi wengi wamepoteza maisha kwa sababu ya kuuliwa na mamba, aidha, kwa kudumbukia au kuzama wakati wa kuogelea, tulijitahidi kujenga daraja ya muda ili kunusuru hali hiyo na wananchi, lakini changamoto iliyopo ni daraja hilo kuharibika mara kwa mara hasa kipindi hiki cha msimu wa mvua, ambapo mto umejaa tunaiomba serikali itusaidia kujenga daraja la kudumu ili kuondokana na hali hii," alisema Gwamaka.

Buponelo Japhet alisema daraja hilo linaharisha maisha ya watoto wanaokwenda shuleni hasa wa darasa la kwanza mpaka la sita huvushwa kwa kutumia mitumbwi.

Akizugumzia tatizo hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ilondo, Atukuzwe Mwambaka, alisema baadhi ya wananchi wake walijeruhiwa na mamba na wengine kuumia wakitembea ndani ya daraja hilo.

Alisema mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha wananchi kutumia mitumbwi kuvuka badala ya daraja kwa ajili ya kufanya shughuli zao za uzalishaji hasa za kilimo cha mpunga.

Aliongeza Diwani wa Kata ya Mwaya, Absolom Mwankemwa, aliahidi kujenga daraja la kudumu katika Mto Mbaka, lakini ameshindwa kutimiza kwa sababu ya kusumbuliwa na maradhi kwa kipindi kirefu sasa. Kijiji cha Ilodo ni moja kati ya vijiji vyenye uhitaji mkubwa wa madaraja ya kudumu wilayani Kyela vikiwamo pia vijiji vya Ipande na Kyangala.

# Wakulima mpunga wachekelea skimu ya umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu, MOMBA**

WAKULIMA wa zao la mpunga wanaonufaika na skimu ya umwagiliaji ya Naming'ongo katika Kata ya Chitete Wilaya ya Momba mkoani Songwe, wamesema uzalishaji wa zao hilo umeongezeka kutoka gunia 10 kabla ya mradi hadi gunia 15 kwa hekari moja.

Wakizungumza na Nipashe wakulima hao walisema, mradi wa skimu umeleta matokeo mazuri kwenye zao la mpunga kwa kuwa umeongeza tija na kipato kwa mkulima.

Miongoni mwa wakulima hao, Aloyce Baton, alisema katika msimu huu wa kilimo ambao umekuwa na mvua za kusuasua skimu ya umwagiliaji ya Naming'ongo imekuwa msaada, kwa kuwa wanaendelea kumwagilia mazao yao.

Alisema licha ya skimu hiyo kuwa msaada kwao, lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya kupata maji kwa wakati kutokana na mirefeji iliyopo kutokidhi mahitaji.

"Mifereji iliyopo haitoshi kuhudumia wakulima wote ndani ya skimu, hivyo tunaiomba serikali kupitia wataalamu wao kuongeza mirefeji ambayo itatosheleza mahitaji," alisema Baton.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Oscar Adam, alikiri kuwa mifereji ya maji iliyopo haitoshi kuhudumia wakulima na kwamba wataendelea kuboresha iliyopo na kuongeza mifereji mingine.

Adam alisema inatakiwa kuboreshwa lakini kwa tatizo lililopo tayari hatua zilishachukuliwa isipokuwa baadhi ya wakulima wameshindwa kufuata maelekezo ya wataalamu.

"Tunaendelea na jitihada za kutafuta fedha ili kujenga mifereji mingine katika skimu hiyo, ili wakulima waongeze uzalishaji kwenye mazao yao, lakini tunawaomba wakulima waendelee kuitunza mirefeji iliyopo," alisema Adam.

**"Mifereji iliyopo haitoshi kuhudumia wakulima wote ndani ya skimu, hivyo tunaiomba serikali kupitia wataalamu wao kuongeza mirefeji ambayo itatosheleza mahitaji," alisema Baton.**





# Wakumbushwa kulipa kodi ya pango

Na Peter Mkwavila, DODOMA

WAFANYABIASHARA wa masoko katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma wametakiwa kulipa kodi ya pango kwa ajili ya vibanda vya biashara kwa wakati ili kuepukana na usumbufu wakati wa zoezi la ukaguzi.

Aidha, wafanyabiashara hao wametakiwa kuhakikisha wanakuwa na mikataba halali ya upangaji katika vibanda vyao ili wawe huru katika kufanya biashara zao.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa soko la Chang'ombe wakati wa zoezi la kukagua na kuhamasisha ulipaji kodi ya pango pamoja na mikataba.

Akizungumza kwenye ukaguzi huo ambao unaendelea kufanyika katika masoko yote ya jiji, alisema kuwa zoezi hilo pamoja na ushauri wa kuwataka kulipa kwa wakati na kujaza mikataba halali, limefanikiwa kutokana na elimu inayoendelea kutolewa kwa wafanyabiashara.

"Kumekuwapo na mwitikio mkubwa kati ya wafanyabiashara na Jiji katika utoaji wa ushirikiano wa ulipaji kodi na ujazaji wa mikataba halali, hii ni kutokana na elimu ambayo inayoendelea kutolewa hadi sasa kwa wafanyabiashara wote kwa mujibu wa maelekezo husika," alisema.

Awali akizungumza na wafanyabiashara wa masoko ndani ya Jiji aliwashauri kufanya biashara zao kwenye maeneo maalumu yaliyotengwa kwa shughuli hizo badala ya kupanga holela.

Alisema kuwa hivi sasa kumekuwapo na uvamizi kwa wafanyabiashara ambao wanaopanga biashara zao maeneo yasiyo rasmi, suala ambalo limekuwa likikwamisha fursa ya matumizi ya miundombinu kama njia za watembea kwa miguu na wale waendesha vyombo vya moto.

Ofisa masoko huyo huyo pia alisema kuwa pamoja na mwitikio wa wafanyabiashara waliouonyesha kwa upande wa halmashauri, imebainika baadhi yao wamelimbikiza madeni yao ya kodi na pango kwa muda mrefu, hali ambayo imekuwa ikisababisha kuikosesha mapato ya halmashauri.

Alisema hali hiyo imechangia pia kutokamilika kwa wakati malengo iliyojiwekea Halmashauri ya Jiji ndani ya masoko, suala ambalo limedhoofisha jitihada za serikali katika kupeleka huduma za kimaendeleo kwenye miradi yake.

**"Kumekuwapo na mwitikio mkubwa kati ya wafanyabiashara na Jiji katika utoaji wa ushirikiano wa ulipaji kodi na ujazaji wa mikataba halali, hii ni kutokana na elimu ambayo inayoendelea kutolewa hadi sasa kwa wafanyabiashara wote kwa mujibu wa maelekezo husika," alisema.**

# Wataalamu nchini Marekani sasa kuzuru miradi chakula

Na Peter Mkwavila, DODOMA

WATAALAMU wa kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Cornell, nchini Marekani wanatarajia kuwasili jijini Dodoma kwa ajili ya kutembelea miradi ya uhakika ya chakula kwa mbinu ya kilimo hifadhi katika wilaya ya Bahi na Chamwino mkoani hapa inayotekelezwa na Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT).

Miradi hiyo inayolenga kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi inatekelezwa na DCT kwa ushirikiano na Episcopal Relief and Development (ERD) ya New York nchini Marekani.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo DCT, Lister Nyang'anyi, alisema ziara hiyo itajikita katika kufanya utafiti na tathmini shirikishi ya miradi hiyo.

"Lengo kuu ni kuangalia kwa kiasi gani DCT kupitia miradi hiyo inawawezesha wakulima katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, mafanikio, changamoto na kutoa mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto hizo kwa ajili ya matokeo chanya," alisema.

Aliongeza kuwa, katika ziara hiyo wataalamu hao watapata fursa pia ya kutembelea Chama cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima (TCCIA), mkoani Dodoma.

"Lengo la kutembelea TCCIA ni kujifunza kwa pamoja na kubadilishana uzoefu juu ya mbinu mbalimbali ambazo taasisi ya TCCIA inawezesha jamii katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Aidha, aliongeza kuwa malengo mengine ni kujifunza mbinu za kilimo, kilimo hifadhi, mazao yanayoliwa, mifugo na mifumo ya ufugaji, mifumo ya kilimo pamoja na mbinu za uvunaji maji shambani.

Kwa upande wake Katibu wa TCCIA, mkoani Dodoma, Idd Senge, alisema wamefurahi kupata fursa ya kutembelewa na wataalamu hao.

"Ugeni huu ni muhimu kwetu kwani utatupa fursa ya kujifunza mambo mengi kutoka kwa wataalamu hao," alisema Senge.

Pamoja na hayo aliongeza kuwa TCCIA wamejipanga vyema katika kufanikisha zoezi hilo shirikishi linalolenga kuboresha ufanisi wa sekta za kilimo na chakula katika wilaya husika.



Meneja wa Benki ya Abc Mkoa wa Dodoma, Anna Weswasi (kulia), akimkabidhi msaada mtoto Damaris Mhembano wa kituo cha yatima Kijiji cha Matumaini jijini Dodoma, kwa niaba ya watoto wanaotunzwa hapo. Benki hiyo ilitoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni moja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jamii yaombwa kusaidia wenye mahitaji

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

JAMII imeombwa kujitokeza kuwasaidia watu wenye mahitaji katika maeneo mbalimbali ili wasijione kuwa wametengwa.

Ombi hilo lilitolewa jana na Meneja wa Benki Abc, Anna Wesiwasi, wakati wafanyakazi wa benki hiyo walipokwenda kukabidhi msaada katika kituo cha watoto yatima cha Kijiji cha Matumaini jana.

Wesiwasi aliiomba jamii kujitokeza kuwasaidia wahitaji wanaotunzwa kwenye vituo na wale walioko majumbani ili wasijisikie kutengwa kutokana na kukosa mahitaji muhimu.

"Watoto hawa hawakupenda kuishi katika mazingira haya ila kutokana na kukosa wazazi hivyo wanahitaji faraja kutoka kwetu sote," alisema.

Meneja huyo alisema benki hiyo imetoa msaada huo kutokana na kupata faida katika biashara yake hivyo ni wajibu kuirudishia kwa jamii katika kuendelea kuunga mkono serikali.

Alitaja vitu walivyokabidhi katika msaada huo kuwa ni unga wa ngano, sukari, juisi, pipi, mafuta ya kula na ya kujipaka, daftari na kalamu.

Alisema thamani ya vitu hivyo walivyokabidhi ni zaidi ya Sh. milioni moja, na wataendelea kurudisha faida zaidi kwa wananchi kwa kutoa vitu mbalimbali.

Kwa upande wake mlezi wa kituo cha watoto yatima wa Kijiji cha Matumaini, Sista Consolata Nyongo, alisema kituo hicho kinatunza watoto 150 wanaoishi kwa matumaini wa kuanzia umri wa siku moja na kuendelea.

Sista Nyongo, alisema miaka ya nyuma kituo hicho kilikuwa kikipokea misaada kutoa nje ya nchi, lakini kutokana na hali ya uchumi kuyumba duniani wafadhili hao hawaleti tena misaada kwa hiyo wamebaki kuwategemea wasamari wema hapa nchini.

"Tunamshukuru Mungu wasamaria wema na taasisi nyingi zimekuwa zikijitokeza kutoa misaada kila wakati na tunawaomba wasichoke kuwasaidia watoto hawa," alisema.

Alisema kituo hicho kinatunza watoto ambao wazazi wao wamefariki kutokana na ugonjwa wa Ukimwi na wakati mwingine wamekuwa wakiletwa wakiwa kwenye hali mbaya.

Aliwaomba wasamaria wema kuendelea kujitokeza kuwasaidia kutokana na idadi kubwa ya watoto wanatunzwa hapo kwa sababu wapo wanaosoma shule za msingi na sekondari na wengine wapo vyuo vya ufundi na chuo kikuu.



# Waziri aagiza kuharakisha kwa utungwaji wa kanuni

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Maalim, amezitaka taasisi zinazosimamia sheria kuharakisha utungaji wa kanuni kwa kuwa kikwazo hicho kinasababisha zishindwe kutumika.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na watendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria katika eneo la Vuga Mjini Unguja alipofika katika tume hiyo kujitambulisha baada ya kuteuliwa katika nafasi hiyo hivi karibuni.

Alitaka tume hiyo ya kurekebisha sheria kuzipatia elimu taasisi zinazosimamia sheria ili kuharakisha utungwaji wa kanuni kwa sheria ambazo zimeshapitishwa.

Miongoni mwa sheria ambazo zimeshapitishwa, lakini zinashindwa kutumika kutokana na kukosa kanuni ni sheria ya mikataba na sheria ya ajira na uhusiano kazini.

Aidha, aliwataka watumishi wa tume hiyo kufuata sheria za utumishi wa umma kwa kuwa kuna baadhi ya watumishi wamekuwa wakikiuka sheria hiyo kwa kutohudhuria kazini bila ya sababu za msingi.

"Wapo baadhi ya wafanyakazi wamekuwa watoro kazini na hawafiki kwa wakati, hivyo ni vyema kuacha tabia hii," alisema.

Aliwataka wafanyakazi hao kuwa na umoja na ushirikiano ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ikiwamo kuzipitia sheria na kuzifanyia marekebisho pale panapohitajika.

"Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, hivyo bila ya ushirikiano ufanisi wa kazi utashindwa kupatikana," alisema.

Aliwataka wafanyakazi hao kujiendeleza kielimu na wasiridhike na elimu waliyonayo ili kuweza kupata fursa mbalimbali.

Naye Mwenyekiti wa Tume hiyo ya Kurekebisha Sheria, Jaji Bakari Mshibe, alisema kuwa sheria ndio moyo wa nchi, hivyo bila ya kuwapo nchi inaweza kuingia katika machafuko.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi B, Ali Abdallah Natepe (kushoto), akipokea alama ya funguo wa gari kutoka kwa Ofisa Mauzo wa Kampuni ya GF Trucks, Filbert Peter, wakati wa hafla ya kukabidhi magari na mitambo ya kubebea takataka katika halmashauri hiyo, mjini Zanzibar jana. Katikati ni Meya wa Halmashauri hiyo, Maabad Ali Maulid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kampuni yajipanga usafi kukabiliana masika

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAKATI mvua za masika zikiendelea katika maeneo mengi ya Tanzania, Manispaa ya Wilaya ya Magharib B Unguja imejipanga kikamilifu kuhakikisha hali ya usafi wa mazingira unaimarika.

Kuimarika kwa usafi huo kunatokana na manunuzi ya vifaa vipya vya usafi ikiwamo magari na mtambo maalumu wa kukusanyia taka, ambapo jumla ya Sh. milioni 400 zimetumika katika ununuzi wa vifaa hivyo.

Akizungumza mjini Zanzibar wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ali Abdalla Natepe, alisema ununuzi wa vifaa hivyo utaongeza ufanisi mkubwa katika ufanyaji wao wa kazi za kila siku.

Baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa ni toroli, ndoo za kuhifadhia taka, vifaa maalumu vya kujikinga na uchafu (glovers), fagio, magari, mtambo wa kukusanyia taka aina ya XCMG na FAW vyote kutoka kampuni ya GF Trucks & Equipment LTD.

Alisema ununuzi wa vifaa hivyo utasaidia kupunguza tatizo la mrundikano wa taka katika halmashauri hiyo.

**Akizungumza mjini Zanzibar wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ali Abdalla Natepe, alisema ununuzi wa vifaa hivyo utaongeza ufanisi mkubwa katika ufanyaji wao wa kazi za kila siku.**

# RC akemea wanaodhalilisha thamani ya noti

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amepiga marufuku matumizi mabaya ya fedha.

Mkuu wa Mkoa huyo alitoa rai hiyo baada ya kuwapo kwa vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watu katika sherehe mbalimbali za harusi kutunzana fedha kwa mitindo mbalimbali, ikiwamo kuzishona kama nguo na kuzibandika katika miamvuli au vikapu.

Mkuu wa mkoa huyo alitoa kauli hiyo wakati akifungua mafunzo ya uwekezaji na udhamini wa fedha na mikopo kwa watendaji mbalimbali wa serikali yaliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Alisema ni vyema wananchi wakakumbuka kuchezea fedha bila kujali gharama kubwa ya serikali ya kuzitengeneza, atambue kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Alieleza kuwa ni vyema kila mmoja akaheshimu sheria na kanuni za nchi bila ya kujiingiza katika matatizo kwa kuchezea fedha kinyume na taratibu.

"Kwa mujibu wa sheria, fedha hairuhusiwi kuharibiwa kwa njia yoyote ile, kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria, " alisema.

Mkurugenzi wa Benki ya Tanzania Ofisi ya Zanzibar, Yahya Ali Sejuko, alisema kuiharibu fedha ni kosa na iwapo mtu atagundulika anaweza kushtakiwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Wakizungumza na Nipashe kuhusiana na kauli hiyo ya serikali, wananchi wa Zanzibar walisema kuwa wanaunga mkono kauli hiyo kwani baadhi ya watu walikuwa wakifanya kufuru katika sherehe za maharusi.

"Kwa kweli kuna kufuru kubwa inayofanyika siku hizi katika shughuli yetu, utakuta watu wanatunzana tenga ambalo limefumwa kwa noti halali wakati baadhi ya watu wanashinda mitaani hawana chakula," alisema Asha Ali mkaazi wa Mjini Unguja.

Aidha, alisema kitendo hicho cha kuzisanifu fedha kwa mitindo mbalimbali zinajenga matabaka kwa wale waliokuwa wana shida na wale ambao wanafanya vitendo hivyo kwa kujionyesha hadi katika mitandao ya kijamii.

Aliishauri serikali kutekeleza agizo hilo kwa vitendo ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia ya kuzichezea fedha.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 8 April**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 9 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 10 April**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 11 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 12 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 13 April**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 14 April**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 8 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 9 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 10 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 11 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 12 April**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 13 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 14 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |







## CAPITAL RADIO

**CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM**
**FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE**

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

HABARI KIMATAIFA

# Waandamanaji waomba mazungumzo na jeshi

**KHARTOUM,** Sudan

WAANDAMANAJI Sudan wameendelea kuandamana kwa siku tatu mfululizo karibu na makao makuu ya jeshi la nchi hiyo, yaliyopo jijini Khartoum.

Juzi waandamanaji hao waliomba mazungumzo ya moja kwa moja na jeshi kwa ajili ya kuundwa serikali ya mpito itakayochukua nafasi ya Rais Omar Al-Bashir, msimamo wa hivi karibuni wa jeshi nchini humo unaonekana kuwapa nguvu waandamanaji hao.

Katika taarifa iliyosomwa mbele ya watu zaidi ya 40,000 waliokusanyika tangu Jumamosi mbele ya makao makuu ya jeshi yaliyopo katikati mwa Jiji la Khartoum, ujumbe wa upinzani ulitoa wito wa kumtaka Rais Omary Al-Bashir na serikali yake wajiuzulu.

**Magari ya jeshi sasa yanazuia njia zote zinazoelekea eneo hilo, ambapo waandamanaji wamekusanyika. Waandamanaji sasa wanapewa ulinzi na jeshi.**

Taarifa hiyo ilitaka kuundwa kwa baraza kuu litakalo wajumuisha wawakilishi wa jeshi na waandamanaji ili kujadili utaratibu wa kuondoka kwa Rais Al-Bashir na pia kuundwa kwa serikali ya mpito.

Hayo yanajiri wakati vikosi vya usalama vimezingira maeneo kadhaa katika mji mkuu wa Sudan tangu wiki iliyopita, ili kukabiliana na watu wanaoelekea karibu na makao makuu ya jeshi, ambapo wamekusanyika waandamanaji.

Juzi, kulitokea makabiliano kati ya jeshi na vikosi vya usalama wakati baadhi ya maofisa wa polisi walipojaribu kurusha risasi hewani na mabomu ya kutoa machozi kwa lengo la kuwatawanya waandamanaji.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kumekuwa na hali ya sintofahamu katika jeshi na kwamba vitengo kadhaa vya jeshi vimeasi amri ya waziri.

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari, Chawgui Abdel Azim ambaye alihojiwa na redio ya kimataifa ya Ufaransa (RFI), alitoa ushuhuda juu ya ushirikiano huo wa baadhi ya askari na waandamanaji.

"Magari ya jeshi sasa yanazuia njia zote zinazoelekea eneo hilo, ambapo waandamanaji wamekusanyika. Waandamanaji sasa wanapewa ulinzi na jeshi. Vikosi vya usalama na wanamgambo wanaotoa msaada kwa vikosi hivyo hawawezi kuthubutu tena kuwatawanya," alisema Azim.

Juzi jioni Waziri wa Ulinzi alibaini kuwa vikosi vya jeshi vinaelewa sababu za maandamano na havipingi malalamiko au madai ya wananchi, lakini havitokubali nchi itumbukie katika machafuko. **RFI**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres (kushoto), akifanya mazungumzo na Mkuu wa Jeshi la Libyan National Army, Kamanda Khalifa Haftar, walipokutana Benghazi. **PICHA: REUTERS**

# Israel yapiga kura, Netanyahu akiwania muhula wa tano

**YERUSALEM,** Israel

WANANCHI wa Israeli wamepiga kura jana, kuwachagua wabunge 120 wa Baraza la Wawakilishi, uchunguzi ambao umeonyesha kuwa vyama vinavyomuunga mkono Waziri Mkuu anayemaliza muda wake, Benjamin Netanyahu vitaibuka na ushindi.

Chama cha mrengo wa kulia cha Benjamin Netanyahu Likud, kinapambana na chama cha mrengo wa kati Blue and White kinachoongozwa na Jenerali mstaafu, Benny Gantz.

Tangu uchaguzi wa kwanza wa Israeli kufanyika mwaka 1949, hakuna chama hata kimoja cha kisiasa kilichofanikiwa kupata wingi wa viti katika Baraza la Wawakilishi, hali ambayo wakati mwingine imekuwa ikisababisha mazungumzo ya kutaka kuundwa kwa serikali ya umoja.

Kulingana na uchunguzi wa gazeti la kila siku la Yedioth Ahronoth, lilieleza kuwa chama cha Benny Gantz kinatarajia kupata viti 30 katika Baraza la Wawakilishi, huku chama cha Likud kikipata 26.

Lakini vyama vya muungano wa mrengo wa kulia vinavyomuunga mkono Benjamin Netanyahu vinatarajia kupata viti 63 kati ya 120 katika Bunge hilo, idadi ambayo ni ndogo lakini inatosha kupitisha sheria.

Ili kushiriki katika Bunge, chama kinapaswa kupata angalau asilimia 3.25 ya kura, ambayo ni sawa na viti vinne bungeni.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa saa 1:00 asubuhi kwa saa za Israeli na zoezi la kupiga kura lilimalizika saa 12:00 jioni.

Baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi, Rais Reuven Rivlin atawasiliana na viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa na kumchagua anayeona ana uwezo wa kuunda serikali, na siyo lazima kiongozi wa chama ambacho kimeshinda viti vingi.

Kiongozi atayechaguliwa atakuwa na siku 42 kutangaza serikali, vinginevyo Rais ataomba mwingine kuchukuwa nafasi hiyo. **RFI**

## Teknolojia mpya kunasa chatu yagunduliwa

**WASHINGTON,** Marekani

WAFANYAKAZI wa hifadhi ya wanyama ya Big Cypress iliyopo Frorida nchini Marekani, imemnasa chatu mkubwa mwenye urefu wa futi 17 kwa kutumia teknolojia mpya ya kuwanasa viumbe wavamizi.

Nyoka huyo jike ndiye mkubwa zaidi kuwahi kunaswa kwenye hifadhi ya Big Cypress, alikuwa na uzito wa kilo 63.5, na mimba ya mayai 73.

Chatu ambao ni wavamizi kwenye eneo hilo, wanatishia sana maisha ya viumbe wa asili wa Jimbo la Florida.

Watafiti katika hifadhi hiyo walivategeshea vifaa maalumu madume ya chatu ili kuwatafuta majike yanayopandwa na kukaribia kutaga.

Pamoja na kuwaondoa nyoka wavamizi, hifadhi hiyo inatumia matokeo ya utafiti zake ili kustadi tabia za nyoka na kutengeneza njia mpya za kukabiliana nao.

Chatu wanachukuliwa kama viumbe wavamizi jimboni Florida tangu walipoonekana kwa mara ya kwanza katika viunga vya Everglades miaka ya 1980.

Lakini chatu wengi katika jimbo hilo walitoroka kwenye vituo vya utafiti vya uzalishaji baada ya kimbunga Andrew cha mwaka 1992. **BBC**

## UN yataka mapigano Libya yakomeshwe

**TRIPOLI,** Libya

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, jana, alitoa wito wa kusitishwa mara moja kwa operesheni za kijeshi nchini Libya baada ya mapigano kusababisha maelfu ya watu kukimbia makazi yao, pamoja na uwanja wa ndege katika mji mkuu Tripoli kushambuliwa.

Uwanja wa Ndege wa Tripoli ambao umekuwa ukifanya kazi ulishambuliwa na ndege za kivita za vikosi vya Marshal Khalifa Haftar, ambavyo vinaendesha mashambulizi dhidi ya mji mkuu wa Libya.

Tangu Alhamisi ya wiki iliyopita, vikosi vya Marshal Khalifa Haftar vinavyodhibiti mashariki mwa Libya vinapigana na majeshi ya serikali ya umoja wa kitaifa na kusababisha mamia ya wananchi kupoteza maisha na zaidi ya 3,400 kuyatoroka makazi yao.

Guterres alitoa wito huo wa kusitishwa mapigano pamoja na kuzitaka pande mbili zinazovutana kuzuwia mzozo kuwa mkubwa zaidi.

Msemaji wa Guterres, Stephane Durarric, alisema kwamba hakuna suluhisho la kijeshi katika mzozo wa Libya na kutoa wito kwa pande zote kujihusisha haraka na majadiliano ya kufikia suluhisho la kisiasa.

Kamanda Khalifa Haftar, Mkuu wa Jeshi alilolitengeneza binafsi la Libyan National Army LNA, aliamuru majeshi yake kuuteka mji wa Tripoli kutoka kwa serikali inayoungwa mkono kimataifa inayoongozwa na Fayez Serraj. **DW**

# Mshtakiwa dawa za kulevya aachiwa huru

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Kihemba Mtamamchungu, ameachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baada ya kuonekana hana hatia dhidi ya tuhuma za kusafirisha gramu 81.8 za dawa za kulevya aina ya Heroin.

Aliachiwa huru katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Kasonde Maira baada ya ushahidi wa Jamhuri kuwa wa shaka dhidi ya mshtakiwa.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu alisema upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi sita na vielelezo mbalimbali na upande wa utetezi ukiwa na mashahidi wawili. Maira alisema miongoni mwa mashahidi hao ni ofisa wa polisi kitengo cha dawa za kulevya aliyetajwa kwa jina la Wamba ambaye ndiye pekee anayedaiwa kukamata dawa hizo za kulevya wakati wa upekuzi katika nyumba ya mshtakiwa.

Hata hivyo, alisema ushahidi wa upande wa utetezi ulionyesha shaka kuhusu upatikanaji wa dawa hizo kupitia kwa mashahidi wake akiwamo mwenyekiti wa serikali ya mtaa aliokuwa akiishi mshtakiwa, Sharifa Mrisho.

Hakimu alisema shahidi huyo huru, aliieleza mahakama kwamba alipofika nyumbani kwa mshtakiwa alikuta tayari maofisa wa polisi kitengo cha dawa za kulevya wameshaingia ndani kufanya upekuzi, huku mshtakiwa akiwa nje amefungwa pingu.

"Nadhani ushahidi wa upande wa mashtaka unahitaji nyongeza. Ushahidi wa upande wa utetezi bado unatikisa ushahidi wa upande wa mashtaka. Katika kesi hii sikuelewa kwa nini upande wa mashtaka haukuleta mashahidi muhimu kama Hossen Salum na Sharifa ambao walikuwa viongozi wa serikali ya mtaa," alisema Hakimu.

Alisema ushahidi huo unaonyesha kwamba bado kuna shaka ya kuwapo uwezekano wa dawa hizo za kulevya kupandikizwa

Alisema kutokana na hali hiyo, mahakama inamwona mshtakiwa hana hatia na inamwachia huru.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

# AUDITED RESULTS

## FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

The year of 2018 saw continued growth in the local cement industry, with the market increasing at a higher rate than in previous years. Competition was again fierce, and yet despite the cement over capacity in the local market, TPCPLC once again strengthened its market leadership.

The efforts made throughout the year on the operational side to increase clinker production, whilst overcoming technical challenges, combined with the focus on producing and selling high quality products, whilst maintaining strong customer relationships and service excellence, has allowed TPCPLC to report an improved full year result.

Total volumes sold in 2018 increased by 9% on 2017, and with revenue also increasing by 28%, this resulted in an operating profit of TZS 80.1Bn being recorded, a 28% increase on the previous full year result.

| INCOME STATEMENT | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 346,863,384 | 273,157,459 |
| Cost of sales | (223,923,847) | (189,852,039) |
| **Gross profit** | **124,939,537** | **83,305,420** |
| Selling and administrative expenses | (27,221,412) | (25,029,949) |
| Other operating income | 148,927 | 22,463,707 |
| Depreciation and amortization | (17,806,015) | (18,066,388) |
| **Operating profit** | **80,061,037** | **62,672,790** |
| Financial items | 1,683,745 | 2,925,035 |
| **Profit before tax** | **81,744,782** | **65,597,825** |
| Taxes on income | (24,878,688) | (30,001,432) |
| **Net profit for the period** | **56,866,094** | **35,596,393** |
| Other comprehensive income, net of tax | (403,822) | (1,362,319) |
| **Total comprehensive income** | **56,462,272** | **34,234,074** |
| Number of shares | 179,923,100 | 179,923,100 |

| BALANCE SHEET | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| **Assets** | | |
| Intangible fixed assets | 1,304,535 | 2,635,382 |
| Tangible fixed assets | 140,948,038 | 150,539,113 |
| Non-current financial assets | 7,513,661 | 16,749,420 |
| **Non current assets** | **149,766,234** | **169,923,915** |
| Inventories | 55,104,226 | 41,711,116 |
| Trade and other receivables | 44,712,022 | 37,662,988 |
| Other current financial assets | 7,191,052 | 4,114,476 |
| Cash and cash equivalents | 65,987,258 | 34,739,002 |
| **Currents assets** | **172,994,558** | **118,227,582** |
| **Total assets** | **322,760,792** | **288,151,497** |
| **Equity and Liabilities** | | |
| **Equity** | **224,935,758** | **186,465,797** |
| Long term provisions | 8,205,223 | 6,867,069 |
| Provision for deferred taxes | 21,035,003 | 25,220,943 |
| **Non current liabilities** | **29,240,226** | **32,088,012** |
| Dividend payable | 3,850,962 | 15,519,795 |
| Trade and other payables | 61,158,088 | 45,643,564 |
| Taxes payables | 3,575,758 | 8,434,329 |
| **Current liabilities** | **68,584,808** | **69,597,688** |
| **Total equity and liabilities** | **322,760,792** | **288,151,497** |

**Prospects**
The company continues to face increasing competition, but TPCPLC will continue to work to maintain its market leadership position.

**Dividend**
The Board proposes a dividend for 2018 of TZS 290 per share, same as for the previous year.

The Register of Members will close on 8 May 2019, and the last day of trading cum dividend will be 3 May 2019. The dividend will be paid on or about 30 June 2019.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support during the year. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders in the future.

These financial statements were approved by the Board of Directors on 8 April 2019

**BY ORDER OF THE BOARD**

**Alfonso Velez**
**For Chairman of the Board**
**10 April 2019**

| STATEMENT OF CASH FLOW | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| Profit before tax | 81,744,782 | 65,597,825 |
| Depreciation and amortisation | 17,806,015 | 18,066,388 |
| Interest received | 1,350,833 | 867,496 |
| Income tax paid | (31,997,950) | (20,645,698) |
| Elimination of non cash items | (1,354,655) | (25,539,694) |
| Change in working capital | (4,522,481) | 24,333,732 |
| **Cash flow from operating activities** | **63,026,544** | **62,680,051** |
| **Cash flow from investing activities** | **(2,117,144)** | **(2,934,268)** |
| Dividend paid | (29,661,144) | (48,182,450) |
| **Change in cash and cash equivalents** | **31,248,256** | **11,563,333** |
| Cash and cash equivalent 01.01 | 34,739,002 | 23,175,669 |
| Change in cash | 31,248,256 | 11,563,333 |
| **Cash and cash equivalent 31.12** | **65,987,258** | **34,739,002** |

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O. Box 1950**
**Dar es Salaam**
**Tanzania.**
**Tel +255 746 810930 Fax: +255 746 810931**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**

215168302


# 'Uboreshaji afya kwa wote utasaidia kufikia maendeleo endelevu'

**Na Mashaka Mgeta**

SERIKALI imeshauriwa kuwekeza katika ongezeko la bajeti ya afya ili kufanikisha jitihada za kufikia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na ongezeko la watu wanaopata huduma za afya nchini.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Afya (HDT), Dk. Peter Bujari, kwenye taarifa yake katika maadhimisho ya Siku ya Afya kwa wote yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Dk. Bujari alisema serikali inastahili pongezi kwa kuonyesha nia njema kwa kuongeza bajeti ya wizara ya afya kutoka Sh. trilioni 1.99 kwa mwaka 2016/17 hadi Sh. trilioni 2.2 mwaka 2017/18.

Alisema kwa mujibu wa taarifa zilizopo, serikali ipo katika hatua nzuri za kufanikisha upatikanaji huduma bora za afya kufikia ngazi ya kaya na jitihada mbalimbali zinazofanyika kwenye maeneo tofauti nchini.

Hata hivyo, alisema ongezeko la kiasi hicho kwenye bajeti ni sawa na nusu ya mahitaji ya sekta ya afya kwa mujibu wa makadirio ya mkakati wa afya wa 2015-2020 na kwamba fedha zilizotolewa zilikuwa ni pungufu ya bajeti iliyotengwa.

"Mfano mwaka 2017/2018 makadirio ya wizara yalikuwa ni Sh. trilioni 4.35, wakati bajeti ilikuwa ni Sh. trilioni 2.2," alisema Dk. Bujari kupitia taarifa iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Programu wa HDT, Salvator Hokororo.

"Matokeo yake nchi haijafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) hususani sehemu ya 3.8.1 inayohusu kuongeza huduma muhimu za afya muhimu," alisema na kuongeza kuwa wakati Tanzania ikiwa na watu 36 kati ya 100 wanaopata huduma za afya, Kenya ni 57, Rwanda wakiwa ni 53 na Uganda ni 44.

Pia Dk. Bujari alisema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoshiriki harakati za kimataifa kuhakikisha kila raia anayehitaji huduma za afya, anapata bila kizuizi, hivyo ipo haja kwa viongozi wa ngazi zote kujitolea na kuwekeza kwenye 'afya kwa wote'.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
09/04/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMISI tarehe 11/04/2019** kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MTO WA MBU kuelekea ARUSHA, gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/T916DCG.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 17.50
   Upana –mita 2.90
   Kimo – mita 4.60
3. Njia itakayotumika **MTO WA MBU hadi ARUSHA kupitia MAKUYUNI,** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215167902

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
09/04/2019


## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe **13/04/2019** kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **CHEKERENI** kuelekea ARUSHA, gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/T916DCG.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 17.50
   Upana –mita 3.28
   Kimo – mita 4.60
3. **Njia itakayotumika CHEKERENI hadi ARUSHA kupitia MACHAME GATE**, gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215167702

## KUPOTEA KWA CHETI



**Kennedy Wilfred Mushi a**natangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S.4545/0066** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Mbwawa .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KMR/RB/3940/2019**

115166702

## KUPOTEA KWA CHETI




**Saudani Abdala** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0212/0109** kilichotolewa na Baraza la Taifa la mitihani mwaka 1996 katika shule ya Sekondari ya wasichana Machame .

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:
MAG/PS/BI/21/VOL.IV/300**

115166402

## KUPOTEA KWA CHETI



**Anaitwa STEPHEN G.DYUMYEKO** amepotelewa na cheti cha elimu ya SECONDARI alichosomea ktk shule ya KIGURUNYEMBE SECONDARI.

**Alichomaliza mwaka 1984.Chenye index namba S.359/153.**

**Kw yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi,Taarifa ya polisi; MOR/RB/4325/2019.**

215167202


Kwa Habari Motomoto usikose

Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi No. 23/2019**

**Ombi la SOPHIA DAUDI KIRITA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu AMON MWAKAGUGU**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 9/4/2019

115166502

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi No.22/2019**

**Ombi la SOPHIA DAUDI kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi Marehemu SHIDA AMON MWAKAGUGU**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 9/4/2019

115166602


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# MAN UNITED VS BARCELONA

## Ni mechi ya kisasi Ligi ya Mabingwa, rekodi mbovu ugenini shida kwa kina Messi leo...

**MANCHSTER,** England

BILA shaka kwa sasa Barcelona ni klabu yenye maisha ya furaha zaidi barani Ulaya.

Wanaongoza Ligi ya Hispania, maarufu kama La Liga, kwa tofauti ya pointi 11. Pia wameshatinga fainali ya Kombe la Kombe la Mfalme ['Copa de Rey'].

Kwa vyovyote vile, miamba hiyo ya Hispania chini ya kocha, Ernesto Valverde, watakuwa na kila sababu ya kujiamini pale watakapoingia dimbani kucheza na Manchester United leo Jumatano katika mchezo wa raundi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Ushindi wao wa mwisho ulikuwa dhidi ya Atletico Madrid Jumamosi iliyopita, ambapo hadi dakika ya 84 ilikuwa hakuna bao.

Zikiwa zimesalia dakika tano tu mchezo kumalizika, Luis Suarez, alipiga kombora moja lililomshinda mlinda mlango wa Atletico, Jan Oblak ambaye alikuwa nyota kwa upande wa timu yake kwa kuokoa michomo mingi ya Barca.

Zahama tena ikarudi baada ya dakika moja tu kwa Lionel Messi kupachika bao la pili baada ya kuwahadaa walinzi na mlinda mlango wa Atletico.

Lionel Messi ameshapachika mabao 33 ya La Liga hadi sasa, huku akikaribia kushinda Kiatu cha Dhahabu kwa msimu wa tatu mfululizo.

Matokeo dhidi ya Atletico ilikuwa ni mara ya pili kwa Suarez na Messi kuamua matokeo ya mwisho ya klabu yao ndani ya dakika za lala salama.

Jumatano wiki iliyopita, Barcelona walitoka sare ya mabao 4-4 dhidi ya Villarreal. Hadi dakika ya 89 Villarreal walikuwa wanaongoza kwa mabao 4-2.

**Zikiwa zimesalia dakika tano tu mchezo kumalizika, Luis Suarez, alipiga kombora moja lililomshinda mlinda mlango wa Atletico, Jan Oblak ambaye alikuwa nyota kwa upande wa timu yake kwa kuokoa michomo mingi ya Barca.**




Ilipotimu dakika ya 90, Suarez akaandika bao la tatu na ndani ya dakika mbili za majeruhi, Messi akaiandikia Barcelona goli la nne na kuondoa aibu ya kufungwa na timu iliyopo kwenye nafasi tatu za mkiani.

Habari mbaya zaidi kwa Manchester United ni kuwa, Suarez na Messi wamekuwa wakifumania nyavu kwa kasi zaidi msimu huu.

Wawili hao wamefunga mabao 14 katika mechi sita zilizopita (mabao 10 kwa Messi, Suarez manne), na kwa msimu huu hadi sasa Messi kashafunga mabao 43 katika michezo 40. Pia ametoa pasi za mwisho 17 zilizozaa mabao.

Wachambuzi wengi wanaamini huu ndiyo unaweza ukawa msimu bora zaidi kwa Messi, na ni wale ambao hawajamwangalia akicheza kwa siku za hivi karibuni tu ndio ambao wataendelea kudhania kuwa kiwango chake kimeporomoka.

Messi na Suarez wanafanya kazi vizuri pamoja wakiwa uwanjani, lakini si kwamba wao ndio watu hatari pekee kwenye kikosi cha Barca.

Mchezaji ambaye anashirikiana kwa karibu zaidi na Messi ni beki wa pembeni Jordi Alba, ambaye amekuwa bingwa wa kumpenyezea Messi mipira kwenye eneo la hatari.

Swali kubwa zaidi ni nani ataungana na wawili hao kwenye safu ya ushambuliaji dhidi ya Manchester United. Jumamosi waliungana na winga wa zamani wa Liverpool, Philippe Coutinho, ambaye mashambulizi yake yote yalinaswa na kipa wa Atletico.

Hata hivyo, Coutinho hajakuwa na msimu mzuri hadi sasa, na kuna uwezekano mkubwa nafasi yake ikachukuliwa na Ousmane Dembele iwapo atakuwa ameimarika afya yake.

Gerard Pique ameendelea kuwa na msimu mzuri baada ya kubwaga manyanga kuchezea timu ya Taifa ya Hispania.

Kocha Valverde pia ana 'uti wa mgongo' imara unaoongozwa na kipa Marc-Andre ter Stegen, beki wa kati kisiki Piquena kiungo Arthur Melo.

Arthur ndiye mchezaji ambaye mashabiki wengi wa Man United hawamfahamu, ni raia wa Brazil aliyejiunga na miamba hiyo ya Hispania akitokea klabu ya Gremio mwanzoni mwa msimu huu.

Lakini hata kama hujawahi kumuona kabla, anaweza asiwe mgeni machoni mwao maana aina yake ya uchezaji ni kama nguli Xavi.

Japo ni jambo gumu kumlinganisha mtu yeyote na Xavi. Arthur amekuwa akicheza vizuri kwenye kiungo cha kati na kuwa na wastani wa takwimu mzuri kama Xavi.

Katika mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Valencia mwanzoni mwa msimu, kiungo huyo mwenye miaka 22, alifikia rekodi ya kupiga pasi nyingi zaidi (135) kwenye mchezo wa ugenini wa La Liga. Rekodi kama hiyo iliwekwa mwaka 2012 na Xavi.

Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, aliendа kushuhudia mchezo kati ya Barcelona na Atletico mwishoni mwa wiki.

Licha ya kuwa na mafanikio mazuri nyumbani, kwa sasa Ligi ya Mabingwa Ulaya ndio kipaumbele namba moja kwa klabu hiyo.

Miamba hiyo imekuwa ikiyaaga mashindano hayo katika hatua ya robo fainali kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita.

Katika kipindi chote hicho, habari mbaya zaidi kwa Barcelona ilikuwa ni wapinzani wao wa jadi katika soka la Hispania, ndiyo ilikuwa ikinyanyua ndoo mara kwa mara na msimu uliopita ilitwaa kwa mara ya tatu mfululizo.

Tayari Messi ameshawaahidi mashabiki wa Barcelona mwanzoni mwa msimu huu kuwa: "Tunaahidi kuwa tutafanya kila tuliwezalo ili kulirudisha kombe lile zuri hapa Camp Nou."

Lakini Man United hawatakiwi kukata tamaa kabisa, sababu Barcelona wanafungika.

### UDHAIFU WA BARCA

Udhaifu mkubwa wa Barcelona ni safu yake ya ulinzi, ambayo kwa mara kadhaa imedhihirisha kuwa haiwezi kuzuia mashambulizi ya kushtukiza.

Hilo lilionekana wazi kwenye sare yao ya 4-4 na Villarreal ambao wanapambana ili kujinusuru na kushuka daraja.

Barca pia kwa miaka ya hivi karibuni hawana rekodi nzuri katika mechi za ugenini katika hatua ya mtoano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barca hawajashinda mechi yoyote kwenye hatua ya mtoano tangu walipoifunga Arsenal mabao 2-0 Februari mwaka 2016 - na kwenye kipindi hicho wamepokea vipigo vizito ugenini kutoka kwa Atletico (2-0), Paris St Germain (4-0), Juventus (3-0) na AS Roma (3-0).

Hivyo, kuna kila sababu kwa United kuamini kuwa wanaweza kuiadhibu Barcelona inayoongozwa kikamilifu na Messi, lakini haitakuwa kazi rahisi.

## HABARI MICHEZO




# ZAHA AIKATALIA UNITED

**LONDON,** England

WILFRIED Zaha amesema hafikiri lolote zaidi ya Crystal Palace wakati huu tetesi zikiendelea kumhusisha na kuondoka klabuni hapo.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 26, yupo katika kiwango cha juu msimu huu, akiifungia klabu hiyo ya kusini mwa London mabao nane kwenye mechi 29 za Ligi Kuu alizocheza.

Tetesi kwamba atajiunga kwa mara nyingine na Manchester United zimeibuka katika kipindi cha hivi karibuni, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast amesisitiza kuwa halengi kuondoka hapo Selhurst Park.

"Mustakabali wangu wa baadaye upo Palace," alinukuliwa na Sky Sports akisema.

"Nipo Palace, sifikiri kuhusu lolote[lile].

"Ninacheza tu soka langu na nitaona mustakabali wangu wa baadaye utakavyokuwa kwangu."

Zaha alikuwa usajili wa mwisho wa Alex Ferguson katika kikosi cha Manchester United wakati alipojiunga na miamba hiyo ya Old Trafford mwaka 2013, na akarudi klabu yake hiyo ya utotoni, Palace mwaka 2015, mwanzoni ikiwa ni kwa mkopo, kabla ya kujiunga kwa uhamisho wa kudumu.

# Emery hana uhakika na Koscielny, Xhaka

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, ametoa taarifa ya majeruhi ya Laurent Koscielny na Granit Xhaka, wakati wakijiandaa na mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Kombe la Ligi ya Europa dhidi Napoli kesho, Alhamisi.

'Washika Bunduki' hao wanakwenda kwenye mchezo huo wakiwa wametoka kufungwa na Everton katika mechi ya Ligi Kuu ya England Jumapili, ambapo Sokratis Papastathopoulos alionyeshwa kadi ya njano ya 10 kwa msimu huu na kufungiwa mechi mbili za ligi.

Na sasa kurudi kwa beki wa kati Laurent Koscielny, ambaye alikuwa nje ya dimba tangu kwenye mchezo wa hatua ya mtoano wa timu 16-bora dhidi ya Rennes.

Hata hivyo, Emery ameshindwa kutabiri mchezo wake dhidi ya Napoli, akibainisha kwamba hakutarajia kipigo kutoka kwa Everton.

"Sijui. Pengine Laurent angeweza kurudi na kucheza leo [juzi], lakini haiwezekani. Nataka kuwa na mwelekeo chanya kuelekea mchezo wa Alhamisi."

Pia alimzungumzia kiungo wa kimataifa wa Uswisi, Xhaka, ambaye amekuwa nje ya dimba tangu katika mchezo dhidi ya Rennes na Emery ameelezea: "Xhaka naye sijui kama atakuwapo dimbani kwenye mchezo wa Alhamisi."

Wachezaji, Rob Holding, Hector Bellerin na Danny Welbeck bado wataendelea kuwa nje kutokana na majeraha, lakini Konstantinos Mavropanos, ambaye alikuwa anasumbuliwa na nyonga alirudi kwenye mchezo wa kirafiki Aprili mwaka huu na kuna uwezekano akawa fiti kwa mchezo wa Alhamisi.




# Van Dijk ampigia kura ya mchezaji bora Raheem




**MANCHESTER,** England

BEKI wa Liverpool, Virgil van Dijk amempigia kura mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling, kuwa mchezaji bora wa mwaka wa England, PFA.

Van Dijk amekuwa nguzo kuu ya mafanikio ya Liverpool kwenye safu ya ulinzi msimu huu kwa kuwa na rekodi nzuri ya kushinda na pia wakiwa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya wapinzani wao, Manchester City.

Wakati huo huo, Sterling mwenye umri wa miaka 24 amefunga mabao 15 kwa City hadi sasa.

"Nimefanya kile nilichofikiria ninastahili," alisema Van Dijk.

"Amekuwa na msimu wa kuvutia. Ningeweza kumpigia kura Bernardo Silva pia na wachezaji wengine wa City.

"Lakini nimekuwa tu mkweli. Nafikiri ameimarika zaidi kama mchezaji. Tutaona kama atashinda."

Liverpool kwa sasa wanaongoza msimamo wa ligi kwa pointi mbili zaidi dhidi ya Manchester City, ikiwa imecheza mechi moja zaidi, wakati kikosi hicho cha Jurgen Klopp kikipigania kushinda taji hilo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

"Nafikiri timu nyingi kwenye ligi zingeweza kuwa kwenye nafasi yetu kwa sasa. Tupo kwenye nafasi nzuri," ameongeza mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, Van Dijk ambaye alijiunga na klabu hiyo ya Anfield kwa pauni milioni 75 katika usajili wa Januari mwaka jana.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SARRI: NI VIGUMU SANA KUMBAKISHA HAZARD

●●● Pauni milioni 100 ni rahisi sana katika soko la sasa, tutajaribu kumshawishi ila tunapaswa kuheshimu...

**LONDON,** England

MAURIZIO Sarri amekewa wazi kuwa dau la pauni milioni 100 linalotajwa kwa Eden Hazard ni rahisi sana, lakini akakiri kwamba hana nguvu ya kumbakisha Chelsea.

**Hazard juzi aliing'arisha Chelsea kwa mabao yake mawili wakati wakishinda 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya West Ham, ushindi uliyoipeleka hadi nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo, saa chache baada ya kuripotiwa na Sky Sports News kwamba Real Madrid imezidi kujiamini kuwa itamsajili Mbelgiji huyo majira ya joto.**

Lakini sasa Sarri amesema kumbakisha Hazard itakuwa ni vigumu, ila anaamini sokoni kwa sasa mshambuliaji huyo anagharimu zaidi ya pauni milioni 100.

Aliiambia Sky Sports: "[pauni milioni 100] ni rahisi sana, katika soko la sasa ni rahisi sana. Tuliona kila bei nadhani katika soko la dirisha la usajili lililopita. Hivyo nadhani ni vigumu sana kumbadili Hazard na mchezaji mwingine."

Alipoulizwa nguvu gani alizonazo katika kumbakisha Hazard klabuni hapo, Sarri alijibu: "Siwezi kufanya lolote [kumbakisha yeye], kwa sababu klabu imekubaliana naye, lakini kama Eden anataka kupata uzoefu mwingine, ni vigumu sana kumbakisha, nadhani.

"[Tutajaribu kumshawishi] kwamba tunajaribu kujizatiti, kuwa moja ya timu bora England, pamoja na Ulaya, lakini nadhani ninapaswa kuheshimu uamuzi wake."

Aidha, akizungumza na Sky Sports baada ya mechi, Hazard yeye mwenyewe aliulizwa kama mashabiki wa West Ham kuimba "Yupo mbali Madrid" ilikuwa kweli, lakini aligeukia kuhusu kubaki.

Hazard ambaye ameshafunga mabao 19, kwenye mashindano yote msimu huu, alisisitiza kuwaambia kuwa 'yupo mbali Madrid' ni wongo, lakini akakiri mustakabali wake wa baadaye utaamuliwa mwishoni mwa msimu.

"Ni waongo. Ninaelekeza akili yangu Chelsea hadi mwishoni mwa msimu. Ninachotaka tu ni kumaliza nne-bora na kutwaa ubingwa wa Europa League. Bado tuna mengi ya kufanya na kisha tutaona.

"Kwa sasa tupo katika kasi nzuri. Tumeshinda mechi tatu mfululizo na kimawazo ni vizuri kuendelea kama hivyo. Nne-bora ni lengo letu, kutwaa Europa League ni changamoto kwetu, hivyo tunapaswa kuendelea kupigania vyote vilivyopo mbele. Tunaweza kulifanya hilo."

## ZISIKUPITE

### UTD YAMWANDALIA DAU RICE

MANCHESTER United inaandaa pauni milioni 50 majira ya joto kwa ajili ya kutoa ofa kwa kiungo wa West Ham, Declan Rice. ***(Irish Independent)***

### HAKIJAELEWEKA TORONTO

KLABU ya Toronto FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (Major League Soccer), hatafanikisha dili la kumsajili Arjen Robben, 35, baada ya kusitisha mazungumzo na winga huyo Mholanzi, ambaye anaondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu. ***(ESPN)***

### POGBA AICHANGANYA UNITED

KOCHA msaidizi wa Manchester United, Mike Phelan, amesema kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, bado ni lulu na kumtaka abaki Old Trafford. ***(Telegraph)***

### TAGLIAFICO AIITA ARSENAL

BEKI wa kushoto wa Ajax, Nicolas Tagliafico, amesema majira haya ya joto yanaweza kuwa "muda sahihi" wa kutua klabu za England. Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 26 anawindwa na Arsenal. ***(Mirror)***

### ADAMS AWINDWA EVERTON

EVERTON inaandaa ofa kwa mshambuliaji wa Birmingham City, Muingereza Che Adams, 22. ***(Football Insider)***

### BARCA YAFUNGUKA KUZUIWA

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amesema klabu hiyo ilitaka kumsajili Paul Pogba, lakini haikuweza kushindana na Manchester United wakati alipoondoka Juventus mwaka 2016. ***(ESPN)***

### WEST HAM KUMTEMA CARROLL

WEST Ham haitampa ofa ya mkataba mpya Andy Carroll, 30, mwishoni mwa msimu. Straika huyo wa England alipatwa na majeraha ya kifundo cha mguu yanayomweka nje ya uwanja hadi mwishoni mwa msimu. ***(Mail)***

### HAZARD JR KUIKATAA LIVER

LIVERPOOL imewasilisha ofa kubwa kwa Thorgan Hazard, lakini kiungo huyo wa Borussia Monchengladbach anataka kujiunga na Borussia Dortmund, ambayo inamtaka kwenda kuziba pengo la Mmarekani Christian Pulisic, 20, aliyejiunga na Chelsea. ***(Sun)***

### AWATULIZA MURPHY, GAYLE

KOCHA wa Newcastle United, Rafael Benitez, amesema straika Dwight Gayle, 28, na winga Jacob Murphy, 24, ambao wote wanacheza kwa mkopo West Brom, bado wanaweza kuwa na mustakabali mzuri katika klabu yake, licha ya kuhusishwa na mpango wa kubadilishana na mshambuliaji wa West Bromwich Albion, Salomon Rondon, ambaye anacheza kwa mkopo hapo St James' Park. ***(Chronicle)***

### ANOGEWA CSKA MOSCOW

WAKALA wa straika wa Everton, Nikola Vlasic, 21, amesema nyota huyo wa kimataifa wa Croatia anataka kubaki CSKA Moscow kwa uhamisho wa kudumu mara mkataba wake wa mkopo wa muda mrefu utakapomalizika mwishoni mwa msimu wa majira ya joto. ***(Championat, via Liverpool Echo)***

# Lyon: Bado tupo sana Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa African Lyon, Salvatory Edward, amesema kuwa timu yake haijakata tamaa na inaamini inaweza kubakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo sasa inaelekea ukingoni.

Kauli ya kocha huyo imekuja baada ya kuchapwa mabao 2-0 na Yanga katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Salvatory alisema kuwa mechi zao sita zilizobaki msimu huu zinaweza kuwabakisha kwenye ligi hiyo ya juu nchini, licha ya wadau wengi kuamini nafasi ya wao kubakia imeshapotea.

"Hatujakata tamaa, ligi bado haijamalizika, kama ilivyo kwa bingwa bado hajajulikana, na vile vile timu zitakazoshuka daraja pia hazijajulikana, mpaka siku ya mwisho," alisema nyota huyo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars.

Aliongeza kuwa bado ataendelea kurekebisha makosa anayoyabaini ili waweze kufanya vizuri katika mechi zao zinazofuata.

"Tutapambana mpaka mechi ya mwisho, TFF ndio itatangaza rasmi timu zitakazoshuka na si mtu mwingine, huwezi kujua lolote linaweza kutokea hapa katikati, sisi bado tupo sana kwenye Ligi Kuu," alisisitiza kocha huyo.

African Lyon yenye pointi 22 ndiyo inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaongozwa na Yanga yenye pointi 71 ikifuatiwa na Azam FC wenye pointi 63.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 30 | 22 | 5 | 3 | 48 | 20 | 71 |
| 2. Azam | 30 | 18 | 9 | 3 | 48 | 18 | 63 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 5. Mtibwa Sugar | 31 | 13 | 6 | 12 | 32 | 24 | 45 |
| 6. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 7. Kinondoni MC | 31 | 9 | 14 | 8 | 32 | 23 | 41 |
| 8. Coastal Union | 32 | 9 | 14 | 9 | 28 | 31 | 41 |
| 9. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 10. Singida United | 32 | 10 | 9 | 13 | 24 | 32 | 39 |
| 11. Ndanda | 30 | 10 | 9 | 11 | 20 | 29 | 39 |
| 12. Stand Utd | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 13. Mbeya City | 30 | 10 | 7 | 13 | 30 | 33 | 37 |
| 14. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 30 | 8 | 12 | 10 | 24 | 29 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# SERENGETI BOYS MORALI IPO JUU, CAMEROON, MOROCCO WAWASILI

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wenyeji Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17, Serengeti Boys, walirejea nchini juzi usiku, yosso kutoka Cameroon na Morocco wamewasili tayari kusubiri kuanza kwa fainali za Afrika (Afcon U-17) ambazo zitaanza kurindima jijini Dar es Salaam kuanzia Jumapili.

Cameroon ndio ilikuwa timu ya kwanza kuwasili nchini, ikifuatiwa na Morocco ambazo zote ziko katika Kundi B na jana jioni zilitarajiwa pia kuwasili timu nyingine tatu.

Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Oscar Mirambo, aliliambia gazeti hili kuwa wamerejea salama na vijana wana ari kubwa ya kutekeleza yale waliyofundishwa.

**Mirambo alisema anaamini watapambana kwa lengo la kupata ushindi katika mechi zote watakazocheza ili waweze kutimiza malengo yao ya kucheza fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Oktoba mwaka huu nchini Brazil.**

Kocha huyo alisema katika kujiandaa na mashindano hayo, Serengeti Boys imecheza mechi za kirafiki 21 na timu mbalimbali katika Bara la Afrika, Ulaya na klabu za hapa nchini.

"Tumerejea na sasa tuko katika vipimo, ni utaratibu wa CAF (Shirikisho la Soka Afrika), ila napenda kusema kuwa kila kitu kwa upande wa timu yetu kiko sawa sawa na tunachosubiri ni kupambana uwanjani," alisema Mirambo.

Serengeti Boys itafungua pazia la mashindano hayo kwa kuikaribisha Nigeria katika mchezo wa kwanza utakaochezwa kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na baadaye Angola watachuana na Uganda kuanzia saa 1:00 usiku.




Msemaji wa Bikosports, Geoffrey Lea (kushoto), akimkabidhi tuzo ya Mchezaji Bora wa mwezi Machi, mshambuliaji mahiri wa Klabu ya Simba, John Bocco, baada ya wiki iliyopita kutangazwa kushinda tuzo hiyo ambayo mchakato wake unadhaminiwa na Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya Michezoni ya Bikosports. **NA MPIGAPICHA WETU**




# *Chama aiona Mazembe 'ikifia' DR Congo*

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO 'muuaji wa dakika za mwisho' wa Simba, Mzambia Clatous Chama, amefunguka kuwa licha ya kushindwa kufurukuta dhidi ya TP Mazembe katika mechi ya mkondo wa kwanza Uwanja wa Taifa, anatumai akipata nafasi Jumamosi kwa kushirikiana na wenzake wapinzani wao 'watafia' kwao DR Congo.

Katika michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa, Chama amekuwa msaada mkubwa kwa Simba, kwani ameshaifungia mabao matano ikiwa ni pamoja na bao muhimu dhidi ya Nkana FC lililoipeleka timu yake hatua ya makundi na la pili dhidi ya AS Vita lililowahakikishia kutinga hatua ya robo fainali.

Simba ilishindwa kuibuka na ushindi Jumamosi katika mechi hiyo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kulazimishwa sare tasa Taifa, huku nahodha John Bocco akikosa penalti.

Na licha ya Chama kuanza katika mechi hiyo, hakuwa katika ubora wake na kusababisha kocha Patrick Aussems kumtoa na kumuingiza Okwi aliyeanzia benchi Jumamosi.

Hata hivyo, juzi Chama alieleza kutofurahishwa na matokeo hayo, lakini akaweka wazi kuwa yeye na wenzake wanaahidi kupambana katika mechi ya DR Congo hadi kupata ushindi.

"Hakika hatukutarajia kuona mechi hii ikimalizika kwa matokeo kama haya, ila bado Simba ina nafasi na tutapambana na kufanya tulichoshindwa kukifanya hapa nyumbani," alisema Chama mwenye umri wa miaka 27 kwa sasa.

Simba ambayo inahitaji sare yoyote ya mabao ama ushindi ili kutinga nusu fainali ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika, inatarajia kusafiri kwa ndege maalum ya kukodi kuifuata TP Mazembe Ijumaa tayari kwa mechi hiyo itakayopigwa Jumamosi.



Emery hana uhakika na Koscielny, Xhaka UKURASA 29



Cristiano Ronaldo tayari yupo fiti kuelekea mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati Juventus itakaposhuka dimbani leo kuivaa Ajax kwenye hatua hiyo. Ronaldo hajacheza mechi yoyote tangu Machi 25, mwaka huu, kutokana na majeraha ya paja jambo ambalo lilizua hofu kuwa huenda ataikosa mechi hiyo ya leo. **PICHA: MTANDAO**

## Zahera aigeukia TFF kiwango kibovu Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yake kupata ushindi dhidi ya African Lyon kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema hafurahishwa na namna timu yake inavyocheza, lakini lawama hizo akizielekeza kwa Bodi ya Ligi ya TFF kutokana na ratiba kutokuwa rafiki kwao.

Yanga juzi ikiwa katika uwanja wake wa nyumbani, CCM Kirumba jijini Mwanza, iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, shukrani zikimwendea Heritier Makambo aliyetupia mabao yote mawili.

Hata hivyo, pamoja na ushindi huo Zahera, alisema juzi kuwa Yanga imekuwa ikishindwa kucheza soka la kuvutia licha ya kupata matokeo mazuri kutokana na ratiba kuwa karibu na timu kutumia muda mrefu kusafiri jambo linalowachosha wachezaji wake.

"Wachezaji wamekuwa wakisafiri umbali mrefu na wanakuwa na siku moja tu ya kupumzika kabla ya kushuka uwanjani baada ya safari ndefu, kimwili wanakuwa wamechoka," alisema na kutolea mfano:

"Tutacheza dhidi ya Azam Uwanja wa Taifa Aprili 29 na tarehe moja mwezi unaofuata tunatakiwa kushuka uwanjani [Uwanja wa Samora, Iringa] kucheza mechi ya nusu fainali ya Kombe ya FA dhidi ya Lipuli."

Aidha, Zahera alieleza kutofurahishwa na namna ambavyo baadhi ya timu kubakiza mechi tano, huku wao na Azam FC wakibakiza nane, wakati Simba ikiwa na michezo 16 mkononi kabla ya ligi hiyo kufikia ukiongoni.

Yanga inaongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 71 baada ya kushuka dimbani mara 30 sawa na Azam FC iliyopo nafasi ya pili ikiwa na alama 63, wakati Simba iliyocheza mechi 22 ina pointi 57.

# Simba yapambana nje ndani

## ●●● Aussems yeye uwanjani, viongozi wakomaa na Caf, waepuka hujuma, kuifuata Mazembe na pipa lao Ijumaa...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI uongozi wa Simba ukilikomalia Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kwa kitendo cha kubadilishiwa waamuzi wa mechi yao ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya TP Mazembe, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Patrick Aussems, yeye kazi yake ni moja tu, kukiandaa kikosi hicho kupambana uwanjani na ameweka wazi kwamba ubora walionao kwa sasa unawapa matumaini ya kushinda na kufika mbali zaidi.

**Awali, Caf ilitangaza mechi hiyo itakayochezwa Jumamosi mjini Lubumbashi, itachezeshwa na waamuzi kutoka Ethiopia ambao ni Bamlak Tessema Weyesa, Temesgin Samuel Atango na Gilbert Cheruiyot, huku mwamuzi wa akiba akiwa ni Mkenya Peter Waweru.**

Lakini Kamati ya Waamuzi ya Caf, juzi iliitaarifu Simba kwa barua kuwapo kwa mabadiliko ya waamuzi ambapo sasa watakaochezesha mechi hiyo itakayopigwa Jumamosi nchini Congo kuwa ni Janny Sikazwe ambaye atasaidiwa na Romeo Kasengele, Audrick Nkole wote kutoka Zambia, huku mwamuzi msaidizi namba moja akiwa ni Berhe Tesfagiorgis O'michael wa Eritrea.

Hatua ambayo uongozi wa Simba chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Crescentius Magori, tayari wameandika barua Caf kupinga na wakitaka ufafanuzi wa sababu ya kiufundi iliyotolewa katika mabadiliko hayo ni ipi.

Hata hivyo, kikosi cha wachezaji 23 na viongozi saba wa Simba kitaondoka nchini keshokutwa asubuhi kuelekea Lubumbashi, DR Congo tayari kuwavaa wenyeji wao TP Mazembe, huku Kocha Mkuu, Patrick Aussems akieleza ana matumaini makubwa kwa ubora wao uliowafikisha katika hatua hiyo waliyopo.

Mabingwa mara tano wa Ligi ya Mabingwa Afrika, TP Mazembe watakaribisha Simba katika mchezo huo wa marudiano baada ya kulazimisha sare tasa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa.

Aussems aliliambia gazeti hili jana kuwa waliingia katika mashindano hayo ya mwaka huu wakiwa wamejiandaa na waliamini wanaweza kufika mbali.

"Malengo yetu msimu huu ilikuwa ni kutinga hatua ya makundi, lakini kutokana na ubora ambao tumekuwa tukiuonyesha kadri tunavyosonga mbele, tumeonekana tunastahili kufika hapa tulipo, na bado tuna nafasi ya kusonga mbele endapo mambo yatakwenda kama tulivyopanga," alisema Aussems.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa anajivunia kikosi chake kimeimarika na kinacheza kwa kufuata maelekezo kwa asilimia kubwa.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa timu hiyo, Haji Manara, alisema kikosi cha timu yao kitaondoka Ijumaa asubuhi kwa ajili ya kuwafuata TP Mazembe na maandalizi ya safari hiyo yamekamilika.

Manara alisema kuwa majina ya wachezaji watakaosafiri yatajulikana baada ya mazoezi ya leo, lakini akimtaja beki wa kati wa kimataifa, Paschal Wawa nafasi yake ya kwenda ni ndogo kutokana na majeraha aliyoyapata katika mchezo uliopita.

Alisema pia Simba imeandaa utaratibu wa kusafiri na mashabiki na kwa njia ya ndege maalum ya kukodi na kwamba gharama yake ni Dola za Marekani 500 kwa mtu mmoja, huku Dola za Marekani 200 kwa usafiri wa basi wakati gharama ya kulipia visa ni Dola za Marekani 50.

Aliongeza kuwa hadi jana mchana Caf ilikuwa halijajibu chochote kuhusiana na malalamiko yao waliyoyawasilisha kuhusiana na mabadiliko ya waamuzi watakaochezesha mechi hiyo ya Jumamosi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >